UNIVERSITY of RWANDA

**KOLEJI YA ELIMU**

# MCHANGO WA TEHAMA KATIKA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA STADI YA KUZUNGUMZA KATIKA LUGHA YA KISWAHILI: MFANO WA SHULE TEULE ZA SEKONDARI NYAMASHEKE-RWANDA

**NA**

**NIYOBUHUNGIRO EMMANUEL**

**218001026**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA MAHITAJI YA SHAHADA YA UMAHIRI WA ELIMU KATIKA KISWAHILI NA ELIMU KATIKA CHUO KIKUU CHA RWANDA, NDAKI YA ELIMU**

**OKTOBA, 2024**

# IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, **Niyobuhungiro Emmanuel,** ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu ya asili na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada yoyote.

Niyobuhungiro Emmanuel

(Mwanafunzi)

Tarehe: 10/10/2024

## ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa tasnifu yenye mada **"Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza katika Lugha ya Kiswahili: Mfano wa Shule Teule za Sekondari, Nyamasheke- Rwanda,"** iliandaliwa chini ya usimamizi wake na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri wa Elimu katika Kiswahili na Elimu.

Dkt. Wallace Kapele Mlaga (PhD)

(Msimamizi)

Tarehe: 10/10/2024

# SHUKRANI

Shukrani za dhati ziende kwa Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai na uwezo wa kukamilisha masomo yangu. Pili, napenda kumshukuru msimamizi wangu, Dkt. Wallace Kapele Mlaga, kwa ushauri wake mzuri na mwongozo wa kitaalamu ambao uliniwezesha kukamilisha tasnifu hii kwa mafanikio. Bila jitihada zake na ujuzi wake wa thamani, nisingeweza kufikia hatua hii.

Ninamshukuru sana mke wangu, Vumiliya Francine, kwa mchango wake mkubwa katika safari yangu ya masomo. Ushirikiano wake na msaada wake umenipa nguvu na ujasiri wa kufikia malengo yangu. Ninathamini upendo na uvumilivu wake, ambao umenisaidia kuvuka changamoto zote. Asante kwake kwa kuwa nguzo yangu imara na mshirika wa maisha yangu.

Shukrani za dhati kwa wazazi wangu, Sebiziga Mathieu na Uwimana Margueritte, kwa malezi yao makini na msaada wao usio na kifani. Ninawatakia baraka tele na furaha maishani mwao. Pia, ninatoa shukrani kwa ndugu zangu wote kwa upendo na kujitolea kwao katika safari yangu ya masomo. Msaada wao umenisaidia sana kufikia malengo yangu, na ninawapenda sana. Mungu awajalie maisha marefu yenye fanaka na neema zake ziwaendee daima.

# TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabaruku kwa mke wangu mpendwa, Vumiliya Francine, ambaye msaada wake na uvumilivu wake umekuwa nguzo muhimu katika safari yangu ya masomo. Pia, ninawashukuru sana wazazi wangu, Sebiziga Mathieu na Uwimana Marguerite, kwa malezi yao makini na msaada wao usio na kifani ambao umenisaidia kufikia malengo yangu. Ninawathamini na ninawapenda sana kwa michango yao ya thamani katika maisha yangu.

# IKISIRI

Utafiti uliofanyika ulikuwa na lengo la jumla la kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Malengo mahususi ya utafiti yalikuwa mawili. Kwanza, kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Pili, kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Kwa kutimiza malengo haya, utafiti uliegemezwa katika Nadharia ya Kuunganishwa. Wango la utafiti lilihusisha wakurugenzi, wakuu wa masomo, wanafunzi na walimu katika shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke. Sampuli ya utafiti ilihusisha wanafunzi 115 wa kidato cha sita. Wanafunzi hawa waliteuliwa kwa makusudi kwa kuwa ndio ambao wana umahiri katika Kiswahili ukilinganisha na wanafunzi wa vidato vya chini. Aidha, sampuli ilihusisha walimu 5, wakurugenzi 5 na wakuu wa masomo 5 ambao waliteuliwa kwa kutumia usambulishaji lengwa. Ili kukusanya data, mbinu za usaili, uchambuzi matini na ushuhudiaji zilitumiwa. Aidha, matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba TEHAMA ina nafasi kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili. Kwanza, TEHAMA hurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza. Pili, TEHAMA inawezesha walimu na wanafunzi wa lugha kupata zana za kisasa za kufundishia stadi za kuzungumza. Tatu, TEHAMA ina nafasi katika kuongeza hamasa ya kuzungumza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Nne, TEHAMA inatumiwa ili kuwezesha wanafunzi kuwasiliana na wazawa wa Kiswahili kwa urahisi. Hata hivyo, matokeo yanaonesha changamoto katika matumizi ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na uhaba wa zana za TEHAMA na ukosefu wa ujuzi wa kutumia programu za TEHAMA. Ili kuepukana na changamoto hizi, tunapendekeza kuandaa semina kwa walimu wa Kiswahili, kupanga ratiba ya matumizi ya chumba cha kompyuta, kuongeza zana za TEHAMA kwa ajili ya kufundisha stadi za kuzungumza Kiswahili. Mwisho, utafiti umetoa miongozo ya utumiaji wa michezo ya KiTEHAMA na mikutano ya video mtandaoni na utumiaji wa programu za mtandaoni za kufundishia na kujifunzia stadi za kuzungumza Kiswahili.

**Maneno ya Msingi**: *TEHAMA, Ufundishaji na Ujifunzaji, Stadi ya Kuzungumza*

# YALIYOMO

IKIRARI NA HAKIMILIKI ........ ii
ITHIBATI YA MSIMAMIZI ........ iii
SHUKRANI ........ iv
TABARUKU ........ v
IKISIRI ........ vi
YALIYOMO ........ vii
ORODHA YA VIFUPISHO ........ xii
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ........ 1
1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 1
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti ........ 5
1.4 Malengo ya utafiti ........ 5
1.4.1 Lengo la Jumla ........ 5
1.4.2 Malengo Mahususi ........ 5
1.5 Maswali ya Utafiti ........ 6
1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 6
1.7 Mawanda ya Utafiti ........ 7
1.7.1 Mawanda ya Kimaudhui ........ 7
1.7.2 Mawanda ya Kijiografia ........ 8
1.7.2 Mawanda ya Kimuda ........ 8
1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake ........ 8

1.9 Mpangilio wa Utafiti ........ 9

1.10 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ........ 9

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO ........ 10

2.1. Utangulizi ........ 10

2.2 Stadi ya Kuzungumza ........ 10

2.3 Matatizo ya Ufundishaji wa Stadi ya Kuzungumza ........ 11

2.4 Utumiaji wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Stadi ya Kuzungumza ........ 12

2.5 Mbinu za Ufundishaji wa Stadi ya Kuzungumza ........ 13

2.5.1 Utumiaji wa Michezo ya Uigizaji katika Ufundishaji wa Stadi ya Kuzungumza ........ 14

2.5.2 Utumiaji wa Midahalo katika Ufundishaji wa Stadi ya Kuzungumza ........ 15

2.6 Nafasi ya TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza ........ 16

2.6.1 TEHAMA na Stadi za Kuzungumza ........ 17

2.6.2 TEHAMA na Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kuzungumza Kiswahili ........ 22

2.7 Mbinu za Utumiaji wa TEHAMA katika Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza ........ 24

2.7.1 Utumiaji wa Michezo ya KiTEHAMA ........ 25

2.7.2 Utumiaji wa Mikutano ya Video Mtandaoni ........ 26

2.7.3 Utumiaji wa Programu za Mtandaoni za Kufundishia na Kujifunzia Stadi za Kuzungumza ........ 27

2.7.4 Utumiaji wa Teknolojia ya Utambuzi wa Sauti ........ 28

2.8 Mapengo ya Utafiti Tangulizi ........ 30

2.9 Nadharia ya Utafiti ........ 31

SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI ........ 33

3.1 Utangulizi ........ 33
3.2 Paradima ya Utafiti ........ 33
3.3 Usanifu wa Utafiti ........ 34
3.4 Eneo la Utafiti ........ 35
3.5 Wango na Sampuli ya Utafiti ........ 35
3.5.1 Wango la Utafiti ........ 35
3.5.2 Sampuli ya Utafiti ........ 36
3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 37
3.6.1 Mahojiano ........ 37
3.6.2 Ushuhudiaji ........ 37
3.6.3 Uchambuzi wa Matini ........ 38
3.7 Aina za Data Zilizokusanywa ........ 38
3.7.1 Data za Msingi ........ 38
3.7.2 Data za Upili ........ 39
3.8 Vifaa vya Utafiti ........ 39
3.9 Uchanganuzi wa Data ........ 39
3.10 Itikeli ya Utafiti ........ 39
3.11 Uhalali na Uthabiti wa Utafiti ........ 40
3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu ........ 41
SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI ........ 42
4.1 Utangulizi ........ 42
4.2 Nafasi ya TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza ........ 42
4.2.1 TEHAMA Hurahisisha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kuzungumza ........ 42

4.2.2 TEHAMA Huwezesha Upanikanaji Zana za Kisasa za Kufundishia Stadi za Kuzungumza ........ 46

4.2.3 TEHAMA Huongeza Hamasa ya Kuzungumza Kiswahili ........ 49

4.2.4 TEHAMA Huwezesha Wanafunzi Kuzungumza na Wazawa wa Kiswahili ........ 51

4.3 Miongozo ya Utumiaji wa TEHAMA katika Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili ........ 52

4.3.1 Utumiaji wa Michezo ya KiTEHAMA ........ 53

4.3.2 Utumiaji wa Mikutano ya Video Mtandaoni ........ 55

4.3.3 Utumija wa Programu za Mtandaoni za Kufundishia na Kujifunzia Stadi za Kuzungumza ........ 57

4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne ........ 58

SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 59

5.1 Utangulizi ........ 59

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........ 59

5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza ........ 59

5.2.2 Lengo Mahususi la Pili ........ 60

5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti Iliyotumika ........ 60

5.4 Hitimisho ........ 61

5.5 Mapendekezo ........ 62

5.5.1 Mapendekezo kwa Wanafunzi ........ 62

5.5.2 Mapendekezo kwa Walimu wa Kiswahili ........ 62

5.5.3 Mapendekezo kwa Viongozi wa Shule ........ 62

5.5.4 Mapendekezo kwa Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda ........ 63

5.5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ........ 63
5.6 Muhtasari wa Sura ya Tano ........ 63
MAREJELEO ........ 64
VIAMBATISHO ........ 72
Kiambatisho I. Mwongozo wa Usaili kwa Walimu wa Kiswahili ........ 72
Kiambatisho II. Mwongozo wa Usaili kwa Wakuu wa Masomo na Wakurugenzi ........ 73
Kiambatisho III. Mwongozo wa Ushuhudiaji ........ 74
Kiambatisho IV. Mwongozo wa Uchanganuzi Matini kuhusu Mwongozo wa Utumiaji wa TEHAMA katika Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili 75
Kiambatisho V. Idhini ya Itikeli ya Utafiti ........ 76
Kiambatisho VI. Barua ya Chuo ya Kukusanya Data ........ 77
Kiambatisho VII. Kibali cha Wilaya cha Kukusanya Data ........ 78
Kiambatisho VIII. Mpango Kazi wa Utafiti ........ 79
Kiambatisho IX. Ripoti ya Mfanano ........ 80

# ORODHA YA VIFUPISHO

**Dkt:** Daktari

**ES:** Ecole Secondaire

**GS**: Groupe Scholaire

**Khj**: Keshatajwa hapo juu

**TEHAMA**: Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**Whj**: Wameshatajwa hapo juu

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Sura ya kwanza inatoa taarifa za msingi kuhusu utafiti uliofanyika. Sura ya kwanza ina sehemu nyingine ndogo. Sehemu hizo ni kama vile utangulizi, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti, mpangilio wa utafiti na muhtasari wa sura ya kwanza.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Neno TEHAMA ni kifupisho cha "Teknolojia ya Habari na Mawasiliano", na linahusu matumizi ya teknolojia katika usambazaji wa habari na mawasiliano (Miltenoff, 2004). Kwa mujibu wa Negoescu na Bastina-Bratu (2016), TEHAMA inajumuisha mifumo yote ya kiteknolojia inayotumika kutengeneza, kuhifadhi, kuchakata na kusambaza habari. Pia, TEHAMA inahusiana na njia za mawasiliano kama vile simu, redio au televisheni na inachangia katika upatikanaji wa maandishi, video na ishara za video ambazo zinaweza kusafirishwa duniani kote kupitia taarifa za kidijiti. Kulingana na Bilyalova (2016), TEHAMA kwa ujumla inajumuisha matumizi ya vifaa vya kidijiti na programu mbalimbali zinazohusiana moja kwa moja na kompyuta.

Vifaa na programu hizi ni pamoja na projekta, blogu mbalimbali, kamusi za mtandaoni, vitabu vya mtandaoni, tovuti, michezo ya mtandaoni, Yutube, Watsapu, Instagramu, Twita, maandishi na sauti, baruapepe na nyinginezo (Bilyalova, khj; Billon, Marco & Lera-Lopez, 2017; Ahmadi, 2018, & Mofareh, 2019). Kutokana na meelezo haya, TEHAMA inaweza kufasiliwa kama jumla ya teknolojia inayotumika kwa kuwasilisha, kuhifadhi na kusambaza habari kwa kutumia vifaa vya kidijiti kama kompyuta, simu za mkononi, mitandao ya kijamii na programu mbalimbali.

Kulingana na Lechman, Kutrzeba na Mustakoski (2020), TEHAMA inachukua jukumu muhimu katika maendeleo ya jamii duniani. Watu wametumia teknolojia hii kwa kiasi kikubwa katika kufanikisha mawasiliano muhimu katika maeneo mbalimbali kama vile siasa, biashara, uchumi, michezo, elimu na mambo mengine. Ratheeswari (2018) pia anasisitiza kuwa katika uwanja wa elimu, TEHAMA imekuwa ikifanya kazi muhimu katika mchakato wa kufundisha na kujifunza mambo mbalimbali yanayohusu jamii, kama vile kufundisha na kujifunza lugha ya pili au lugha ya kigeni.

Hii inaonesha kuwa, walimu na wanafunzi wamejitahidi kubadilika na kuzingatia mahitaji ya kisasa ya jamii, hasa yale yanayohusiana na matumizi ya sayansi na teknolojia. Hii imefanya iwezekane kwa walimu kutumia TEHAMA darasani kwa lengo la kufundisha kwa ufanisi zaidi na kwa weledi, huku wakilenga kukidhi mahitaji ya wanafunzi (Bratu na Negoescu, 2016).

Ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA umekuwa ukitekelezwa kwa mafanikio katika masomo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na masomo ya sayansi na masomo ya sanaa. Hii imeleta maendeleo makubwa katika sekta ya elimu. Kama inavyoelezwa na Ahmadi (2018), njia ambayo mwalimu anatumia darasani ina jukumu muhimu katika kusaidia mchakato wa ujifunzaji wa lugha. Katika masomo ya sanaa, kujifunza lugha ya kigeni ni mojawapo ya maeneo ambayo TEHAMA imekuwa ikitumika kwa mafanikio. Wanafunzi wamekuwa wakijifunza kwa kutumia kompyuta kama chombo muhimu cha kutoa maarifa darasani. Hii inaonyesha jinsi TEHAMA inavyoweza kuimarisha mchakato wa kujifunza na kufundisha, hasa katika maeneo ya lugha na sanaa.

Whelan (2008) na Akram, Abdelrady, Al-Adwan & Ramzan (2022) wanasisitiza kuwa matumizi ya TEHAMA huwezesha walimu kufikia vyanzo mbalimbali vya maarifa kwa haraka na kwa usahihi. Vilevile, wanaeleza kuwa vyanzo hivyo vya maarifa vinawachochea wanafunzi kujifunza zaidi. Kulingana na melezo haya, TEHAMA imeleta mageuzi katika uwanja wa elimu kwa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo mbalimbali, kukuza ufundishaji wa stadi za lugha ya pili na kuongeza motisha kwa wanafunzi kupitia upatikanaji rahisi wa vyanzo vya maarifa na mawasiliano kwa walimu.

Kwa upande mwingine, Marlina (2018) anasema kwamba stadi za lugha ni uwezo au ujuzi wa kutumia lugha ipasavyo katika kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika. Huu ni ujuzi ambao mtu anahitaji ili kuwasiliana vizuri na kuelewa lugha fulani. Stadi hizi husaidia katika mawasiliano na uwasilishaji wa mawazo, hisia na habari kwa ufanisi kulingana na mazingira tofauti. Lengo la kila mjifunzaji wa lugha yoyote ile ni kuweza kuzimudu stadi hizi zote za lugha (Marlina, khj).

Licha ya umuhimu wa stadi nne za lugha katika kuweza kuwasiliana kwa lugha mahususi, Rao (2019) anabainisha umuhimu wa stadi ya kuzungumza katika ulimwengu huu wa kimataifa. Uwezo wa kuzungumza lugha ni mojawapo ya stadi muhimu zaidi katika mawasiliano ya ufanisi (Rao, khj).

Ingawa kusikiliza, kusoma na kuandika ni muhimu pia, uwezo wa kuzungumza unatoa jukwaa la moja kwa moja la kuwasiliana na watu kutoka tamaduni tofauti na kuelewa maoni yao kwa urahisi. Kupitia kuzungumza, mtu anaweza kubadilishana mawazo, kuelezea hisia na kufikisha ujumbe wake kwa njia inayoeleweka na kuvutia (Rao, khj). Hii inafanya kuzungumza kuwa msingi muhimu katika kuimarisha uhusiano na kujenga uelewa wa pamoja katika ulimwengu ambao mawasiliano ya kimataifa ni muhimu sana. Kwa hiyo, ufundishaji wa lugha ni lazima utilie mkazo ukuzaji wa stadi ya kuzungumza ambayo ni msingi wa mawasiliano.

Licha ya umuhimu wa stadi ya kuzungumza katika mchakato wa kujifunza lugha, mara nyingi walimu wanapofundisha lugha, hawaweki mkazo katika stadi ya kuzungumza, ijapokuwa stadi hii ni msingi muhimu katika kufikia umilisi wa lugha (Kurum, 2016). Wakati mwingine, umakini wa mafundisho huwekwa zaidi katika stadi za kuandika na kusoma, huku stadi ya kuzungumza ikapuuzwa au ikapewa nafasi ndogo (Qasserras, 2023). Hii inaweza kusababisha upungufu katika uwezo wa wanafunzi kuelewa lugha, kubaini matumizi ya lugha na kushiriki katika mawasiliano kwa ufanisi. Kwa hiyo, upuuzaji wa stadi ya kuzungumza, huwazuia wanafunzi kuweza kuwasiliana kwa ufasaha kwa kutumia lugha lengwa.

Kulingana na Ahmadi (2018), imeonekana kwamba idadi kubwa ya wanafunzi wa lugha ya pili inakabiliwa na upungufu katika stadi ya kuzungumza, na hii inaathiri vibaya ufanisi wao katika kufikia umilisi wa lugha lengwa. Kutokuwa na uwezo wa kuzungumza vizuri, kunaweza kusababisha kukosekana kwa ujasiri katika mawasiliano ya lugha (Akram, Abdelrady, Al-Adwan & Ramzan, 2022). Jambo hili huwaathiri wanafunzi na huwazuia kuelewa ujumbe unaotolewa. Pia, jambo husika huazuia wanafunzi kujibu kwa wakati na hudhoofisha uwezo wa wanafunzi wa kutumia lugha lengwa kwa kuzingatia muktadha wa kijamii. Maelezo ya Ahmadi (khj) & Akram, Abdelrady, Al-Adwan & Ramzan (khj) yanaonesha kwamba, idadi kubwa ya wanafunzi wa lugha ya pili wanakosa stadi ya kuzungumza na jambo hili huathiri vibaya umilisi wao wa lugha lengwa.

Kwa lengo la kukuza stadi za lugha miongoni mwa wanafunzi wa lugha ya pili, watafiti tofauti wamebainisha TEHAMA kama nyenzo bora inayoweza kutumiwa katika ukuzaji wa stadi hizo miongoni mwa wanafunzi wa lugha ya pili ikiwemo stadi ya mawasiliano. Kwa mfano, kulingana na Kumar & Tammelin (2014), stadi ya kuzungumza katika kujifunza lugha inaweza kufundishwa kwa ufanisi zaidi kupitia matumizi ya TEHAMA.

Vifaa vya TEHAMA kama vile mikutano ya mtandaoni, programu za mazungumzo na zana za mawasiliano mtandaoni hutoa fursa kwa wanafunzi ya kujieleza katika lugha lengwa, kuwasiliana na wengine na kushiriki katika majadiliano ya lugha lengwa. Zana hizi za TEHAMA husaidia kuunda mazingira halisi ambayo wanafunzi wanaweza kujifunza na kufanya mazoezi ya ujuzi wao wa kuzungumza. Aidha, zana hizi zinawezesha mwingiliano wa moja kwa moja na mazungumzo ya lugha kwa njia inayowafanya wahusika wajisikie kama wapo katika mazingira halisi ya mazungumzo (Kumar & Tammelin, whj). Hii inaweza kuchangia sana katika kuboresha stadi yao ya kuzungumza katika lugha ya pili au lugha ya kigeni. Hapa ikumbukwe kwamba utafiti wa Kumar & Tammelin (whj) umejikita sana kwenye matumizi ya TEHAMA katika ukuzaji wa stadi ya kuzungumza Kiingereza.

Zaidi ya hayo, tafiti mbalimbali zimebainisha kwamba TEHAMA imetumika ili kufanikisha ujifunzaji wa lugha ya pili. Utafiti wa Ibrahim (2016) unaonesha kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni kwa kutumia TEHAMA umefanyika zaidi kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiingereza kama lugha ya pili au ya kigeni. Aidha, Billon, Marco & Lera-Lopez (2017) anaonesha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa lugha ya kigeni hususan Kiingereza. Vilevile, Bilyalova (2016) anathibitisha kuwa TEHAMA imekuwa ikitumiwa katika mchakato wa kujifunza lugha za kigeni kama vile Kiingereza. Kwa kuongezea, Chapelle, & Sauro, (2017) anaonyesha kuwa TEHAMA imetumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha chache za Ulaya kwa wanafunzi wanaojifunza lugha za kigeni.

Isitoshe, kuna watafiti tofauti wanaojadili mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Kevogo (2017) amezungumzia kwa kina jinsi TEHAMA inavyochangia katika mchakato wa ufundishaji wa Kiswahili kwa ujumla. Msigwa (2019) na Vincent & Msigwa (2021) wameelezea jinsi lugha ya Kiswahili imeingizwa katika mfumo wa TEHAMA na kujadili changamoto zinazojitokeza katika muktadha huo.

Hata hivyo, licha ya maelezo yaliyotolewa na watafiti tofauti, bado, kuna changamoto kadhaa ambazo zinahitaji kushughulikiwa ili kufanikisha matumizi sahihi na yenye tija ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Mojawapo ya changamoto hizo ni hizi zifuatazo. Mosi, baadhi ya tafiti za hapo awali, zilijikita katika lugha ya Kiingereza ambayo si sawa na lugha ya Kiswahili.

Pili, idadi kubwa ya tafiti za hapo awali, zimeonesha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa Kiingereza na Kiswahili kwa ujumla. Kwa kuwa stadi ya kuzungumza ambayo ni kitovu cha umilisi wa lugha. Sisi tulipata shauku ya kufanya utafiti wetu ili kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Uwezo wa kuzungumza lugha ni mojawapo ya stadi muhimu zaidi katika mawasiliano ya ufanisi (Rao, 2019). Aidha, licha ya Kumar & Tammelin (2014) kusema kwamba stadi ya kuzungumza inaweza kufundishwa vema kwa kutumia TEHAMA. Idadi kubwa ya wanafunzi wa lugha ya pili wanakosa stadi ya kuzungumza na jambo hili huathiri vibaya umilisi wao wa lugha lengwa (Ahmad, 2018; Akram, Abdelrady, Al-Adwan & Ramzan, 2022). Hivyo basi, tulipata shauku ya kufanya utafiti ili tuchunguze mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

### 1.4 Malengo ya utafiti

Utafiti ulilenga kutimiza lengo la jumla moja na malengo mahususi mawili.

#### 1.4.1 Lengo la Jumla

Lengo la jumla lilikuwa kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

#### 1.4.2 Malengo Mahususi

Utafiti ulikusudia kutatimiza malengo mahususi mawili ambayo ni haya yafuatayo:

i) Kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda

ii) Kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda

### 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti ulitarajia kujibu maswali mawili. Maswali hayo ni pamoja na:

i) Je, TEHAMA ina nafasi ipi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda?

ii) Je, ni miongozo gani ya kutumia TEHAMA inaweza kuundwa ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda?

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti uliofanyika ulilenga kuchunguza jinsi TEHAMA inavyochangia katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule katika Wilaya ya Nyamasheke, nchini Rwanda. Kama inavyoelezwa na Akram, Abdelrady, Al-Adwan & Ramzan (2022) na Ghavifekr & Rosdy (2015), TEHAMA ina jukumu muhimu katika kuimarisha mchakato wa ujifunzaji wa lugha kwa kutoa zana za mazoezi, fursa za kuwasiliana kwa lugha halisi na ufikiaji wa vyanzo mbalimbali vya kujifunza. Hii inaweza kuchangia katika kukuza ushiriki na ufasaha wa lugha. Kwa hiyo, matokeo yake utafiti yatakuwa na umuhimu mkubwa kwa wanafunzi, walimu, watafiti wajao na wadau wa elimu.

Mosi, yatakuwa na mchango muhimu katika kuboresha elimu kwa wanafunzi wa shule za sekondari katika wilaya ya Nyamasheke, nchini Rwanda. Leo hii, TEHAMA imekuwa sehemu muhimu ya maisha yetu. Kwa hiyo, kuzingatia jinsi inavyoweza kutumika kwa ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ni jambo la msingi.

Kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya kimataifa inayokua kwa kasi, kuwa na stadi za kuzungumza Kiswahili kunaweza kutoa fursa nyingi kwa wanafunzi. Hata hivyo, matokeo ya utafiti yatachangia katika kuboresha uwezo wa wanafunzi wa kuzungumza kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

Pili, yatakuwa na umuhimu mkubwa kwa walimu wa Kiswahili kwani utasaidia kubainisha nafasi ya TEHAMAkatika kuboresha stadi ya kuzungumza Kiswahili. Zaidi ya hayo, matokeo ya utafiti wetu yatatoa mwanga kuhusu mbinu bora za utumiaji wa TEHAMA katika mchakato wa

kufundisha na kujifunza stadi ya kuzungumza Kiswahili. Matokeo ya utafiti yatawezesha walimu kupata ufahamu wa kina kuhusu jinsi ya kutekeleza matumizi ya TEHAMA kwa ufanisi katika darasa la Kiswahili, kuongeza ufanisi wao katika ufundishaji na kuboresha matokeo ya ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza lugha ya Kiswahili. Hii itawasaidia walimu kuunda mazingira bora ya kufundisha ambayo yanachangia katika maendeleo ya wanafunzi katika stadi ya kuzungumza lugha ya Kiswahili.

Tatu, matokeo haya yanatarajiwa kuhamasisha wapangaji wa sera za elimu nchini Rwanda kuongeza bajeti inayotengwa kwa shule za sekondari kwa ajili ya kununua vifaa vya TEHAMA. Hii itasaidia kuboresha mazingira ya kujifunza, kuimarisha upatikanaji wa teknolojia, na kuongeza ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji. Kupitia uwekezaji huu, wanafunzi wataweza kupata maarifa ya kisasa zaidi na kuendana na mahitaji ya ulimwengu wa sasa wa kidigiti.

Nne, matokeo yatakuwa muhimu sana kwa watafiti wajao kwa sababu utatoa mwanga kuhusu jinsi TEHAMA inavyochangia katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili. Kuelewa mchango huu utasaidia utashiriki katika upatikanaji wa marejeleo na pia kutoa mwongozo kuhusu namna ya utumiaji wa TEHAMA kwa ufanisi katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza lugha ya Kiswahili.

Isitoshe, matokeo ya utafiti yatachangia sana katika kuboresha sera za elimu nchini Rwanda, hasa kwa matumizi ya TEHAMA katika kufundisha stadi za kuzungumza. Matokeo haya yatawaonesha walimu mbinu za kisasa za kufundisha kwa kutumia teknolojia, kama vile programu za mazoezi ya matamshi na mazungumzo. Hii itawapa wanafunzi nafasi ya kufanya mazoezi zaidi, kupokea mrejesho wa haraka, na kuimarisha ufasaha wao, hivyo kuongeza uwezo wao wa kushiriki kikamilifu katika mijadala ya kimataifa.

### 1.7 Mawanda ya Utafiti

Mawanda ya utafiti yamegawanyika katika mawanda matatu. Mosi, kuna mawanda ya kimaudhui. Pili, kuna mawanda ya kijiografia. Tatu kuna mawanda ya kimuda.

#### 1.7.1 Mawanda ya Kimaudhui

Kwa kawaida, lugha hujumuisha stadi kuu nne ambazo ni stadi ya kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika. Ingawaje stadi za lugha ni nne, utafiti ulijikita katika ukuzaji wa stadi ya kuzungumza katika lugha ya Kiswahili. Aidha, hata kama kuna mbinu nyingi ambazo zinaweza kutumiwa ili kufundishia na kujifunzia stadi ya kuzungumza, utafiti ujikita kwenye uchunguzaji

wa nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke katika nchi ya Rwanda.

### 1.7.2 Mawanda ya Kijiografia

Kwa mawada ya kijiografia, utafiti ulifanyika katika wilaya ya Nyamasheke nchini Rwanda. Wilaya hii ni wilaya ambayo ina tarafa 15. Tarafa hizo ni: Bushekeri, Bushenge, Cyato, Gihombo, Kagano, Kanjongo, Karambi, Karengera, Kirimbi, Macuba, Mahembe, Nyabitekeri, Rangiro, Ruharambuga na Shangi. Wilaya ya Nyamasheke ni wilaya ambayo iko karibu na mpaka wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hii ina maana kwamba katika wilaya hii kuna idadi kubwa ya wasemaji wa Kiswahili ikilinganishwa na maeneo mengine nchini Rwanda. Aidha, wilaya ya Nyamasheke pia ni miongoni mwa wilaya ambako mradi wa serikali wa kompyuta moja kwa kila mwanafunzi ulianzishwa, hususan katika wilaya zinazopakana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Hii inafanya Nyamasheke kuwa mahali panapofaa katika kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda. Kwa hiyo, utafiti ulifanyika katika shule tano zilizoteuliwa kutoka kwenye tarafa ya Kanjongo, Kagano, Karambi na Macuba. Shule hizo ni pamoja na GS Mbuga, GS Tyazo, ES Tyazo, GS Gitwa na GS Karambi. Madarasa yaliyochaguliwa ni madarasa ya kidato sita kwa kuwa wanafunzi wa madarasa haya ndio wenye umahiri katika uzungumzaji wa Kiswahili.

### 1.7.2 Mawanda ya Kimuda

Utafiti ulilenga kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Kwa hiyo, kuhusiana na mawada ya kijiografia, utafiti ulishughulikiwa kipindi cha wakati cha kutoka kwa mwaka 2022 hadi mwaka 2024.

## 1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Wakati wa kufanya utafiti, mtafiti alikabiliwa na vikwazo tofauti. Kwanza, mtafiti alichelewa kupata kibali cha kukusanya data kutoka chuoni. Kwa kukabilina na kikwazo hiki, mtafiti alikutana na uongozi unaohusika na kuwaelezea kwamba kibali kinahitajika haraka. Baada ya kukutana na uongozi husika, kibali kilitolewa.

Pili, kuna baadhi ya walimu ambao hawakuelewa maswali yaliyokuwa kwenye mwongozo wa usaili. Ili kuepukana na kikwazo hiki, kabla ya kuanza usaili, mtafiti aliwaelezea washiriki wa utafiti kila swali ili waweze kulielewa kwa kina.

Mwisho, wakurugenzi na wakuu wa masomo wote hawakujua lugha ya Kiswahili. Ili kuepuka kikwazo hiki, maswali yaliyokuwa kwenye mwongozo wa uasili yalitafsiriwa katika Kiingereza. Aidha, wakurugenzi na wakuu wa masomo waliruhusiwa kujibu kwa lugha wanayoifahamu zaidi.

### 1.9 Mpangilio wa Utafiti

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza inalenga kutoa maelezo ya awali kuhusu utafiti. Sura ya pili inaelekeza juu ya kukagua vyanzo mbalimbali vya maandiko vinavyohusiana na mada ya utafiti. Sura ya tatu inajumuisha mbinu na njia zitakazotumika katika utafiti. Sura ya nne inachambua na kufafanua matokeo ya utafiti. Hatimaye, sura ya tano, ambayo pia ni sehemu ya mwisho, inatoa muhtasari, suluhisho, na mapendekezo yatakayotokana na matokeo ya utafiti.

### 1.10 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura ya kwanza inatoa muhtasari wa utafiti, ikihusisha utangulizi, usuli wa tatizo, tamko la tatizo, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu, mawanda, vikwazo, mpangilio wa utafiti, na muhtasari wa sura. Sura inayofuata itahusu mapitio ya maandiko.

# SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1. Utangulizi

Sura hii inajikita katika kuangazia mapitio mbalimbali ya maandiko yaliyotumika katika utafiti. Mapitio hayo yamegawanyika katika sehemu zifuatazo: utangulizi, stadi ya kuzungumza, matatizo ya ufundishaji wa stadi za lugha, utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza, mbinu za ufundishaji wa stadi ya kuzungumza, utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji wa stadi ya kuzungumza, mapengo ya utafiti, nadharia ya utafiti, na muhtasari wa sura ya pili.

## 2.2 Stadi ya Kuzungumza

Stadi ya kuzungumza ni uwezo wa kuzungumza na watu kwa ufanisi (Hussain, 2017). Stadi ya kuzungumza ni mhimili muhimu sana katika mawasiliano ya kibinadamu. Inajumuisha ufahamu wa sarufi na msamiati, uwezo wa kusikiliza, uwezo wa kutamka, matumizi ya lugha ya mwili na ujasiri mbele ya watu, iwe ni mbele ya watu unaowajua au wageni (Thornbury, 2005). Stadi hii inaleta uwezo wa kushirikisha wengine kwa ufanisi, kuhakikisha ujumbe unafikishwa kwa ufasaha, na kujenga mawasiliano ya kina na watu unaozungumza nao. Maelezo haya yanaonesha kwamba stadi ya kuzungumza ni stadi ambayo inamwezesha mtu kuwasilisha fikra na mawazo yake kwa ufasaha.

Kulingana na umuhimu wake katika mawasiliano, stadi ya kuzungumza inasaidia watu kujenga uhusiano na wenzao (Rao, 2018). Kulingana na Garcia (2021), uwezo wa kuwasiliana vizuri unaweza kuleta maelewano, kuzuia migogoro, na kukuza ushirikiano mzuri katika maeneo mbalimbali ya maisha yetu, iwe ni katika kazi, mahusiano ya kibinafsi, au shughuli za kijamii. Watu wenye stadi bora za kuzungumza mara nyingi hufanikiwa zaidi katika maisha yao, kwa kuwa wanaweza kujenga mahusiano mazuri na kuvutia watu kwa urahisi zaidi. Hivyo basi, uwezo wa kuzungumza kwa ufasaha unakuwa ni chombo muhimu sana katika kutimiza malengo yetu na kufanikiwa katika maisha. Licha ya maelezo haya, Rao (khj) & Garcia (khj) hawakufanya tafiti kuhusu stadi ya kuzungumza Kiswahili. Kwa hiyo sisi, tutajikita katika stadi za kuzungmza Kiswahili kwa kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi husika.

Kwa mujibu wa Lightbown & Spada (2006), ufundishaji wa stadi ya kuzungumza ni muhimu sana kwani stadi hii huathiri moja kwa moja mafanikio ya wanajamii katika maisha yao. Kupitia stadi hii, watu wanaweza kujenga uhusiano mzuri na wengine, kufikisha ujumbe kwa ufasaha na kuwasiliana kwa ufanisi katika maeneo mbalimbali ya maisha yao, iwe ni kazi, familia au jamii kwa ujumla (Garcia, 2021). Garcia (khj) anasisistiza kwamba ukosefu wa stadi za kuzungumza unaweza kusababisha matatizo ya mawasiliano, migogoro na hata kuzuia fursa za kujitokeza katika maisha. Hii ina maana kwamba, ni muhimu kwa jamii kuwekeza katika ufundishaji wa stadi hii ili kuwawezesha wanajamii kufanikiwa katika maeneo yote ya maisha yao. Kwa hiyo, utafiti wetu ulikusudia kuchunguza nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

**2.3 Matatizo ya Ufundishaji wa Stadi ya Kuzungumza**

Matatizo yanayokumba ufundishaji wa stadi ya kuzungumza ni mengi na yanaweza kuathiri uwezo wa wanafunzi katika kujifunza lugha lengwa kwa ufanisi (Nanai, 2023). Mojawapo ya changamoto kuu ni ukosefu wa zana za kufundishia na kujifunzia (Zake & Akinyemi, 2020). Mara nyingi, mazingira ya kujifunzia hayana vifaa vya kutosha vinavyoweza kuwawezesha wanafunzi kujifunza na kukuza stadi zao za kuzungumza. Hii inaweza kudhoofisha uwezo wao wa kuelewa na kutumia lugha ya lengwa katika mazungumzo ya kila siku (Zake & Akinyemi, whj). Hali hii ilitochochea kufanya utafiti ili tuchunguze ikiwa ukosefu wa zana za kufundishia na kujifunzia ni mojawapo ya matatizo ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili katika shule za ekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

Pili, uhaba mkubwa wa walimu wenye uwezo wa kufundisha stadi ya kuzungumza huweza kukabili ufundishaji wa lugha. Kulingana na Holmqvist (2019), walimu wengi wanaweza kuwa na ujuzi mzuri wa lugha ya lengwa, lakini wakawa hawajui mbinu au mazoea bora ya kufundisha stadi hii ya kuzungumza lugha hiyo. Hii inaweza kusababisha matumizi ya mbinu duni za ufundishaji, ambazo hazitoi fursa za kutosha kwa wanafunzi kujieleza kwa ufasaha au kujiamini katika mazungumzo yao. Kulingana na maelezo haya, tuliamua kufanya utafiti ili kuchunguza hali ilivyo katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa kubainisha mchango wa TEHAMA katika kukabiliana na tatizo yauhaba wa walimu wenye uwezo wa kufundisha stadi ya kuzungumza Kiswahili.

Aidha, tatizo jingine linaloweza kukabili ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza ni kusisitizia sana stadi za kusoma na kuandika kuliko stadi ya kuzungumza. Mara nyingi, mitaala inazingatia zaidi kusoma na kuandika kuliko kuzungumza. Hii inaweza kusababisha mazingira ambayo wanafunzi wanapewa nafasi ndogo au hawapewi umuhimu wa kutosha katika kujifunza kuzungumza. Idadi kubwa ya walimu wanapofundisha lugha, huwa hawatilii mkazo stadi ya kuzungumza ingawaje stadi hii ni muhimu katika umilisi wa lugha (Kurum, 2016 & Qasserras, 2023). Hii ndiyo sababu Ahmadi (2018) & Akram, Abdelrady, Al-Adwan & Ramzan (2022) wanasema kwamba idadi kubwa ya wanafunzi wa lugha ya pili wanakosa stadi ya kuzungumza na jambo hili huathiri vibaya umilisi wao wa lugha lengwa.

Kwa hiyo, utafiti wetu ulikusudia kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Hii ni kwasababu TEHAMA ina mchango mkubwa katika ufundishaji wa lugha ya pili (Ibrahim, 2016; Billon, Marco & Lera-Lopez, 2017 na Chapelle, & Sauro,2017).

### 2.4 Utumiaji wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Stadi ya Kuzungumza

TEHAMA ni mbinu inayotumia vifaa vya kielektroniki na kiteknolojia katika uchakataji, usambazaji na uhifadhi wa taarifa (Bilyalova, 2016). Katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza, TEHAMA inaleta fursa pana ya kuboresha mbinu za kufundishia lugha na kusaidia katika maendeleo ya uwezo wa mawasiliano katika lugha husika. Matumizi ya TEHAMA katika elimu yanajumuisha vifaa kama kama kompyuta, simu za mkononi, mitandao ya kijamii, programu za mafunzo na mengineyo. TEHAMA inaleta njia mpya ya kujifunza lugha kwa njia inayotegemea teknolojia na kufungua upeo mpana wa fursa za mawasiliano na kujifunza kwa wanafunzi.

TEHAMA inawapa wanafunzi fursa ya kusikiliza na kuiga sauti na mazungumzo ya wazawa wa lugha na huwezesha wanafunzi kuwa na matamshi sahihi (Idayani & Sailun, 2017). Vifaa kama redio, video na programu za mazungumzo hutoa mifano halisi ya lugha ambayo wanafunzi wanaweza kuiga kwa ufasaha zaidi. Teknolojia inaweza kutumiwa na walimu ili kuwawezesha wanafunzi kujenga ufasaha wao kwa kusikiliza lugha asilia kwa njia ambayo inaweza kuwa ngumu kupatikana katika mazingira ya kawaida ya masomo ya lugha.

Kama wanavyoeleza Idayani & Sailun (whj), matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa lugha huongeza motisha kwa wanafunzi na kuwaongezea hamasa ya kufanya juhudi katika kuelewa lugha hiyo. Wanapopata fursa ya kuwasiliana na kutumia zana za teknolojia, wanachochewa kufanya bidii zaidi katika kujifunza lugha kwa kuiga na kutumia mifano waliyoiona kupitia vyombo vya TEHAMA. Hii inawafanya kuwa na hamasa kubwa zaidi ya kutumia lugha hiyo katika mazingira tofauti.

Kulingana na Chirag (2003), moja ya faida muhimu ya kutumia TEHAMA katika kufundisha stadi ya kuzungumza ni gharama ndogo. Programu, zana za mtandaoni na vifaa vingine vya TEHAMA mara nyingi hupatikana kwa gharama ndogo au hata bure. Hii inaweza kupunguza hitaji la vifaa vingi ghali na kufanya njia hii kuwa rahisi kupatikana katika mazingira mbalimbali ya kujifunzia lugha (Chirag, khj). Kutumia TEHAMA katika kufundisha stadi ya kuzungumza pia inaweza kutoa ufikiaji mpana kwa wanafunzi wanaotaka kuboresha ujuzi wao wa lugha.

Kwa hiyo, matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza huongeza ufanisi wa mchakato wa kujifunza stadi ya kuzungumza lugha na hupunguza gharama za vifaa vya kujifunzia, huku pia yakichochea motisha na hamasa ya wanafunzi katika mchakato huo. Baada ya kupitia maandiko tofauti na kuona kwamba TEHAMA inaweza kuchangia katika ukuzaji wa stadi ya kuzungumza lugha, tulipata shauku ya kufanya utafiti ili tuchunguze mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

### 2.5 Mbinu za Ufundishaji wa Stadi ya Kuzungumza

Lengo kuu la utafiti lilikuwa kuchunguza jinsi TEHAMA inavyochangia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza katika lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, ilikuwa bora kupitia maandiko kuhusu ufundishaji wa stadi ya kuzungumza. Stadi ya kuzungumza inahusu uwezo wa kueleza mawazo, fikra, na taarifa kwa uwazi na ufanisi kupitia mawasiliano ya maneno. Inajumuisha ufasaha, matamshi, sauti na uwezo wa kujieleza kwa mpangilio mzuri wakati wa kuwasiliana na watu wengine (Maulana, Musthafa, & Hayati, 2020). Kwa hiyo, ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza inajumuisha siyo tu matumizi sahihi ya msamiati na sarufi bali pia ishara za kimya kama vile lugha ya kimwili na sauti ili kuwasilisha ujumbe kwa usahihi na kwa ujasiri.

Kulingana na Maulana na wenzake (whj), katika mafundisho ya stadi ya kuzungumza, ni muhimu kwa walimu kutumia mazoezi ya kuzungumza. Mazoezi haya huchangia katika kuwapa mwanga wanafunzi kuhusu jinsi ya kuandaa mawazo yao kwa ajili ya kujieleza. Kupitia mazoezi ya mazungumzo, wanafunzi hupata fursa ya kuboresha uwezo wao wa kuzungumza kwa ufasaha katika lugha wanayojaribu kujifunza. Hii inawasaidia kujenga ujasiri na uwezo wa mawasiliano katika lugha hiyo, wakati wakijifunza jinsi ya kuwasilisha mawazo yao kwa njia inayoeleweka na yenye ufanisi. Kwa hiyo hapo chini ni mapitio ya maandiko kuhusu mbinu za ufundishaji wa stadi ya kuzungumza.

### 2.5.1 Utumiaji wa Michezo ya Uigizaji katika Ufundishaji wa Stadi ya Kuzungumza

Michezo ya uigizaji ni moja wapo ya njia muhimu ya kufundisha stadi ya kuzungumza kwa sababu inawapa wanafunzi uzoefu wa kujifunza kuwasiliana kwa njia ya vitendo (Bhatti, 2021). Mwanafunzi akichukua nafasi ya mhusika mkuu au mdogo katika uigizaji, anapata fursa ya kujifunza jinsi ya kujieleza na kuelewa hisia na mtazamo wa tabia hiyo.

Kwa kufanya hivyo, mwanafunzi hupata ujuzi wa kuwasilisha mawazo yake kwa ufasaha na kujifunza kusikiliza na kuelewa mambo mbalimbali yanayohusu muktadha wa tabia husika. Hii inajenga ujuzi wa mawasiliano, kujiamini na uwezo wa kujieleza kwa njia inayoeleweka kwa hadhira.

Kama inavyoelezwa na (Bhatti, khj), michezo ya uigizaji ni michezo ya kujifanya kama mtu mwingine ambapo wanafunzi wanajifunza kutenda au kuchukua jukumu la mtu mwingine katika hali fulani. Michezo ya uigizaji inaweza kukuza stadi ya kuzungumza kwa kuwaruhusu wanafunzi kutumia lugha yenye viwango vya juu kuliko wangefanya katika hali za kawaida. Michezo hii inawasaidia wanafunzi kujifunza msamiati na lugha mpya kutoka kwa wenzao, kuwasiliana kwa uhuru katika mazingira salama na kuimarisha kushiriki katika hali halisi kama vile kwenye mazungumzo, mijadala, kufanya kazi kwa pamoja, ushirikiano na kujaribu kuwashawishi wengine (Bhatti, khj). Aidha, kupitia michezo ya uigizaji, wanafunzi wanapata fursa ya kuimarisha stadi ya kuzungumza miongoni mwao.

Zaidi ya kuimarisha stadi ya kuzungumza kwa kutumia maneno, michezo ya uigizaji pia husaidia katika kukuza uwezo wa kuonyesha hisia na maoni kwa njia ya kisanii wakati wa mazungumzo (Wulandari, Ayuningtias & Yana, 2019). Wanafunzi wanapojishughulisha na uigizaji, wanajifunza kutumia lugha ishara za kimwili na sauti kwa njia inayowakilisha vyema hisia na

mawazo ya tabia wanayoigiza. Hii inawawezesha kuonyesha kuunganisha maneno na ishara wakati wa kuzungumza jambo ambao ni muhimu sana katika mawasiliano.

Kwa hiyo, michezo ya uigizaji hutoa fursa kwa wanafunzi kujifunza kuwasiliana kwa vitendo, kuonyesha hisia na maoni kwa njia ya kisanii, na hivyo kuimarisha stadi zao za kuzungumza. Maelezo haya yanaonesha kwamba michezo ya uigizaji ina mchango mkubwa katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza lugha ya Kiingereza.

Maelezo husika, yalituchochea kufanya utafiti ili tuchunguze ikiwa michezo ya uigizaji inaweza kushiriki katika ukuzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili. Hivyo basi, utafiti wetu ulikusudia kuchunguza namna ambavyo TEHAMA inaweza kujumuishwa katika utumiaji wa michezo ya uigizaji katika kufundisha stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

**2.5.2 Utumiaji wa Midahalo katika Ufundishaji wa Stadi ya Kuzungumza**

Midahalo ni jukwaa muhimu linalowapa wanafunzi fursa ya kujenga uwezo wao wa kuzungumza katika lugha, suala ambalo ni msingi wa stadi ya kuzungumza (Arung, 2016). Kupitia midahalo, wanafunzi wanajikuta wakijifunza jinsi ya kutumia lugha kwa ufasaha na kuwasiliana waziwazi kuhusu mada mbalimbali. Hii ina maana kwamba, midahalo huwapa wanafunzi nafasi ya kufanya majadiliano kwa kutumia lugha yao wenyewe na kuelewa jinsi ya kujibu maswali au hoja kwa njia inayoeleweka kwa wengine, hivyo kuimarisha uwezo wao wa kuwasiliana kwa ufasaha.

Aidha, kwa mujibu wa Arung (khj), ufundishaji wa stadi ya kuzungumza lugha huweza kufanyika kwa kutumia midahalo kwa kuwa inawapa wanafunzi uwezo wa kufanya maandalizi ya kina kabla ya kuzungumza, jambo ambalo ni muhimu katika kuendeleza stadi yao ya kuzungumza. Kabla ya kushiriki katika midahalo, wanafunzi hulazimika kutafiti na kutayarisha hoja zao, kufanya utafiti kuhusu mada na kuandaa vigezo vya kusaidia hoja zao.

Hii huwawezesha kuwa na ufasaha na ufanisi katika kujieleza na kuhakikisha hoja zao zinathaminiwa na wenzao.

Zaidi ya hayo, kulingana na Bellon (2000), kupitia ufundishaji wa stadi za kuzungumza kwa kutumia midahalo, wanafunzi hujikuta wakikabiliana na changamoto za kujieleza mbele ya wengine. Hatua inayosaidia wanafunzi katika kuimarisha ujasiri wao. Wanapojikuta katika

mazingira ya midahalo, wanafunzi wanapata uzoefu wa kuzungumza mbele ya hadhira na kufanya hivyo mara kwa mara huwasaidia kuondoa hofu na wasiwasi wa kujieleza. Hii hujenga ujasiri na kuwapa uwezo wa kuzungumza bila woga katika mazingira mbalimbali.

Isitoshe, ufundishaji wa stadi za kuzungumza kwa kutumia midahalo unawapa wanafunzi fursa ya kukuza uwezo wa kuwashawishi wengine kupitia mazungumzo. Bellon (khj) anasema kwamba, wanapojadiliana na kujaribu kushawishi wenzao kuhusu mtazamo wao kuhusu mada fulani, wanajifunza mbinu za kushawishi, tutoa hoja zenye nguvu na kueleza mawazo yao kwa njia inayowavutia wengine. Hii huwapa uwezo wa kujenga hoja zao na kusikiliza hoja za wengine, jambo ambalo ni muhimu sana katika mawasiliano ya kuvutia na kujenga hoja zenye msingi.

Kulingana na maelezo ya hapo juu, midahalo hutoa jukwaa muhimu kwa wanafunzi kujenga stadi ya kuzungumza, kuimarisha ufahamu wao wa lugha na kuondoa hofu ya kujieleza mbele ya hadhira. Maelezo haya yanaonesha kwamba midahalo ina nafasi kubwa katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza kwa kuwa inawasidia wanafunzi kujenga hoja kwa mantiki fasaha na kuwashawishi wengine katika mazungumzo. Kwa kuwa tafiti za hapo juu zimejikita katika lugha ya Kiingereza, utafiti wetu, ulikusudia kudhihirisha namna ambavyo midahalo inaweza kutumiwa katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa kutumia TEHAMA katika shule za sekondari za Wilaya ya Nyamasheke.

### 2.6 Nafasi ya TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza

Lengo mahususi la kwanza la utafiti lilikuwa kuchunguza na kuthibitisha jukumu la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke, nchini Rwanda.

Kwa hivyo, ili kufikia lengo hili, tuliamua kufanya uchunguzi wa maandiko yanayohusiana na nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza. Hivyo, sehemu hii imegawanyika katika vipande viwili: TEHAMA na ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza lugha na TEHAMA na ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili.

### 2.6.1 TEHAMA na Stadi za Kuzungumza

Kwenye muktadha wa elimu ulimwenguni, leo TEHAMA imekuwa hitaji la msingi na sehemu muhimu sana ya elimu (Benmeddah, 2017). TEHAMA katika mfumo wa stadi za kidijiti imekuwa mojawapo ya stadi ambazo wanafunzi lazima wapate, mbali na stadi za kuandika, kusoma na kuhesabu katika Karne ya 21 (Benmeddah, khj). Wazo hili linathibitisha kwamba TEHAMA ni stadi muhimu ambayo imejumuisha katika elimu ili kufanikisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo basi, sehemu hii inasheheni mapitio ya maandiko kuhusu nafasi ya TEHAMA kwenye mchakato wa ufundishaji wa stadi ya kuzungumza lugha kwa ujumla.

#### 2.6.1.1 TEHAMA Hurahisisha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kuzungumza

TEHAMA katika elimu inapaswa kuungwa mkono sana kwani wanafunzi wa sasa ndio vijana wa baadaye ambao watashiriki katika kuunda sio tu maisha yao binafsi, bali pia jamii zao, taifa na ulimwengu kwa ujumla.

Kulingana Omidvar & Bahadorfar (2014), ni jukumu la kila mdau wa sekta ya elimu kuunga mkono mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazotegemea matumizi ya TEHAMA ambazo zingeweza kuwa na ufanisi zaidi na kukidhi mahitaji ya ulimwengu wa kisasa. Kwa mujibu wa Omidvar & Bahadorfar (whj), TEHAMA inajitokeza kama chombo kinachofaa kwa kukuza ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza lugha.

Kama inavyoelezwa na Abdelbaki (2021), majukwaa ya TEHAMA yameleta mapinduzi katika mchakato wa kujifunza na kufundisha stadi ya kuzungumza kwa wanafunzi. Abdelbaki (khj), anaongeza kwamba, kwa kupitia rasilimali za mtandaoni na zana za kujifunzia zinazopatikana kwa urahisi kwa kutumia TEHAMA, wanafunzi wanapata fursa ya kushiriki katika mazoezi ya kuzungumza katika mazingira mbalimbali. Programu za mafunzo zinazopatikana mtandaoni zinawawezesha wanafunzi kupakua vifaa vya kujifunzia vinavyohusiana na stadi ya kuzungumza.

Hivyo ni kama vile vifungu vya mazungumzo, midahalo na mazoezi ya kuzungumza lugha lengwa kwa usahihi (Abdelbaki, khj). Hii inawawezesha wanafunzi kujiboresha na kuendeleza uwezo wao wa kujieleza kwa ufasaha na kwa uhakika.

Zaidi ya hayo, TEHAMA inawaruhusu wanafunzi kufanya mazoezi yao ya kuzungumza kwa kurejikodi na kujitathmini. Kulingana na Abdelbaki (khj), kupitia zana za TEHAMA kama

programu za kurekodi sauti au video, wanafunzi wanaweza kurekodi hotuba zao au majadiliano na kisha kujitathmini. Hii inatoa fursa ya kujiongezea ujasiri, kuona maendeleo yao na kutambua maeneo ya kuboresha katika stadi ya kuzungumza. Kwa kufanya marekebisho yanayohitajika kulingana na tathmini zao binafsi, wanafunzi wanaweza kuimarisha stadi yao ya kuzungumza na kujenga ujasiri katika kutumia lugha kwa ufasaha.

Maandiko ya hapo juu yameeleza umuhimu na faida za kutumia TEHAMA katika kukuza stadi ya kuzungumza katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiingereza. Yamefafanua jinsi TEHAMA inavyoweza kuleta mapinduzi katika elimu kwa kutoa fursa za mazoezi na tathmini za stadi ya kuzungumza kwa wanafunzi. Pia, yameonesha jinsi TEHAMA inavyowawezesha wanafunzi kujiboresha kwa kurekodi na kujitathmini, hivyo kuongeza ufasaha na ujasiri wao katika matumizi ya lugha. Kwa kuongezea, maandiko hayo yameonesha umuhimu wa TEHAMA kama chombo muhimu cha kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wenye ufanisi. Kutokana na maelezo haya, tuliamua kufanya utafiti wetu ili tuchunguze namna ambavyo utumiaji wa TEHAMA unavyoweza kurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa kuzungumza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

#### 2.6.1.2 TEHAMA Huwasaidia Walimu Kupata Zana za Kisasa za Kufundishia Stadi za Kuzungumza

Ufundishaji wa stadi ya kuzungumza unahitaji zana za kisasa ambazo si rahisi kwa kila shule kuzipata (Yasim, Lubis, Noor & Kamarudin, 2016). Kwa hiyo, TEHAMA inakuja kama suluhisho la kuwezesha walimu na wanafunzi wa lugha, walimu kupata zana za kisasa za kufundishia stadi za kuzungumza. Kulingana na Reid (2002), TEHAMA inasaidia walimu kupata zana za kisasa zinazoboresha mchakato wa kufundisha stadi za kuzungumza.

Kupitia zana hizi, walimu wanaweza kutoa mafunzo ya ubunifu na yenye ufanisi ambayo husaidia wanafunzi katika maendeleo yao ya stadi ya kuzungumza. Kwa mfano, taarifa na programu zinazopatika mtandaoni zinazotumika katika darasa hutoa zana za kipekee kama vile mifano halisi ya mazungumzo, mazoezi ya kusikiliza na zana za kujifunzia lugha (Reid, khj).

Zana hizi huwa na mchango mkubwa katika kuwafanya wanafunzi kuhisi kuwa na uzoefu wa moja kwa moja katika lugha wanayojifunza na hii huchochea uelewa wao na kujiamini wanapokuwa wanazungumza lugha lengwa.

Aidha, Reid (khj) anasema kwamba, TEHAMA hutoa fursa kwa walimu kuunda na kupata zana za kufundishia kwa njia ya ubunifu zaidi. Kupitia matumizi ya zana za dijiti kama video, maonesho ya dijiti na maudhui mengine ya mtandaoni, walimu wanaweza kuunda nyenzo zinazovutia na zinazohusika kwa wanafunzi.

Kwa mfano, kupitia matumizi ya TEHAMA, walimu wanaweza kubuni video za mafunzo, vikao vya mazungumzo au maingiliano fasaha ya moja kwa moja yanayowawezesha wanafunzi kushiriki kikamilifu na kujifunza stadi za kuzungumza katika mazingira yanayovutia (Reid, khj). Wazo hili linathibitisha kwamba matumizi ya TEHAMA husaidia walimu kuunda zana za ufundishaji ambazo ni faafu katika ukuzaji wa stadi ya kuzungumza kwa wanafunzi.

Kwa kuongezea, TEHAMA inaruhusu walimu kupata zana ambazo zinawasaidia kufuatilia maendeleo ya wanafunzi katika stadi ya kuzungumza kwa njia iliyorahisishwa (Benmeddah, khj). Kupitia programu na zana za mtandaoni, walimu wanaweza kufuatilia mazoezi na mawasilisho ya wanafunzi, kutathmini matokeo yao na kutoa mrejesho wa moja kwa moja. Hii inawawezesha walimu kubaini maeneo ya udhaifu na uwezo za wanafunzi na kutoa msaada unaofaa ili kuimarisha stadi ya kuzungumza lugha lengwa.

Maelezo ya hapo juu yanaweza kuleta tija kubwa katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa njia ya TEHAMA. Kwanza, yanathibitisha umuhimu wa TEHAMA kama suluhisho la kuwezesha walimu na wanafunzi kupata zana za kisasa za kufundishia stadi za kuzungumza, ambazo zinaweza kuwa ngumu kupatikana kwa kila shule kwa njia za kawaida.

Pia, yanaonesha jinsi TEHAMA inavyowezesha walimu kutoa mafunzo ya ubunifu na yenye ufanisi kupitia zana za dijiti zinazoboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza. Hatimaye, yanaonesha jinsi TEHAMA inavyowasaidia walimu kufuatilia na kutoa mrejesho wa moja kwa moja kwa wanafunzi, kuongeza ufanisi wa mchakato wa kujifunza stadi ya kuzungumza.

Mambo haya yalituchochea kutaka kuelewa jinsi TEHAMA inavyoweza kutumika kwa ufanisi katika mazingira ya kufundishia Kiswahili kuzingatia stadi ya kuzungumza. Hivyo basi, utafiti

wetu ulikusudia kubainisha namna ambavyo walimu wa Kiswahili wanaweza kupata kwa urahisi vifaa vya kufundishia na kujifunzia stadi ya kuzungumza Kiswahili katika shule za sekondari za Wilaya ya Nyamasheke.

#### 2.6.1.3 TEHAMA Huongeza Hamasa ya Kuzungumza Lugha Lengwa Miongoni mwa Wanafunzi

Mara nyingi, ufundishaji wa lugha unakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa hamasa ya kujifunza lugha hiyo miongoni mwa wanafunzi (Kovac & Mrsic, 2017). Kulingana na Mullamaa (2010), TEHAMA ina jukumu muhimu katika kuongeza hamasa ya wanafunzi katika kujifunza na kuzungumza lugha lengwa. Kwa kutumia njia za kisasa za mawasiliano kama vile mikutano ya mtandaoni, programu za simu, video na filamu, TEHAMA inawafanya wanafunzi kujihisi katika mazingira ya kujifunza yenye kuvutia na ya kujishirikisha katika ufundishaji na ujifunzaji (Passey & Goodison, 2004). Hii husaidia kuondoa vizuizi vya kimazingira na kuwapa wanafunzi fursa ya kujenga ujasiri na hamasa katika kuzungumza lugha lengwa.

Zaidi ya hayo, Mohanta, Mahato & Sutradhar (2023) waanasema kwamba TEHAMA inawasaidia wanafunzi kupata mbinu mbalimbali za kujifunza lugha kwa njia ya kuvutia. Kupitia matumizi ya TEHAMA, wanafunzi huweza kupata na kufikia Programu za mafunzo ya kielimu, nyimbo, filamu za kielimu, vikao vya majadiliano zana nyingine za kuelimisha ambazo husaidia katika kuchochea hamasa ya wanafunzi katika kujifunza na kuzungumza lugha lengwa. Kwa hiyo, matumizi ya TEHAMA ni mbinu mwafaka ya kuongeza ushiriki wa wanafunzi na kuwafanya waweze kujishirikisha na kufurahia mchakato wa kujifunza ili waweze kuzungumza lugha lengwa kwa ufasaha.

Isitoshe, kupitia TEHAMA, wanafunzi wanapata fursa ya kuwasiliana na kushirikiana na wenzao kutoka sehemu mbalimbali za dunia (Mohanta na wenzake, whj). Hii inawawezesha kufanya majadiliano, kubadilishana uzoefu na kufanya mazoezi ya lugha kwa muktadha halisi. Kwa njia hii, TEHAMA hukuza msisimko na hamasa katika ujifunzaji lugha. Hii ina maana kwamba, matumizi ya TEHAMA yanawaruhusu wanafunzi kuunda uhusiano na jamii za kimataifa na kuvutiwa zaidi pamoja na kupata fursa ya kuzungumza na kuwasiliana na watu wenye asili na tamaduni tofauti. Kwa hiyo, matumizi ya TEHAMA huongeza hamasa ya wanafunzi ya kujifunza na kuzungumza lugha lengwa.

Baada ya kupitia maandiko tofauti, tulioona kwamba watafiti tofauti wamebainisha kwamba TEHAMA hukuza hamasa ya kujifunza na kuzungumza. Vilevile, wakati wa mapitio ya maandiko, tuliona kuwa kuna uhaba wa tafiti zinazozungumzia matumizi ya TEHAMA katika ukuzaji wa hamasa ya kujifunza na kuzungumza Kiswahili hasa kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda. Hali hii ilitupa shauku ya kufanya utafiti ili kuthathmini nafasi ya TEHAMA katika ukuzaji wa hamasa ya kujifunza na kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari katika wilaya Nyamasheke nchini Rwanda. Tulifikiri kwamba utafiti utakuwa ushahidi wa kwamba TEHAMA ina au haina mchango katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kupitia ukuzaji wa hamasa ya kujifunza na kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda.

#### 2.6.1.4 TEHAMA Hurahisisha Ushirikiano kati ya Wanafunzi wa Lugha ya Pili na Wazawa wa Lugha Hiyo

Kushirikiana na wazawa wa lugha kunaimarisha siyo tu mchakato wa wanafunzi kujifunza kwa kutoa muktadha wa maisha halisi, bali pia kuinamarisha uwezo wao wa lugha zaidi ya shughuli za kawaida darasani (Pizarro, 2022).

Matumizi ya TEHAMA yana nafasi muhimu katika kufundisha stadi ya kuzungumza katika lugha tofauti kwa sababu ya uwezo wake wa kurahisisha ushirikiano kati ya wanafunzi wanaojifunza lugha hiyo na wazawa wa lugha husika. Kwa mfano, njia kama vile mawasiliano ya video, majukwaa ya mtandaoni, mitandao ya kijamii na programu za mawasiliano ya moja kwa moja zimekuwa zikitumiwa kwa kiasi kikubwa katika kuwasiliana na wazawa wa lugha (Siddig, 2020). Hii inawawezesha wanafunzi kujifunza lugha kwa kusikiliza na kushiriki katika mazungumzo halisi na watu ambao ni wazungumzaji wenye ufasaha wa lugha hiyo.

Pamoja na hilo, TEHAMA inachangia katika kuunda jukwaa la kimataifa ambapo wanafunzi wanaweza kushirikiana na wazawa wa lugha kutoka pande mbalimbali za dunia. Kwa kuzingatia matumizi ya TEHAMA, umbali wa kimwili si kizuizi tena, kwa kuwa TEHAMA imeifanya dunia kuwa kama kijiji kidogo (Chun, Kern & Smith, 2016). Kwa hiyo, kupitia matumizi ya TEHAMA, wanafunzi wanaweza kuingiliana na kufanya mazungumzo na wazungumzaji wa lugha kwa urahisi, bila kujali wako wapi duniani. Hii huwapa wanafunzi fursa ya kufahamu mitindo tofauti ya kuzungumza na kutumia lugha na hivyo kuboresha stadi zao za kuzungumza kwa njia fasaha.

Zaidi ya hayo, TEHAMA inaruhusu wanafunzi kufuatilia na kujifunza kutoka kwa wazawa wa lugha wanapozungumza. Kulingana na Sulistyaningrum (2019), kupitia video, wanafunzi wanaweza kurekodi na kuchambua mazungumzo ya wazungumzaji wa lugha na kisha kujaribu kufuata na kujifunza jinsi maneno hutamkwa, sentensi hufumuliwa na hata lugha ya mwili inavyotumika. Hii inawawezesha wanafunzi kujenga ufasaha wao wa lugha kwa kuiga na kujifunza kutoka kwa wazungumzaji wa lugha ya asili. Kwa hiyo, kupitia matumizi ya TEHAMA, wanafunzi wanaweza kujenga ufasaha wao na kuboresha stadi zao za mawasiliano katika lugha lengwa kwa njia ya asili na inayowafanya waweze kushirikiana na jamii ya wazungumzaji wa lugha husika.

Maelezo ya hapo juu yanaonesha kwamba matumizi ya TEHAMA katika kujifunza lugha husaidia wanafunzi kuwasiliana na wazawa wa lugha kwa muktadha halisi na kuboresha stadi zao za kuzungumza. Maelezo husika yalitusababisha kufanya utafiti ili kuchunguza nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa njia ya kuwawezesha wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamasheke kuwasiliana na wazawa wa Kiswahili kwa urahisi.

### 2.6.2 TEHAMA na Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kuzungumza Kiswahili

Ulimwengu wa utandawazi umeleta ongezeko la matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), hasa katika matumizi ya kompyuta na zana zake. Kwa sababu hii, maendeleo hayo yamesababisha kuenea kwa lugha zinazotumika katika teknolojia hiyo, kama vile Kiingereza na lugha nyingine za Kimagharibi. Kwa kiwango kidogo, pia kumekuwa na athari kwenye lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili (Msigwa, 2019).

Kwa hiyo, maandiko yaliyopitiwa yamebainisha kwamba upo umuhimu wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha yay a pili au kigeni kama ulivyoelezwa hapo chini.

Matumizi ya TEHAMA katika kufundisha stadi za Kiswahili Kiswahili kama lugha ya pili hufanya ufundishaji uwe rahisi zaidi kwa namna mbalimbali (Vicent & Msigwa, 2021). Matumizi ya projekta hutoa fursa ya kuandaa mafunzo kwa njia rahisi kwenye kompyuta na kuyawasilisha kwa wanafunzi kwa urahisi.

Hii husaidia walimu kufunza mambo mengi kwa haraka na kumaliza masomo kwa wakati. Hii inamaanisha kwamba, TEHAMA inawawezesha walimu kukamilisha ufundishaji mapema, hivyo kuwapa muda wa kutosha wa kuwapa wanafunzi mazoezi na marejeo ambayo husaidia katika kufanya ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili uwe wenye manufaa zaidi kwa wanafunzi.

Aidha, kulingana na Vicent na Msigwa (whj), matumizi ya TEHAMA pia hutoa fursa ya kufundisha stadi za Kiswahili kwa watu wa kigeni, hata katika mazingira ambayo mwalimu na wanafunzi hawapo pamoja ana kwa ana. Kwa mfano, mwalimu anaweza kusimamia darasa la wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali duniani bila ya kuwa na mwingiliano wa moja kwa moja. Hii inawezekana kwa kutumia mawasiliano ya mtandaoni kupitia mitandao ya kijamii. Mwalimu anaweza kuanzisha kundi la mazungumzo na wanafunzi wake, wakajadili mada za lugha ya Kiswahili (Vicent & Msigwa, whj). Ni kumaanisha kwamba, kupitia matumizi ya TEHAMA, mwalimu anaweza kuandaa somo, kulirekodi na kulipakia kwenye majukwaa ya ujifunzaji yaliyopo mtandaoni na kuwahimiza wanafunzi kulisoma kupitia mtandao huo. Hivyo, TEHAMA inarahisisha ufundishaji wa stadi za Kiswahili kwa wageni hata kwa umbali.

Zaidi ya hayo, TEHAMA inaweza kusaidia mwanafunzi katika kuelewa dhana zilizokusudiwa na mwalimu, hususani zile zinazohusiana na masuala ya kitamaduni ambayo yanaweza kuwa vigumu kueleweka kwa urahisi bila kutumia njia shirikishi za kisasa (Bilyalova, 2017). Kwa mfano, katika kufundisha masuala ya kitamaduni kama jando na unyago, mwalimu anaweza kutumia vifaa vya TEHAMA kurekodi sherehe hizo na matukio muhimu.

Baadaye, wanafunzi wanapopewa fursa ya kuangalia matukio hayo kwenye video na kusikiliza maelezo yanayohusiana na matukio hayo, huwasaidia kuelewa mada hizo kwa undani zaidi (Msigwa, khj). Hii inathibitisha kwamba matumizi ya TEHAMA yanasaidia mwanafunzi kuelewa mazingira ya kitamaduni na kuongeza ujuzi wake katika lugha.

Isitoshe, kulingana na Msigwa (khj), matumizi ya TEHAMA huchochea hamasa ya wanafunzi katika kusoma na kujifunza stadi za lugha ya Kiswahili. Zana za TEHAMA vinavyoshirikisha wanafunzi bila kuhusisha mwalimu moja kwa moja huwafanya wanafunzi washiriki kwa ufanisi katika mchakato wa ufundishaji wa Kiswahili. Kulingana na Vicent & Msigwa (whj), zana kama

hizi huwahamasisha wanafunzi kushiriki kikamilifu na kujifunza kwa vitendo, wakijitahidi kutumia akili na miili yao.

Wanafunzi wanaotumia muda kwenye kompyuta wanapaswa kuwa makini wanapopata vifaa vya lugha na wanapowasiliana na walimu kupitia mitandao ya kijamii, wakihitaji umakini na jitihada katika kujifunza (Msigwa, khj). Zaidi ya hayo, michezo ya kompyuta iliyoundwa kwa kujifunzia lugha huchochea hamasa ya wanafunzi wa Kiswahili kwa kuwahusisha katika majibu ya haraka, wakiwafanya kuwa na ari na motisha ya kufikia malengo yao ya kujifunza stadi za lugha ya Kiswahili.

Kwa muhtasari, matumizi ya TEHAMA katika kufundisha Kiswahili kama lugha ya pili huwawezesha walimu kufikia wanafunzi kwa ufanisi popote walipo, kutoa mafunzo kwa njia rahisi na kuelezea dhana za kitamaduni kupitia vifaa vya kiteknolojia. Vilevile, zana hizi huchangia kuchochea hamasa ya wanafunzi katika kujifunza kwa kushirikisha mbinu zilizo shirikishi na za kuvutia kama video, mawasiliano mtandaoni na michezo ya kompyuta.

Tafiti za Msigwa (khj) na Vicent & Msigwa (whj) kuhusu TEHAMA na ufundishaji wa Kiswahili, zinabainisha waziwazi nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili kwa ujumla. Pia, zinaonesha jinsi TEHAMA inavyoweza kutumiwa katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Kwa hivyo, utafiti wetu ulikusudia ulikusudia kutoa ufafanuzi juu ya nafasi ya TEHAMA katika kufundisha stadi ya kuzungumza Kiswahili na njia ambazo walimu wanaweza kutumia TEHAMA kufundisha stadi hiyo kwa wanafunzi wa shule za sekondari katika Wilaya ya Nyamasheke, nchini Rwanda. Muktadha huu wa utafiti unathibitisha umuhimu na haja ya utafiti tuliofanya.

## 2.7 Mbinu za Utumiaji wa TEHAMA katika Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza

Utafiti ulikuwa na lengo mahususi la pili la kuunda miongozo ya matumizi ya TEHAMA katika kuboresha mchakato wa kufundisha na kujifunza stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule katika wilaya ya Nyamasheke, Nchini Rwanda. Hivyo, sehemu hii inajikita katika kukusanya na kuchambua maandiko yanayohusu mbinu za matumizi ya TEHAMA katika kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza.

### 2.7.1 Utumiaji wa Michezo ya KiTEHAMA

Ingawa kujifunza lugha mpya kunaweza kuwa jambo linalotisha, michezo ya elimu kwa video inaweza kufanya ufundishaji wa lugha kuwa wenye furaha na ufanisi zaidi (Newcombe & Brick, 2017). Kwa kutoa uzoefu wa kujifunza ambao ni shirikishi, michezo ya kupata lugha inaweza kusaidia wajifunzaji kukuza uwezo wao wa lugha katika kama msamiati, sarufi, matamshi na ufahamu wa kitamaduni.

Ufundishaji wa stadi za lugha ya pili kwa watoto katika mazingira ya kawaida mara huwa na matokeo yasiyofurahisha. Lakini, matumizi ya michezo ya TEHAMA, hushiriki vikubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za lugha hasa kwa watu wenye umri mdogo. Kulingana na Froehling (2023), mojawapo ya faida kubwa za kutumia michezo ya kiTEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha mpya ni kuwashirikisha wanafunzi na kuwamotisha ili waweze kufurahia ujifunzaji wa lugha hiyo. Michezo kama hii inaweza kuhusisha mazingira halisi ya ujifunzaji wa lugha na mwingiliano unaoweza kusaidia wanafunzi kujifunza lugha mpya kwa njia inayofurahisha na yenye ufanisi.

Kwa kuwaweka wanafunzi katika ulimwengu wa kidijiti ambapo wanazungukwa na lugha wanayojifunza, michezo ya kiTEHAMA inawaruhusu wanafunzi kujifunza kupitia muktadha na mazoezi badala ya kukariri na kurudia kile wanachosikia.

Kama anavyoeleza na Froehling (khj), lengo kuu la michezo ya kiTEHAMA ni kusaidia wanafunzi kuimarisha stadi za lugha ya pili kwa kuimarisha uwezo wao wa kuzungumza, kusoma na kusikiliza kwa njia inayosisimua. Mchezo hii ina mazungumzo yaliyosimuliwa na uigizaji unaosisimua ambao umeandaliwa kikamilifu kwa ajili ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha.

Hii inaruhusu wajifunzaji wa lugha ya pili kumudu zaidi stadi za lugha pamoja na matumizi ya ishara kimya za kimwili na ishara za kihisia, ambazo zinaweza kusaidia kuimarisha uwezo wao wa mawasiliano (Froehling, khj). Hii ina maana kwamba, michezo ya kiTEHAMA ina mchango mkubwa katika ufundishaji wa stadi za lugha ikiwemo stadi ya kuzungumza.

Kwa hiyo, michezo ya kiTEHAMA imeelezwa kama njia muhimu na yenye ufanisi katika mchakato wa kufundisha na kujifunza lugha mpya kwa kuwa inatoa uzoefu wa mazingira halisi na vitendo. Michezo hii usaidia wanafunzi kufanikiwa kwa kujenga fursa za kibinafsi za

kujifunza lugha hiyo. Utafiti wa Froehling (khj) umeonesha mchango wa michezo ya kiTEHAMA katika ufundishaji wa stadi za lugha ya Kiingereza. Utafiti huu ulitupa shauku ya kufanya utafiti ili kubainisha namna ya utekelezaji wa mbinu ya utumiaji wa michezo ya kiTEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari za Wilaya ya Nyamasheke nchini Rwanda.

### 2.7.2 Utumiaji wa Mikutano ya Video Mtandaoni

Istilahi "mikutano ya mtandaoni" hutumika kuelezea mfumo wa mawasiliano ambapo washiriki wawili au zaidi katika maeneo tofauti wanaweza kuingiliana huku wakitazamana na kusikilizana kwa wakati halisi kwa kutumia vifaa maalum na muunganisho wa intaneti wenye kasi kubwa (Smith, 2003).

Kwa kuwa mikutano ya mtandaoni inawezesha kuvuka umbali wa kijiografia, inaweza kutumiwa na walimu wa lugha za kigeni ambao wanataka kuepukana na changamoto ya ukosefu wa stadi ya kuzungumza darasani kwa kuwawezesha wanafunzi kushiriki katika mwingiliano wa kweli ambapo uzoefu wa mawasiliano unaweza kupanuliwa (Loranc-Paszylk, 2015).

Kuna idadi ya wasomi wanaohusisha mwingiliano unaolenga kuimarisha stadi za kuzungumza katika lugha za kigeni kupitia mikutano ya mtandaoni na masuala ya ujasiri wa kibinafsi, na upunguzaji wasiwasi na hofu katika mawasiliano. Kwa mfano, Kim & Craig (2012) wanasema kuwa, kutokana na mazingatio hayo, si jambo la kushangaza kwamba mikutano ya mtandaoni imekuwa ikitoa mchango muhimu katika uga wa kujifunza lugha, haswa kama njia ya mawasiliano kwa sauti na wazungumzaji waliobobea/wazawa wa lugha na kama njia ya kukuza stadi za mawasiliano miongono mwa wanafunzi. Hii inamaanisha kwamba, mikutano ya mtandaoni imekuwa muhimu katika kujifunza lugha kwa kuwa inawezesha mawasiliano na wazungumzaji wenye ujuzi, ikisaidia pia kuimarisha stadi za lugha kwa wanafunzi.

Zaidi ya hayo, Wang (2007) anasema kwamba, mikutano ya mtandaoni inachangia kwa kiasi kikubwa katika mchakato wa uelimishaji wa stadi za lugha, hasa katika stadi za kusikiliza na kuzungumza. Uwezekano wa wanafunzi kushiriki katika mazungumzo na wazungumzaji walio mahiri katika lugha inayofundishwa hufanya mikutano ya mtandaoni kuwa jukwaa muhimu la kujenga ujuzi wa kusikiliza na kuzungumza. Kupitia muktadha huu, wanafunzi hupata fursa ya kusikiliza lugha lengwa katika matumizi halisi, huku wakipata uelewa wa dhana muhimu na matamshi bora (Wang, 2007). Vilevile, kushiriki katika mazungumzo na wazungumzaji wenye

ufasaha husaidia kuwajengea wanafunzi ujasiri wa kuzungumza, kuwawezesha kujaribu kutumia lugha kwa ufasaha na kwa uhuru (Phillips, 2010).

Hii ina maana kwamba mikutano ya mtandaoni inaboresha uwezo wa wanafunzi wa mawasiliano na kuwapa msukumo katika kuendeleza stadi zao za lugha kwa njia inayowawezesha kushiriki kikamilifu katika muktadha wa lugha. Hata kama, tafiti za hapo juu zinaonesha mchango wa mikutano ya mtandaoni katika ujifunzaji wa stadi za lugha, tafiti hizi zimetoa mchango kuhusu nafasi mikutano ya mtandaoni katika ufundishaji wa stadi za lugha ya Kifaransa na Kiingereza kwa wanafunzi wa shule za msingi.

Kwa hiyo, tuliamua kufanya utafiti ili kuchunguza mchango wa mikutano ya mtandaoni katika uelimishaji wa stadi ya kuzungumza katika Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari za wilaya ya Nyamasheke nchini Rwanda. Isitoshe, utafiti wetu ulikusudia kubainisha hatua za utekelezaji wa mbinu ya utumiaji wa mikutano ya mtandaoni katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza katika Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari za Wilaya ya Nyamasheke nchini Rwanda.

### 2.7.3 Utumiaji wa Programu za Mtandaoni za Kufundishia na Kujifunzia Stadi za Kuzungumza

Programu za mtandaoni za kufundishia na kujifunzia lugha zimekuwa nyenzo muhimu katika mchakato wa elimu ya lugha. Wu, Lee, Schmidt, Heil, Wu & Lee (2016) wanasema kwamba, programu za mtandaoni ni mifumo ya kidijiti iliyoundwa kwa ajili ya kusaidia wanafunzi na walimu katika kufikia malengo ya kufundisha na kujifunza lugha kwa njia iliyorahisishwa na ya kuvutia.

Programu hizi zinajumuisha mazoezi mbalimbali kama vile mazungumzo ya moja kwa moja, mazoezi ya kusikiliza, kusoma na masomo ya kuwasiliana kwa njia ya mtandao. Programu hizi hutoa jukwaa lenye mazingira bora kwa wanafunzi ya kujifunza na kuelewa lugha kwa ufanisi zaidi.

Kwa mujibu wa Thienthong & Lian (2014), programu za mtandaoni huchangia kuboresha ufundishaji wa stadi za lugha kwa urahisi na bila gharama kubwa. Hii ni kwa sababu programu za mtandaoni zinapatikana kwa urahisi na zinaweza kutumiwa na wanafunzi kutoka makundi mbalimbali, bila kujali hali zao za kiuchumi au maeneo wanakoishi. Hii inaweza kuwa na

mchango mkubwa katika kuondoa vizuizi vya ufikiaji wa elimu kwa watu wengi, ikiruhusu kila mmoja kujifunza lugha kwa njia inayowafaa bila ghara ghali.

Aidha, kupitia programu za mtandaoni, wanafunzi hupata fursa ya kukuza ustadi wao katika kusikiliza na kuzungumza (Thienthong & Lian, 2014). Kupitia programu za mtandaoni, wanafunzi wanaweza kufanya mazoezi ya kusikiliza maudhui tofauti na kujihusisha katika mazungumzo na wengine kwa njia ya mtandao, ambayo husaidia katika kuimarisha uwezo wao wa kuelewa na kuzungumza lugha wanayojifunza kwa ufanisi.

Zaidi ya kusikiliza na kuzungumza. Bahrani & Sim (2012) wanasema kwamba programu za mtandaoni zinaweza kushiriki katika kufundisha na kujifunza mada ngumu katika lugha hasa zinazohusiana na itikadi na utamaduni ambazo si rahisi kufundishwa kwa njia ya kawaida. Hii inaongeza ufanisi wa kujifunza lugha kwa kutoa mazingira halisi na yenye ufanisi zaidi ya mazoezi.

Kwa ufupi, kulingana na maelezo yaliyotolewa, programu za mtandaoni za kufundishia na kujifunzia lugha zinaleta njia inayorahisisha ufundishaji wa stadi za lugha. wazo hili lilitufanya tuamue kufanya utafiti ili tubainishe baadhi ya programu za mtandaoni za kufundishia na kujifunzia stadi za lugha na hatua za utekelezaji wa matumizi ya programu hizo katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari za Wilaya ya Nyamasheke nchini Rwanda.

### 2.7.4 Utumiaji wa Teknolojia ya Utambuzi wa Sauti

Teknolojia ya utambuzi wa sauti ni aina ya teknolojia ambayo inatumia mifumo maalum ya kompyuta ili kutambua, kuelewa na kusindika sauti zinazopokelewa au zilizorekodiwa (Carrier, 2017). Carrier (khj) anasema kuwa, teknolojia ya utambuzi wa sauti inafanya kazi kwa kuchambua vipengele vya sauti kama vile mifumo ya mazungumzo, maneno au ishara za sauti na kuzielewa ili kuzalisha matokeo yanayotarajiwa au kuchukua hatua maalum kulingana na sauti hizo. Teknolojia hii inatumika katika maeneo mengi kama vile utambuzi wa hotuba, mifumo ya sauti kwenye vifaa vya kielektroniki na hata katika huduma za kidijiti. Teknolojia hii pia hutumika katika mawasiliano ya simu, uchanganuzi wa data na katika maeneo mengine mengi ambapo ufahamu wa sauti na maneno ni muhimu (Carrier, khj).

Kwa hiyo, teknolojia ya utambuzi wa sauti ni aina ya teknolojia ambayo hutumia kompyuta kutambua, kuelewa na kufasili sauti, ikihusisha maeneo kama utambuzi wa hotuba, vifaa vya kielektroniki na mawasiliano ya simu. Kama inavyobainishwa hapo chini, teknolojia ya utambuzi wa sauti ina mchango katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi tofauti za lugha.

Kulingana na Yuan & Briscoe (2016), matumizi ya teknolojia ya utambuzi wa sauti katika kujifunza lugha yanaweza kuboresha ufasaha wa lugha. Kwanza kabisa, teknolojia hii inaweza kusaidia kurekebisha matamshi ya wanafunzi. Moja ya changamoto kubwa za kujifunza kuzungumza lugha ni kupata matamshi sahihi, hasa kama unajifunza zaidi kivyako. Hata watumiaji asili wa lugha, mara nyingine wanaweza kupata ugumu kutambua sehemu gani ya matamshi ya msemaji inahitaji marekebisho.

Lakini, kupitia matumizi ya teknolojia ya utambuzi wa sauti, ni rahisi sana kutambua sehemu ya matamshi ambayo inahitaji kufanyiwa marekebisho (Yuan & Briscoe, whj). Kwa mujibu wa Gifford (2013), kupitia matumizi ya teknolojia ya utambuzi wa sauti, wanafunzi wanaweza kujifunza kuzungumza kwa kutumia simu au vifaa vingine vya kielektroniki na kufahamu mara moja eneo ambalo linahitaji kuboreshwa. Hii ina maana kwamba, teknolojia ya utambuzi ina mchango muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za lugha hahasa stadi ya kuzungumza kupitia uboreshaji wa matamshi wa lugha lengwa.

Zaidi ya hayo, teknolojia ya utambuzi wa sauti inaondoa hofu ya kufanya makosa katika safari ya ujifunzaji wa lugha (Yuan & Briscoe, whj). Kitu kinachowazuia watu wengi kujifunza stadi za kuzungumza lugha ni hofu ya kufanya makosa mbele ya wasemaji wa asili wa lugha lengwa. Matumizi ya teknolojia ya utambuzi wa sauti, hauhitaji kuwa na wasiwasi wa kufanya makosa, kwani mwanafunzi hufanyia mazoezi kivyake bila kuhusisha mtu halisi.

Kwa hiyo, kujifunza kupitia programu za teknolojia ya utambuzi wa sauti kunaweza kuimarisha ujasiri zaidi katika uwezo wa mwanafunzi na hatimaye kupunguza hofu ya kuzungumza na wazawa wa lugha lengwa. Kulingana na Gifford (khj), teknolojia ya utambuzi wa sauti inawezesha ujifunzaji wa lugha kibinafsi. Kwa hiyo, teknolojia ya utambuzi wa sauti inaweza kupunguza hofu ya kufanya makosa katika kujifunza lugha kwa kuwawezesha wanafunzi kufanya mazoezi kivyao bila kuhusisha wasemaji wa asili na hivyo kuimarisha ujasiri wao katika stadi ya kuzungumza lugha.

Hatimaye, Saville (2015) anasema kwamba, teknolojia ya utambuzi wa sauti zinatoa chaguo la ujifunzaji ambao ni nyumbulifu. Kupitia teknolojia ya utambuzi wa sauti, mwanafunzi anaweza kufanya mazoezi ya kuzungumza wakati wowote anavyopenda bila kuhitaji kupanga muda na mwenzake. Hii inamaanisha kuwa, kupitia teknolojia ya utambuzi wa sauti, mwanafunzi wa lugha ya pili anaweza kufanya mazoezi ya kuzungumza akiwa pahali popote pale kama vile sokoni, kitandani, njiani, bafuni na pengine (Saville, khj).

Hii inaonesha kwamba teknolojia ya utambuzi wa sauti inatoa urahisi wa kipekee wa kujifunza lugha wakati wowote na mahali popote, ikiruhusu mwanafunzi kuweka mazoezi ya kuzungumza katika sehemu mbalimbali za maisha yao ya kila siku.

Kwa muhtasari, matumizi ya teknolojia ya utambuzi wa sauti katika kujifunza lugha huongeza ufasaha wa lugha kwa kusaidia kurekebisha matamshi ya wanafunzi, huku pia ikiondoa hofu ya kufanya makosa mbele ya wasemaji wa asili. Teknolojia hii pia hutoa njia nyumbulifu ya kujifunza, kuruhusu mazoezi ya kuzungumza popote na wakati wowote na hivyo kuimarisha ujifunzaji wa stadi za lugha. Hivyo basi, tuliamua kufanya utafiti ili kubainisha namna ambavyo walimu wanaweza kutumia teknolojia ya utambuzi wa sauti ili kufundisha stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari za wilaya ya Nyamasheke, nchini Rwanda.

### 2.8 Mapengo ya Utafiti Tangulizi

Utafiti uliofanywa na Kumar & Tammelin (2014) unathibitisha kwamba stadi ya kuzungumza inaweza kufundishwa kwa ufanisi kwa kutumia TEHAMA. Ibrahim (2016), Billon, Marco & Lera-Lopez (2017) na Chapelle, & Sauro (2017) wanaonyesha kuwa matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa lugha za kigeni yamejikita zaidi katika lugha ya Kiingereza na lugha chache za Ulaya kwa wanafunzi wanaojifunza lugha hizo kama lugha za pili au za kigeni. Kevogo (2017) pia anaonyesha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili kwa ujumla.

Aidha, tafiti za Msigwa (2019) na Vincent & Msigwa (2021) zinaonesha jinsi lugha ya Kiswahili imeingizwa katika mfumo wa TEHAMA na kuchunguza changamoto zinazojitokeza katika muktadha huo. Hivyo, matokeo haya yanatoa mwanga wa umuhimu wa TEHAMA katika mchakato wa kufundisha na kujifunza stadi ya kuzungumza, na pia wanatoa mwongozo wa jinsi ya kushughulikia changamoto zinazoweza kutokea.

Utafiti uliofanywa na Kumar & Tammelin (2014) unaonesha kwamba, stadi ya kuzungumza inaweza kufundishwa vema kwa kutumia TEHAMA. Ibrahim (2016), Billon, Marco & Lera-Lopez (2017) & Chapelle, & Sauro (2017) wanaonesha kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni kwa kutumia TEHAMA umefanyika zaidi katika ufundishaji lugha ya Kiingereza na lugha chache za Ulaya kwa wanafunzi wanaojifunza lugha hizo kama za pili au za kigeni. Aidha, utafiti uliofanywa na Kevogo (2017) unaonesha jinsi TEHAMA inavyochangia katika mchakato wa ufundishaji wa Kiswahili kwa ujumla. Zaidi ya hayo, tafiti za Msigwa (2019) na Vincent & Msigwa (2021) zinaonesha jinsi lugha ya Kiswahili ilivyoingizwa katika mfumo wa TEHAMA na kujadili changamoto zinazojitokeza katika muktadha huo.

Ingawa tafiti za hapo awali zimetoa maelezo bora na muhimu katika uwanja wa utafiti, bado kuna mapengo kadhaa ambayo yanahitaji kujazwa ili kufanikisha matumizi sahihi na yenye tija ya TEHAMA katika ufundishaji stadi ya kuzungumza Kiswahili. Mojawapo ya changamoto hizo ni hizi zifuatazo. Mosi, baadhi ya tafiti za hapo awali, zinajikita katika lugha ya Kiingereza ambayo si sawa na lugha ya Kiswahili. Pili, idadi kubwa ya tafiti za hapo awali, zinajikita katika mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa Kiingereza na Kiswahili kwa ujumla bila kusisitizia stadi ya kuzungumza ambayo ni kitovu cha umilisi wa lugha.

Mwisho, watafiti waliofanya utafiti kuhusu TEHAMA na ufundishaji wa Kiswahili wanaonesha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili bila kuhusisha stadi mahususi miongoni mwa stadi nne za Kiswahili. Hivyo basi, tulipata shauku ya kufanya utafiti kwa kusudi la kuyajaza mapengo hayo yote ambayo yalidhihirika.

### 2.9 Nadharia ya Utafiti

Nadharia ya Kuunganishwa, kama ilivyoelezwa na Smith na Jones (2015), inasisitiza mahusiano kati ya michakato ya akili kama vile mawazo, hisia, na tabia. Katika utafiti huu, nadharia hii imetumika kwa kutumia mihimili yake mitatu ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke, Rwanda. Mhimili wa kwanza wa kuunganishwa unaonyesha jinsi mawazo, hisia, na tabia zinavyohusiana na kuathiriana. Tulipanga kutumia mhimili huu kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Mabadiliko katika ufundishaji kupitia TEHAMA, kama vile matumizi ya vifaa vya kidijitali na maudhui ya mtandaoni, yalionekana

kuleta mabadiliko chanya katika namna wanafunzi walivyojifunza na kuboresha uwezo wao wa kuzungumza Kiswahili. Hii ilikidhi lengo la kwanza la utafiti kwa kuonyesha jinsi TEHAMA inaweza kuimarisha stadi ya kuzungumza kupitia muingiliano wa mawazo, hisia, na tabia.

Mhimili wa pili unasisitiza kuwa akili inapaswa kueleweka kama mfumo mzima. Katika utafiti huu, tuliutumia mhimili huu kwa kuzingatia kuwa ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza hauhusishi sehemu moja tu ya akili, bali ni mchakato unaohusisha mambo yote ya akili, ikiwa ni pamoja na fikra, hisia, na mtazamo wa kijamii. Hivyo, tulitumia TEHAMA kwa njia ambazo zinajumuisha vipengele vyote vya akili, kama vile kutumia video zinazowahusisha wanafunzi kihisia na kijamii, pamoja na programu za kompyuta zinazowafanya wanafunzi kushirikiana na wenzao. Matumizi haya ya TEHAMA yalilenga kuimarisha ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza kwa njia jumuishi, kufanikisha lengo mahususi la kwanza la kuboresha stadi ya kuzungumza Kiswahili.

Mhimili wa tatu wa nadharia ya kuunganishwa unasisitiza umuhimu wa muktadha wa kijamii na kihisia katika michakato ya akili. Katika kufanikisha lengo mahususi la kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda, tulitumia mhimili huu kwa kuhakikisha kuwa miongozo hiyo inazingatia muktadha wa kijamii na kihisia wa wanafunzi.

Katika utafiti tuliofanya, tulizingatia mazingira wanamoishi wanafunzi, hisia zao kuhusu teknolojia, na athari za kijamii ambazo zinaweza kuathiri utumiaji wa TEHAMA. Kwa njia hii, miongozo iliyoundwa iliboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa kuwa na uelewa wa kina wa hali halisi ya wanafunzi na jamii zao. Hivyo, mhimili huu ulitumika kuunda miongozo ya TEHAMA inayofaa na yenye ufanisi kwa mazingira ya kijamii na kihisia ya wanafunzi, kufanikisha lengo la tatu la utafiti.

### 2.10 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura ya pili imejikita katika mapitio mbalimbali yaliyopitiwa na kutumika katika utafiti. Mapitio hayo yamegawanyika katika sehemu tofauti zinazojumuisha utangulizi, ufundishaji wa stadi za lugha, ufundishaji wa stadi ya kuzungumza, nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza, mbinu za utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji wa stadi ya kuzungumza, mapengo ya utafiti, nadharia ya utafiti, na muhtasari wa sura ya pili. Hivyo basi, sura inayofuata ni methodolojia ya utafiti.

# SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Kulingana na Graziano & Raulin (2006), methodolojia ya utafiti ni mbinu na miundo ambayo inatumiwa kwa kukusanya, kuchambua, kufasili na kuwasilisha data katika mchakato wa kufanya utafiti. Sura hii inatoa mwanga katika methodolojia iliyotumiwa katika utafiti. Kwa hiyo, sura hii ya tatu ina sehemu tofauti. Sehemu hizo ni: utangulizi, paradima ya utafiti, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango na sampuli ya utafiti, mbinu za kukusanyia data, aina ya data zilikazokusanywa, vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data, itikeli ya utafiti, uhalali na uthabiti wa utafiti na muhtasari wa sura ya tatu.

## 3.2 Paradima ya Utafiti

Kuhn (1962) alitumia kwa mara ya kwanza neno "paradima" kumaanisha njia ya kufikiri kifalsafa (Mertens, 2012). Aidha, katika utafiti wa kielimu, neno "paradima" hutumika kuelezea mtazamo wa mtafiti kuhusu ulimwengu (Anand na wenzake, whj). Mtazamo huu ni ule uchunguzi, njia ya kufikiri, mwelekeo wa kufikiri, seti ya imani zinazoshirikishwa katika kutoa maana au tafsiri ya data za utafiti. Ili kuchagua mbinu za kukusanya na kufasili data, watafiti wanapaswa kwanza kutathmini vipengele vya kimethodolojia vinavyohusiana na suala lao paradima ya utafiti (Anand na wenzake whj). Kwa hiyo, kwenye utafitiwetu, paradima ya utafiti ya ufasiri ilitumiwa.

Kwa mujibu wa Pervin & Mokhtar (2022), paradima ya utafiti ya ufasiri inasisitizia kwamba watu tofauti katika jamii huelewa na hufasiri ukweli wa mambo kwa namna tofauti. Hata kama kuna jambo la kweli, kila mtu hulifasiri na hulieleza kivyake. Aidha, watetezi wa paradima hii hutumia mbinu za kitaamuli katika ukusanyaji data (Kivunja & Kuyini, 2017). Njia wanazozitumia ni pamoja na mahojiano, vikundi vya kujadili, ushuhudiaji na kuchunguza nyaraka kama vile makala za magazeti, ripoti au taarifa kutoka katika tovuti (Pervin & Mokhtar, whj). Kwa kuzingatia paradima hii, mambo yafuatayo yalifanyika ili kuumba na kuupa mwelekeo utafiti. Mosi, mtafiti alikusanya data za kitaamuli kutoka kwa watu tofauti wenye mitazamo tofauti kuhusu TEHAMA na ufundishaji wa stadi ya kuzungumza lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

Kwa kukusanya taarifa hizi, mtafiti alitumia mbinu ya usaili. Kwa kuwa kila mtu anakuwa na namna yake ya kutazama na kueleza mambo, taarifa tofauti zilizotolewa na washiriki wa utafiti zililinganishwa ili kupata mtazamo wa kiujumla kuhusu swala la utafiti.

Pili, kutokana na imani ya kwamba hakuna ukweli mmoja katika jamii, baada ya kupata taarifa kupitia usaili, mtafiti alilazimika kwenda uwandani (kwenye shule teule) ili kushuhudia namna ambavyo hali halisi ya utumiaji wa TEHAMA ilivyo katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili. Kwa kuwa hali ya shule moja inaweza kuwa tofauti na ya shule nyingine, mtafiti alifanya ushuhudiaji katika shule zote teule ili kupata picha halisi kuhusu utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

Mwisho, baada ya kupata taarifa kupitia usaili na ushuhudiaji, mtafiti alilazimika kuzichanganua matini ili kutimiza malengo ya utafiti. Mbinu hii ya uchanganuzi matini ilitumiwa ili kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Kwa kuwa watafiti wanatazama mambo kwa aina tofauti, nyaraka za watafiti tofauti, zilichanganuliwa na taarifa zilizopatikana zililinganishwa ili kupata mwongozo fasaha.

### 3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpango ulioandaliwa na unaoelezea njia na taratibu zilizopangwa kwa kusudi la kukusanya, kuchambua na kufasili data katika utafiti (Maxwell, 2013). Aidha, Tierney (2002) anasema kwamba usanifu wa utafiti unahusu mikakati na njia za uchambuzi ambazo zimechaguliwa na mtafiti ili kuunganisha vipengele vya utafiti kwa mantiki ili kuchunguza tatizo la utafiti kikamilifu. Usanifu wa utafiti unajumuisha mpango wa kukusanya, kupima na kufasili data katika utafiti. Kulingana na lengo kuu la utafiti la kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda, utafiti uliofanyika ulikuwa wa kitaamuli.

Chew-Graham, Carl & Mark (2001) wanasisitiza kwamba utafiti wa kitaamuli unahusisha maoni halisi, hisia na ufahamu wa washiriki wa utafiti kuhusu swala linalofanyiwa utafiti. Aidha, mtafiti wa kitaamuli anapaswa kuthamini uelewa na tafsiri za washiriki kuhusu ukweli wao wenyewe kama sehemu isiyoweza kutenganishwa na uzoefu wao wa maisha. Hivyo basi, kwa

kuwa utafiti wetu ulikuwa wa kitaamuli, data za kitaamuli ndizo tu zilizokusanywa na zilichanganuliwa, kufasiliwa na kuwasilisha kwa kutumia ruwaza za mkabala wa kitaamuli.

### 3.4 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni sehemu ya methodolojia ya utafiti inayoonyesha mwelekeo wa kijiografia na kitaaluma kwa kujikita katika mada ya utafiti. Ponera (2019) anasema kwamba eneo la utafiti lazima liainishe wazi mahali ambapo utafiti utafanyika. Utafiti ulifanyika nchini Rwanda kwenye wilaya ya Nyamasheke nchini Rwanda. Wilaya ya Nyamasheke ni wilaya ambayo iko karibu na mpaka wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hii ina maana kwamba katika wilaya hii kuna idadi kubwa ya wasemaji wa Kiswahili ikilinganishwa na maeneo mengine nchini Rwanda. Aidha, wilaya ya Nyamasheke pia ni miongoni mwa wilaya ambako mradi wa serikali wa kompyuta moja kwa kila mwanafunzi ulianzishwa, hususan katika wilaya zinazopakana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Hii ni kutokana na sababu za kihistoria na kijiografia, ikiwa ni pamoja na mabadilishano ya kitamaduni na mahusiano ya biashara na jamii zinazozungumza Kiswahili upande wa mpaka. Kulingana na Nyamutari (2020), maeneo ya mpaka yamepitia athari za lugha na mwingiliano ambao umechangia katika uwepo wa wasemaji wengi wa Kiswahili ukilinganisha na maeneo yasiyokaribiana na mpaka. Kwa hiyo, eneo hili lilitusaidia kupata taarifa zilizofaa katika kuchunguza nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

### 3.5 Wango na Sampuli ya Utafiti

#### 3.5.1 Wango la Utafiti

Kulingana na Williams, (2007), wango la utafiti ni kundi lote la watu au vitu vinavyochunguzwa katika utafiti. Wango la utafiti huweza kujumuisha idadi kubwa ya washiriki au vipengele vinavyohusiana na muktadha wa utafiti (Williams, khj).

Hivyo, wango la utafiti lilijumuisha walimu wa Kiswahili, wakurugenzi, wakuu wa masomo na wanafunzi wa shule za sekondari ambazo zina michepuo ya lugha katika Wilaya ya Nyamasheke, nchini Rwanda.

Shule za sekondari katika wilaya hii zilichaguliwa kushiriki kwa sababu zilitarajiwa kutoa taarifa muhimu kuhusu mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya

kuzungumza katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

### 3.5.2 Sampuli ya Utafiti

Cresswell, (2009) anasema kuwa, sampuli ya utafiti ni kundi la wawakilishi wanaochaguliwa kutoka kwenye jamii kubwa ya washiriki ili kutoa data inayowakilisha kundi lote. Kwa hiyo, utafiti ulitumia mbinu ya usampulishaji lengwa ili kuteua sampuli ya utafiti. Usampulishaji lengwa ni mbinu ya kuchagua sampuli ya utafiti kwa makusudi na kwa uangalifu, ambapo mtafiti huchagua washiriki kulingana na sifa au vigezo maalum vinavyolingana na lengo la utafiti (Palinkas, Horwitz, Green, Wisdom, Duan & Hoagwood, 2015).

Katika utafiti tuliofanya, sampuli ilihusisha wakurugenzi 5, wakuu wa masomo 5, walimu wa Kiswahili 5 na wanafunzi 115 ambao waliteuliwa katika shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda ambazo ni GS Mbuga, GS Tyazo, ES Tyazo, GS Kibogora na GS Karambi. Kwa kuwa kila shule ina mkurugenzi mmoja, mkuu wa masomo mmoja na mwalimu wa Kiswahili mmoja, sampuli hii ilihusisha wakurugenzi 5 (mmoja katika kila shule), walimu wakuu 5 (mmoja katika kila shule), walimu wa Kiswahili 5 (mmoja katika kila shule).

Wilaya ya Nyamasheke ina shule shule za sekondari nyingi, lakini kwa kusudi maalum, tano kati yake zilichaguliwa kwa umakini kwani ndizo zenye mchepuo wa lugha ambapo Kiswahili hufundishwa kama somo la lazima. Kwa upande wa wanafunzi, kwenye kila shule, wanafunzi wa kidato cha 6 katika mchepuo wa lugha walishirikishwa kwenye utafiti. Hii ni kwa sababu, mtafiti alilazimika kushuhudia somo la Kiswahili likifundishwa kwenye vidato vya sita vya mchepuo wa lugha katika shule teule wilayani Nyamasheke.

Kwa hiyo, sampuli ya utafiti ilihusisha wanafunzi 115 wanaojufunza katika kidato cha sita katika kila shule. Wanafunzi hawa waliteuliwa kwa makusudi kwa kuwa ndio ambao wana umahiri katika Kiswahili ukilinganisha na wanafunzi wa vidato vya chini.

Kwa hiyo, sampuli ya utafiti iliyoyochaguliwa ilitarajiwa kuwakilisha kikamilifu wango la utafiti na ilifaa sana katika utimizaji wa lengo la jumla na malengo mahususi ya utafiti.

### 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji wa data ni njia zinazotumika kukusanya taarifa za utafiti ambazo zitatumika kutoa muhtasari wa matokeo ya utafiti (Taherdoost, 2021). Katika utafiti wetu, tulitumia mbinu tatu tofauti za ukusanyaji wa data, yaani mahojiano, ushuhudiaji na uchambuzi wa matini. Mbinu hizi zilishirikiana kwa pamoja kuhakikisha ukusanyaji wa data unaofaa kufikia malengo mahususi ya utafiti.

#### 3.6.1 Mahojiano

Mahojiano ni mojawapo ya mbinu zenye matumaini zaidi za kukusanya data za kitamuli kwa kukutumia mawasiliano na mazungumzo kati ya mtafiti na washiriki wa utafiti (Turner, 2010). Aidha, Turner (khj) anasema kwamba, mbinu ya mahojiano inaruhusu watu kutoa taarifa zao kwa undani, kutoa ufafanuzi wa kina na kushirikisha uzoefu wao kwa njia inayosaidia kuchambua muktadha wa utafiti. Ni kumaanisha kwamba, kupitia mahojiano, mtafiti anapata fursa ya kuelewa vyema mitazamo, maoni na hisia za washiriki kuhusi swala linalofanyiwa utafiti.

Hivyo, tulitumia mbinu ya mahojiano kwa lengo la kukusanya data muhimu katika kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Data hizi zilikusanywa kutoka kwa wakurugenzi, wakuu wa masomo na walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari teule katika wilaya ya Nyamasheke. Mbinu hii ya mahojiano ilitoa fursa ya kupata taarifa moja kwa moja kutoka kwa washiriki na hivyo kuchangia katika kutimiza lengo la kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke, Nchini Rwanda.

Mbinu hii ya mahojiano ilikumbwa na upungufu wa kutoweza kupata taarifa zote kuhusu hali halisi ya nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

#### 3.6.2 Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni njia ambapo mtafiti huangalia na kurekodi tabia za watu binafsi au makundi katika mazingira yao ya asili bila kuingilia au kubadilisha vigezo vyovyote (George, 2023). Ushuhudiaji unaweza kutumika kujibu swali la utafiti kulingana na kile mtafiti anaona.

Lengo la uchunguzi ni kuelezea kigezo au vigezo kadhaa (George, khj). Kwa hiyo, ushuhudiaji ulitumiwa ili nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Kupitia mbinu ya ushuhudiaji, mtafiti hakuwezi kupata taarifa za upili kuhusu miongozo ya utumiaji wa TEHAMA iliyoundwa kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza. Taarifa kama hizi ni lazima zipatikane kwa kuwa zilikusudiwa kuchangia katika kutimiza lengo mahususi la pili la utafiti. Lengo hilo lilikuwa kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Hivyo basi, kwa kutimiza lengo hili, mbinu ya uchanganuzi wa matini ilitumika kwa kukamilisha mbinu ya mahojiano na ushuhudiaji.

### 3.6.3 Uchambuzi wa Matini

Bowen (2009) anasema kuwa, uchambuzi wa matini ni mbinu ya kukusanyia data inayojumuisha kupitia au kufafanua nyaraka, zikiwa ni pamoja na zile zilizochapishwa na zile za kielektroniki, ili kupata maarifa au taarifa kuhusu mada ya utafiti. Nyaraka zinazochambuliwa zinaweza kuwa za aina mbalimbali kama vile vitabu, tovuti, barua, ripoti, hati, makala na nyinginezo

Kwa hiyo, mbinu ya uchambuzi wa matini ilitumiwa kupitia njia ya kusoma kwa makini na kufasili matini tofauti zilizoandikwa na watafiti wa awali. Mbinu ya uchambuzi wa matini ilitumiwa ili kukusanya data za upili zilizofaa katika utimizaji wa lengo mahususi kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

## 3.7 Aina za Data Zilizokusanywa

Utafiti ulikusanya data za aina mbili ambazo ni data za asili na upili.

### 3.7.1 Data za Msingi

Data za msingi ni taarifa zinazopatikana moja kwa moja kutoka kwenye chanzo chake cha asili (Hox & Boeije, 2005). Data za msingi zilikusanywa kupitia mahojiano kati ya mtafiti na wakurugenzi, walimu wakuu, walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa shule za sekondari teule katika Wilaya ya Nyamasheke.

Kwa njia hii, tuliweza kukusanya taarifa moja kwa moja kutoka kwa washiriki na kuchangia katika kufikia lengo maalum la kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

### 3.7.2 Data za Upili

Hox & Boeije (whj) wanasema kuwa, data za upili ni aina ya data ambazo tayari zimekusanywa kwa madhumuni mengine. Mara nyingi, data hizi hukusanywa kutoka kwenye maandiko tofauti. Data za upili zilikusanywa kupitia mbinu ya uchambuzi wa matini.

Data hizi zilitumika kufikia lengo la kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

## 3.8 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti vimefafanuliwa na Ebrahim, (2016) kama kama zana zinazosaidia kwa ujumla katika shughuli za utafiti na zinazohusiana nazo. Vifaa vya Utafiti huwezesha watafiti kukusanya, kupanga, kuchambua, kubainisha kwa njia ya picha na kuchapisha matokeo ya tafiti zao (Ebrahim, khj). Vifaa vya utafiti vilivyotumiwa ni simu, kompyuta, kalamu, daftari, karatasi, na nyaraka tofauti.

## 3.9 Uchanganuzi wa Data

Kulingana na Belotto (2018), uchanganuzi wa data ni mazozi ya kushughulikia data ili kupata taarifa muhimu ambayo inaweza kushirika katika kufanya maamuzi yenye yanayofaa. Aidha, Belotto (khj) anasema kuwa, uchanganuzi wa data ni mchakato wa kukagua, kuchambua, kufasili na kuhakiki data kwa lengo la kugundua taarifa muhimu, kutoa suluhisho na kusaidia katika kufanya maamuzi yanayofaa.

Kwa hiyo, uchanganuzi wa data ulijiegemeza katika ruwaza za mkabala wa kitamuli. Hii ni kwa sababu utafiti ulikuwa wa kitamuli. Hivyo basi, data za utafiti zilichanganuliwa, kufasiliwa na kuwasilisha kwa kutumia madondoo na maelezo.

## 3.10 Itikeli ya Utafiti

Itikeli ya utafiti ni msingi muhimu wa utafiti ambao unanesha msimamo wa mtafiti kuhusu thamani, haki na hadhi za washiriki wa utafiti (Gajjar, 2013). Kwa kuweka wazi malengo yake

na kuzingatia heshima kwa washiriki, itikeli ya utafiti huchangia kujenga mazingira ya uwajibikaji na uwazi katika utafiti.

Kulingana na Cacciattolo (2015), kuhakikisha faragha, kutoa taarifa kwa hiari na kwa uwazi pamoja na kuheshimu haki za washiriki ni mambo muhimu yanayosaidia kuhakikisha kuwa utafiti unafanyika kwa njia inayofuata kanuni za maadili na kuleta mchango chanya kwa jamii. Kwa hiyo, kwa lengo la kuhakikisha itikeli ya utafiti, mambo yafuatayo yalifanyika.

Mosi, mtafiti alihakikisha ushiriki wa hiari wa washiriki wa utafiti. Hakuna mtu yeyote ambaye alishirikishwa katika utafiti kwa ushawishi, kwa tishio au kwa nguvu. Pili, kabla ya ukusanyaji data, mtafiti aliomba ridhaa kutoka kwa Chuo cha Rwanda na kwa wilaya ya Nyamasheke ambazo zilimsaidia kukusanya data katika shule tofauti katika wilaya husika.

Tatu, mtafiti aliwahakikishia washiriki wa utafiti kwamba taarifa watakazozitoa zitatumiwa vizuri na zitatumiwa kwa lengo la kukamilisha maelengo mahususi ya utafiti husika tu. Nne, tafiti aliwahakikishia washiriki wa utafiti kuwa hakuna madhara yoyote yatakayowafikia kutokana na taarifa walizozitoa. Tano, hakuna faranga zilizotolewa ili kupata data.

### 3.11 Uhalali na Uthabiti wa Utafiti

Uhalali wa utafiti unahusu kiasi ambacho utafiti unapima au kutathmini kwa usahihi lengo lake pamoja na kuhakikisha kuwa matokeo yanayopatika ni ya maana na yanaweza kuaminika (Arslan, 2022). Zaidi ya hayo, (Arslan, khj) anasema kwamba, uthabiti wa utafiti unahusu thabiti, hali ya kutobadilika na uwezekano wa kurudiwa kwa matokeo ya utafiti unapofanywa na watafiti tofauti. Uthabiti wa utafiti unaonesha kiasi ambacho utafiti hutoa matokeo thabiti na yanayoweza kuaminika wakati unapofanywa chini ya hali sawa. Kulingana na Kimberlin & Winterstein (2008), katika mchakato wowote wa utafiti, uhalali na uthabiti ni mambo muhimu kuzingatia. Kwa hiyo, ili kuhakikisha uhalali, mambo yafuatayo yalifanyika.

Kwanza, kabla ya kutumia vifaa vya utafiti, mtafiti alipima ufanisi wa kila kifaa kitakachotumiwa. Pili, kabla ya kutumika, zana za kukusanya data, matafiti alihakikisha kwamba kila mshiriki wa utafiti anaelewa kwa kina malengo ya utafiti. Tatu, mtafiti alihakikisha matumizi ya lugha ambayo inaeleweka kwa kila mshiriki wa utafiti bila kujali kiwango chake cha elimu.

Nne, mtafiti alijaribu kutumia mbinu ambazo zitamsaidia kuepukana na vikwazo vinavyoweza kutokea na kukabili mchakato wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Isitoshe, mtafiti alijaribu kufuata methodolojia ya utafiti katika kila hatua ya utafiti.

Aidha, ili kuhakikisha uthabiti, mtafiti alijiepusha na upendeleo wakati wa uchanganuzi, ufasili wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Hii ni kwa sababu mbinu za uchanganuzi wa data zilizotumiwa zilijiepusha na kuingiza maoni ya kibinafsi au mitazamo ambayo inaweza kusababisha upendeleo. Hivyo basi, mtafiti alihakikisha kuwa data zilizokusanywa ziliwasilishwa kama zilivyokuwa, bila kubadilishwa au kuongezwa kitu ili kuboresha matokeo. Hii ilihakikisha kwamba matokeo yaliyoyopatikana ni ya kuaminika na yataweza kutumika kama msingi wa maamuzi na mapendekezo yanayohusiana na utafiti uliofanyika.

### 3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii imetoa mwanga kuhusu methodolojia iliyotumiwa katika utafiti. Hivyo, sura hii ya tatu inajumuisha sehemu tofauti ambazo ni: utangulizi, paradima ya utafiti, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango na sampuli ya utafiti, mbinu za kukusanyia data, aina ya data zitakazokusanywa, vifaa vya utafiti, uchambuzi wa data, itikeli ya utafiti, uhalali na uthabiti wa utafiti na muhtasari wa sura tatu. Sura inajikita katika uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.

# SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, sura hii ina sehemu tofauti. Sehemu ya kwanza ni utangulizi. sehemu ya pili nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza. Sehemu ya tatu ni miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili. Sehemu ya mwisho ni muhtasari.

## 4.2 Nafasi ya TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza

Kwa mujibu wa Omidvar & Bahadorfar (2014) TEHAMA inajitokeza kama chombo kinachofaa kwa kukuza ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza lugha. Kwa hiyo, lengo mahususi la kwanza la utafiti lilikuwa kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Ili kutimiza lengo hili, tulijiegemeza kwenye mhimili wa kwanza na wa pili wa Nadharia ya Kuunganishwa ili kugundua namna ambavyo TEHAMA hushiriki katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza. Mhimili wa kwanza unaosisitiza kwamba, mabadiliko katika mawazo, hisia na tabia moja yanaweza kusababisha mabadiliko katika nyingine. Mhimili wa pili unaonesha kuwa akili inapaswa kueleweka kama mfumo mzima, sio kama mkusanyiko wa sehemu tofauti.

### 4.2.1 TEHAMA Hurahisisha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kuzungumza

Kwa mujibu wa Omidvar & Bahadorfar (2014), ni jukumu la kila mdau wa sekta ya elimu kuunga mkono mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazotegemea matumizi ya TEHAMA ili kuwaandaa wanafunzi kwa mahitaji ya ulimwengu wa kisasa. Kwa hiyo, kwenye utafiti wetu tulichanganua matini tofauti ili tutoe maelezo kuhusu nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza. Kwanza kabisa, matini tulizochanganua zimeonesha kwamba TEHAMA hurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza. Hii ni kwa sababu TEHAMA inatoa majukwaa mbalimbali ya mawasiliano ambayo yanawawezesha wanafunzi kufanya mazoezi ya kuzungumza kwa njia za kiubunifu na zenye mwingiliano zaidi.

Mifumo ya kujifunza kwa njia ya mtandao, kama vile majadiliano ya video na programu za kuboresha matamshi, inawapa wanafunzi fursa ya kujifunza kwa kasi yao wenyewe na kupata maoni ya papo hapo kutoka kwa walimu na wenzao. Hili linathibitishwa na dondoo la hapo chini:

> Technology can stimulate learners' playfulness and immerse them in various scenarios. It allows learners to engage in self-directed activities, providing opportunities for self-paced interactions, privacy, and a safe environment where errors are corrected, and specific feedback is given. Feedback from a machine offers additional value through its ability to track mistakes and immediately link students to exercises focusing on specific errors, thereby improving their speaking skills more easily.
> **Chanzo**: Omidvar & Bahadorfar (2014:11).

> Teknolojia inaweza kuchochea uchezaji wa wanafunzi na kuwazamisha katika hali mbalimbali. Inawapa wanafunzi nafasi ya kushiriki katika shughuli zinazoongozwa na wao wenyewe, fursa za mwingiliano wa kasi yao wenyewe, faragha na mazingira salama ambako makosa yanasahihishwa na maoni maalum yanatolewa. Maoni kutoka kwa mashini yanatoa thamani ya ziada kwa uwezo wa wanafunzi wa kufuatilia makosa na kuwaunganisha wanafunzi moja kwa moja na mazoezi yanayolenga makosa maalum, hivyo kuboresha stadi zao za kuzungumza kwa urahisi zaidi. (TY)

Dondoo hili linaonesha kuwa TEHAMA ina nafasi ya kuwasaidia wanafunzi kucheza na kujifunza katika mazingira salama, wakipata maoni maalum na kurekebisha makosa yao. Pia, maoni kutoka kwa mashine yanawasaidia wanafunzi kuboresha stadi zao za kuzungumza kwa urahisi zaidi. Kwa kuongezea, Abdelbaki (2021) anasema kwamba TEHAMA hurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza kupitia majukwaa yake kama inavyoonekana kwenye dondoo lifuatalo:

> ICT platforms have revolutionized the process of learning and teaching speaking skills for students. Through online resources and easily accessible learning tools provided by ICT, students have the opportunity to engage in speaking practice across various environments. Online training programs enable students to download learning materials related to speaking skills more easily.
> **Chanzo**: Fu (2021:114)

> Majukwaa ya TEHAMA yameleta mapinduzi makubwa katika mchakato wa kujifunza na kufundisha stadi ya kuzungumza kwa wanafunzi. Kupitia rasilimali za mtandaoni na zana za kujifunzia zinazopatikana kwa urahisi kwa kutumia TEHAMA, wanafunzi wanapata nafasi ya kushiriki katika mazoezi ya kuzungumza katika mazingira mbalimbali. Programu za mafunzo zinazopatikana mtandaoni zinawawezesha wanafunzi kupakua vifaa vya kujifunzia vinavyohusiana na stadi ya kuzungumza kwa urahisi zaidi. (TY)

Dondoo hili linaonesha kwamba nafasi ya TEHAMA katika mchakato wa kujifunza na kufundisha stadi ya kuzungumza imekuwa kubwa, kwani majukwaa ya TEHAMA yameleta mapinduzi makubwa. Kupitia rasilimali na zana za mtandaoni zinazopatikana kwa urahisi, wanafunzi sasa wanaweza kushiriki katika mazoezi ya kuzungumza katika mazingira mbalimbali na kupakua vifaa vya kujifunzia kwa urahisi zaidi. Vilevile, kupitia mahojiano na washiriki wa utafiti, ilibainika kwamba TEHAMA inafanya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza uwe rahisi. Kwa mfano, Mwalimu 1 alibainisha mchango wa TEHAMA kwenye dondoo lifuatalo:

> Matumizi ya TEHAMA yamenifanya niweze kuwashirikisha wanafunzi katika mazoezi ya kuzungumza kwa njia ya ubunifu zaidi. Kupitia majukwaa ya mtandaoni kama Zoom na Google Meet, tunaweza kufanya mijadala ya darasani na mazoezi ya kuzungumza kwa wakati halisi, hata kama hatuko katika eneo moja.

Dondoo hili linaonesha kwamba, matumizi ya TEHAMA yamewezesha walimu kuwapatia wanafunzi mazoezi ya kuzungumza kwa njia za ubunifu na za kuvutia zaidi. Wanafunzi wanaweza kushiriki mijadala na mazoezi ya kuzungumza kwa wakati halisi kupitia majukwaa ya mtandaoni, hata kama hawako kwenye eneo moja. Hii ina maana kwamba TEHAMA inarahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili. Kwa kuthibitisha hili, Mkuu wa Masomo 1 alitoa taarifa zifuatazo:

> Mimi ninaona kwamba mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili ni kurahisisha mchakato huu. Kupitia matumizi ya TEHAMA, inakuwa rahisi kuwashirikisha wanafunzi katika mazoezi ya kuzungumza kwa njia za ubunifu na zenye kuvutia zaidi. (TY)
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba mchango wa TEHAMA ni kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili. Dondoo hili linaonyesha kuwa mchango wa TEHAMA ni kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kwa urahisi zaidi. Pia, inaboresha ushiriki wa wanafunzi kupitia mbinu za kisasa zinazochochea mawasiliano ya kina na ufanisi. kwa kuongezea, Mkurugenzi 1 alitoa taariafa kwenye dondoo lifuatalo:

> Kwa kutumia TEHAMA katika shule yetu, tumeboresha kwa kiasi kikubwa ufundishaji wa stadi za kuzungumza. Vifaa vya mtandaoni vimewezesha wanafunzi kuingiliana na walimu na wenzao kwa urahisi zaidi, na pia vimewapa fursa ya kufanya mazoezi ya ziada nje ya muda wa darasa. Hatua hii imeongeza ubora wa elimu tunayoitoa na imetufanya kuwa miongoni mwa shule zinazoongoza katika matumizi ya TEHAMA kwa ufundishaji. (TY)
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba, matumizi ya TEHAMA shuleni yanaboresha sana ufundishaji wa stadi za kuzungumza kwa kurahisisha mwingiliano kati ya wanafunzi, walimu na wenzao. Vifaa vya mtandaoni pia vimewapa wanafunzi fursa ya kufanya mazoezi ya ziada nje ya darasa, na hii imeongeza ubora wa elimu ya walimu, na kutufanya kuwa shule inayoongoza katika matumizi ya TEHAMA kwa ufundishaji.

Data kutoka uchanganuzi matini na usaili zinaonesha kwamba TEHAMA ina mchango wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili. Hata hivyo, data za ushuhudiaji zinaonesha kwamba baadhi ya walimu wa Kiswahili hawana uwezo wa kutosha wa kutumia TEHAMA katika ukuzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili. Kwa mfano, katika shule moja ambapo mtafiti alifanya ushuhudiaji, mwalimu alipofika katika chumba cha kompyuta, alikuta kwamba vifaa havikuwa tayari kwa matumizi.

Mwalimu alishindwa kuviunganisha, hivyo alilazimika kuita mwalimu wa TEHAMA kwa msaada. Hali hii ilikuwa changamoto kwani kati ya dakika 40 zilizokuwa zimepangwa kwa somo, mwalimu alitumia dakika 25 pekee. Zaidi ya hayo, katika darasa hili, ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili haukuwa mzuri kwa sababu baadhi ya wanafunzi walikuwa kwenye programu ambazo hazihusiani na somo lililokuwa linafundishwa.

Aidha, ukosefu wa ujuzi wa TEHAMA na maarifa maalum kuhusu jinsi ya kuichanganya na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji huleta changamoto katika kusaidia wanafunzi kujifunza kwa ufasha (Fu, khj). Kwa hiyo, tunaona kwamba juhudi kadhaa zinahitajika ili kuepukana na changamoto kama hizi katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kupitia matumizi ya TEHAMA katika shule za sekondari wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

Kwa mujibu wa Vicent & Msigwa (2021), taasisi zinazohusika na ufundishaji wa Kiswahili zinalazimika kuandaa semina za mara kwa mara kuhusu matumizi ya vifaa vya TEHAMA, zikifundisha programu kama PowerPoint, Zoom na Skype. Semina hizi zitasaidia kupunguza

changamoto za matumizi ya TEHAMA kwa walimu na wanafunzi, hivyo kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

### 4.2.2 TEHAMA Huwezesha Upanikanaji Zana za Kisasa za Kufundishia Stadi za Kuzungumza

Ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza unahitaji zana ambazo zinawezesha wanafunzi kuzungumza lugha lengwa kwa ufanisi. Hii ni kwa sababu zana hizi huwapa wanafunzi fursa ya kufanya mazoezi ya mara kwa mara na kupata mrejesho wa papo hapo kutoka kwa walimu na wenzao (Emadhavi, 2023). Hata, hivyo, data tulizozipata kupitia uchanganuzi wa matini zimeonesha kwamba TEHAMA inatumiwa na walimu na wanafunzi wa lugha kwa kuwa inawawezesha kupata zana za kisasa za kufundishia stadi za kuzungumza. Hii ni kwa sababu TEHAMA inatoa vifaa vya kidijiti vinavyosaidia katika kuboresha mazoezi ya lugha kwa njia za kisasa na za kuvutia zaidi, huku pia ikitoa fursa za maoni ya papo hapo na marekebisho maalum. Mojawapo ya matini tuliyochanganua imetoa taarifa kwenye dondoo lifuatalo:

> Online course materials, for example, can be available 24 hours a day, 7 days a week. Online classrooms allow students and teachers to interact easily and simultaneously. Relying on ICT, learning and teaching no longer depend solely on printed materials. Various resources are abundantly available online, and speaking skills can be taught through videos, audio, visual presentations and so on.
> **Chanzo**: Abdelbaki (2021:113)
>
> Vifaa vya masomo mtandaoni, kwa mfano, vinaweza kupatikana saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. Madarasa ya mtandaoni yanawawezesha wanafunzi na walimu kuingiliana kwa urahisi na kwa wakati mmoja. Kutegemea TEHAMA, kujifunza na kufundisha sasa hakutegemei tena tu vifaa vya kuchapishwa. Rasilimali mbalimbali zinapatikana kwa wingi mtandaoni, na stadi za kuzungumza zinaweza kufundishwa kupitia video, sauti, maonyesho ya picha na kadhalika. (TY)

Dondoo hili linaonesha kwamba matumizi ya TEHAMA yanarahisisha upatikanaji wa zana za kufundishia stadi ya kuzungumza kwa kutoa vifaa vya masomo mtandaoni ambavyo vinapatikana kila wakati na kila siku. Aidha, madarasa ya mtandaoni yanawezesha wanafunzi na walimu kuingiliana kwa urahisi, huku rasilimali mbalimbali za kujifunzia kama video, sauti na picha zikipatikana kwa wingi na kwa urahisi mtandaoni.

Aidha, TEHAMA inawawezesha wanafunzi kukuza stadi zao za mazungumzo kupitia zana tofauti zinazopatikana mtandaoni. Hili linathibitishwa na dondoo lifuatalo:

> ICT is a widely recognized term and is extensively used globally to teach speaking skills. Students now utilize ICT in the classroom to learn how to speak a language fluently. Online teaching within the classroom is engaging and helps students find suitable materials for their needs. ICT allows us to gather data from various sources for any instruction. To enhance speaking skills, students can access and use different materials available online.
> **Chanzo**: Omidvar & Bahadorfar (2014:13).

> TEHAMA ni neno linalotambuliwa sana na linatumiwa kwa kiasi kikubwa duniani kote kufundisha stadi za kuzungumza. Wanafunzi sasa wanatumia TEHAMA darasani kujifunza jinsi ya kuzungumza lugha kwa ufasaha. Ufundi wa mtandaoni darasani unavutia na unawasaidia wanafunzi kupata vifaa vinavyowafaa. TEHAMA inaturuhusu kukusanya data kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya maelekezo yoyote. Ili kuboresha stadi za kuzungumza, wanafunzi wanaweza kufikia na kutumia vifaa mbalimbali vinavyopatikana mtandaoni. (TY)

Dondoo hili linaonesha kwamba TEHAMA inatambuliwa sana na inatumiwa duniani kote kufundisha stadi za kuzungumza. Kwa kutumia TEHAMA darasani, wanafunzi wanaweza kujifunza lugha kwa ufasaha, kupata vifaa vinavyowafaa, na kutumia rasilimali mbalimbali mtandaoni kuboresha stadi zao za kuzungumza. Hii ina maana kwamba, nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi za kuzunumza Kiswahili ni kuwezesha walimu na wanafunzi kupata zana faafu kwa urahisi. Zaidi ya hayo, nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili inathibitishwa na Mkurugenzi 2 kwenye dondoo lifuatalo:

> TEHAMA inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha stadi za kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi. Inawapa fursa ya kutumia zana za kisasa kama video na programu za lugha. Teknolojia hii inasaidia wanafunzi kufikia malengo yao ya kujifunza kwa ufanisi na kwa hamasa. (TY)
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kulingana na dondoo hili, TEHAMA inaboresha stadi za kuzungumza Kiswahili kwa kutoa zana za kisasa kama video na programu za lugha. Teknolojia hii inawawezesha wanafunzi kufanikisha malengo yao ya kujifunza kwa ufanisi na kwa motisha kubwa. Hivyo basi, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa TEHAMA ina nafasi kubwa katika kuboresha stadi za kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi, jambo linaloendana na mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya Kuunganishwa. Mhimili wa kwanza unahusu jinsi mabadiliko katika mawazo, hisia na tabia yanaweza kuathiriana. TEHAMA, kwa kutoa vifaa vya kisasa kama video na programu za lugha, inawasaidia wanafunzi kufikia malengo yao ya kujifunza kwa ufanisi.

Licha ya haya, maelezo haya yanaonesha kwamba fasihi inawezesha upatikanaji wa zana za kisasa za kufundishia stadi za kuzungumza Kiswahili. Katika utafiti wetu, tuliona kwamba

kwenye shule teule wilayani Nyamasheke, kuna changamoto za uhaba wa zana za TEHAMA. Katika shule hizi, ilionekana kwamba walimu hawafanikiwi kutumia TEHAMA kufikia zana za kufundishia stadi za kuzungumza. Hii ni kwa kuwa zana za TEHAMA ni haba kwenye shule husika. Kwa mfano, katika usaili, Mwalimu 2 alitoa taarifa zifuatazo:

> Changamoto za matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili ni pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kutosha na mtandao. Hapa shuleni, tuna kompyuta chache ambazo hazitoshi kwa kila mwanafunzi. Mara nyingine, ninapanga kufundisha somo kwa kutumia TEHAMA, lakini ninapofika kwenye chumba cha kompyuta, ninakuta kuna mwalimu mwingine. Kwa sababu kuna chumba kimoja cha kompyuta, wakati huo siwezi kufundisha somo langu kama nilivyopanga.
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kulingana na dondoo hili, changamoto kubwa za kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili ni upungufu wa vifaa na matatizo ya upatikanaji wa chumba cha kompyuta. Kwa mfano, mara nyingi kuna ukosefu wa kompyuta za kutosha na wakati mwingine, mwalimu anashindwa kufundisha somo kama ilivyopangwa kutokana na matumizi ya pamoja ya vifaa.

Data kutoka kwenye ushuhudiaji zilithibitisha kwamba kuna changamoto ya uhaba wa zana za TEHAMA za kufundishia stadi za mawasiliano. Kwenye shule nne ambapo ushuhudiaji ulifanyika, mwalimu alikuwa anafundisha somo la Kiswahili. Alikutana na changamoto ya ukosefu wa vifaa vya TEHAMA kama kompyuta za kutosha na projekta, hali iliyomlazimu kuendesha somo lake kama alivyokuwa amelipanga. Yeye, alishindwa kufundisha wanafunzi kuzungumza Kiswahili kutokana na upungufu wa vifaa na ukosefu wa mtandao. Hali hii ilileta machafuko darasani, kwani kila kundi la wanafunzi lilikuwa likimuita mwalimu mara kwa mara kulalamikia kwamba kompyuta yao haifanyi kazi. Jambo hili lilivuruga sana mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa mujibu wa Vicent & Msigwa (2021), uhaba wa vifaa vya kutosha vya kujifunzia na kufundishia Kiswahili ni mojawapo wa changamoto ambazo zinawakabili walimu na wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswalili.

Kwa kuepukana na changamoto hii, Vicent & Msigwa (2021) wanasema kwamba, serikali na taasisi binafsi zihakikishe upatikanaji wa vifaa vya kutosha vya TEHAMA kama kompyuta, projekta, simu za mkononi na vidonge katika maeneo yanayotoa mafunzo ya Kiswahili kwa wageni.

### 4.2.3 TEHAMA Huongeza Hamasa ya Kuzungumza Kiswahili

Ili mtu aweze kuzungumza lugha vizuri, ni lazima kuwepo kwa vichocheo vya kuongeza hamasa ya mtu huyo ya kuzungumza lugha husika. Kama hamasa hiyo haipo, ni rahisi kwa mwanafunzi kushindwa kuzungumza lugha hiyo (Anczewski,1987). Data tulizozipata kupitia uchanganuzi wa matini zimeonesha kwamba TEHAMA ina nafasi katika kuongeza hamasa ya kuzungumza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba matumizi ya TEHAMA yamewezesha wanafunzi kujihusisha zaidi na shughuli za kuzungumza, kuboresha ujasiri wao na kuongeza motisha yao katika kujifunza Kiswahili. Msigwa (2019) anaonesha nafasi ya TEHAMA katika ukuzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kwenye dondoo lifuatalo:

> TEHAMA inamfanya mwanafunzi ajifunze katika hali ya uhai zaidi bila kuchoka. Matumizi ya video nzuri na zenye ucheshi huwasukuma wajifunzaji lugha ya Kiswahili kupenda kujifunza lugha hiyo tofauti na ujifunzaji pasipo kutumia media za video. Kwa muktadha huo, wanafunzi huwa makini kufuatilia kile wanachojifunza kutokana na kuvutiwa na picha, video pamoja na sauti zinazoambatana na picha hizo. Kadhalika, TEHAMA humfanya mjifunzaji ajifunze kwa kutenda na hivyo kumwondolea uchovu; yaani "ujifunzaji kwa kutenda Njia hii humfanya mwanafunzi kuhusisha zaidi matumizi ya viungo vya mwili na akili katika kutafuta matini za kujifunzia.
> **Chanzo**: Vicent & Msigwa (2021:149)

Dondoo hili linaonesha kwamba TEHAMA inamuwezesha mwanafunzi kujifunza kwa hali ya uhai zaidi bila kuchoka, kwa kutumia video zenye ucheshi na picha kuvutia ambazo zinachochea kupenda kujifunza Kiswahili. Hii ina maana kwamba, TEHAMA inamuwezesha mwanafunzi kujifunza kwa kutenda, ikiondoa uchovu na kuongeza uhusiano wa viungo vya mwili na akili katika mchakato wa kujifunza. Zaidi ya hayo, Omidvar & Bahadorfar (2014) wanaonesha nafasi ya TEHAMA katika ukuzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kwenye dondoo lifuatalo:

> By using ICT, teachers and students access software's which are available online to develop speaking skills. By incorporating suitable software through computers the students will play it again and again with their own interest and try to improve their speaking skills, which are most essential in this modernized IT world. The usage of headphones in the lab makes the students to have interest over the subject and induces them to repeat again and again instead of feeling boredom.
> **Chanzo**: Omidvar & Bahadorfar (2014:12)

> Kwa kutumia TEHAMA, walimu na wanafunzi wanaweza kupata programu zinazopatikana mtandaoni ili kuboresha stadi za kuzungumza. Kuunganisha programu zinazofaa kupitia kompyuta kunawaruhusu wanafunzi kuzitumia mara kwa mara nyenzo kwa mafanikio yao katika ukuzaji wa stadi za kuzungumza, ambazo ni muhimu katika dunia ya kisasa ya kidijiti. Matumizi ya vipokea sauti

> katika maabara huongeza hamasa ya wanafunzi kwa somo na kuwahimiza kufanya mazoezi mara kwa mara, hivyo kusaidia kuepuka kuchoka na kuboresha stadi za kuzungumza. (TY)

Dondoo hili linaonesha kwamba TEHAMA inawasaidia walimu na wanafunzi kupata programu mtandaoni zinazowasaidia kuboresha stadi za kuzungumza. Aidha, matumizi ya vipokea sauti katika maabara yanachochea hamasa ya wanafunzi na kuwasaidia kufanya mazoezi mara kwa mara, hivyo kuboresha ujuzi wao wa kuzungumza na kupunguza uchovu. Hii ina maana kwamba walimu wa Kiswahili wanapaswa kutumia TEHAMA na programu mtandaoni ili kuboresha mbinu zao za kufundisha stadi za kuzungumza, na pia kutumia vipokea sauti katika maabara ili kuongeza hamasa na ufanisi wa wanafunzi katika kufanya mazoezi.

Aidha, mahojiano tuliyofanya yameonesha kwamba TEHAMA inawasaidia wanafunzi kuzungumza na wazawa wa Kiswahili kwa urahisi, kuboresha matamshi yao na kuongeza uzoefu wa kujifunza kwa njia za kisasa na za kuvutia. Wakati wa mahojiano Mwalimu 4, alitoa taarifa kwenye dondoo lifuatalo:

> TEHAMA ina mchango mkubwa katika kuvutia wanafunzi kuzungumza Kiswahili wanapofanya kazi na kwa kuzikiliza sauti na kutazama video. Kupitia TEHAMA, wanafunzi wanajifunza stadi za kuzungumza Kiswahili kwa kutumia vifaa vya kidijiti kama video, sauti, na mazoezi ya kiingiliano ambayo yanaongeza ushirikiano na kuvutia. Teknolojia hizi zinawasaidia wanafunzi kupata uelewa mzuri wa kuzungumza Kiswahili, huku wakifurahia mchakato wa kujifunza na kuboresha ufasaha wao kwa njia ya burudani.
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kulingana na dondoo hili, TEHAMA inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuvutia wanafunzi kuzungumza Kiswahili kwa kutumia vifaa vya kidijiti kama video na sauti, ambapo teknolojia hizi zinaimarisha uelewa wao na kuboresha ufasaha wao kwa njia ya burudani.

Mhimili wa pili wa Nadharia ya Kuunganishwa unaonesha kwamba akili inapaswa kueleweka kama mfumo mzima, si mkusanyiko wa sehemu tofauti. TEHAMA inachangia katika hili kwa kubadilisha mtindo wa ufundishaji na ujifunzaji, ambapo teknolojia inachangia kwa pamoja katika kuboresha stadi za kuzungumza kwa kuwamotisha wanafunzi.

Kwa hivyo, walimu wa Kiswahili wanapaswa kutumia TEHAMA kwa ufanisi ili kuongeza motisha na kuboresha uzoefu wa kujifunza kwa wanafunzi, kwa kuzingatia kuwa teknolojia hizi zinachangia katika mfumo mzima wa kujifunza stadi za kuzungumza Kiswahili.

### 4.2.4 TEHAMA Huwezesha Wanafunzi Kuzungumza na Wazawa wa Kiswahili

Data kutoka uchanganuzi wa matini zimeonesha kwamba nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili ni kuwezesha wanafunzi kuwasiliana na wazawa wa Kiswahili kwa urahisi. Hii ni kwa sababu, kupitia TEHAMA, wanafunzi wanaweza kufikia mitandao ya kijamii ambayo inawasaidia kuingiliana na wazawa wa Kiswahili, hivyo kuboresha stadi zao za kuzungumza lugha hii. Hili linathibitishwa na dondoo la hapo chini:

> Through ICT, social media platforms can facilitate free interaction with native speakers of a language. This interaction allows learners to improve their diction and pronunciation of words and phrases, which can significantly enhance the learning process.
> **Chanzo**: Siddig (2020:72)

> Kupitia TEHAMA, majukwaa ya mitandao ya kijamii yanawezakuwasaidia wanafunzi kuingiliana na wazawa wa lugha kwa bure. Mwingiliano huu unawawezesha wanafunzi kuboresha lafudhi na matamshi ya maneno na virai, jambo ambalo linaweza kuboresha kwa kiasi kikubwa mchakato wa kujifunza lugha. (TY)

Dondoo hili linaonesha kwamba TEHAMA inaruhusu majukwaa ya mitandao ya kijamii kuwezesha mwingiliano wa bure na wazawa wa lugha. Mwingiliano huu huwasaidia wanafunzi kuboresha lafudhi na matamshi yao, hivyo kuimarisha kwa kiasi kikubwa mchakato wa kujifunza. Aidha, data kutoka kwenye usaili zimeonesha kwamba TEHAMA inawezesha wanafunzi kuzungumza na wazawa wa Kiswahili. Jambo hili linawasaidia kuboresha ufasaha wanapozungumza Kiswahili. Mwalimu 3 alibainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili katika dondoo lifuatalo:

> TEHAMA ina nafasi muhimu katika ufundishaji ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza, iwe ni katika Kiswahili au lugha nyingine yoyote. TEHAMA inawasaidia wanafunzi kuzungumza na wazawa wa Kiswahili kwa urahisi. Kupitia TEHAMA, wanafunzi wanaweza kujifunza na kuiga matamshi bora ya lugha hiyo kwa urahisi zaidi.
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kulingana na dondoo hili, TEHAMA ina umuhimu mkubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza, ikiwemo Kiswahili. Inawasaidia wanafunzi kuzungumza kwa urahisi na kuiga matamshi bora ya lugha hiyo kwa kutumia teknolojia.

Tena, data kutoka ushuhudiaji zimethibitisha kwamba TEHAMA inawasaidia wanafunzi kuiga namna ambavyo wazawa wa Kiswahili au wataalamu wa lugha hii wanavyoizungumza. Wakati wa ushuhudiaji ilibainika kwamba, walimu wanapotaka kufundisha kuzungumza kwa kutumia TEHAMA, wanatumia nyimbo, mazungumzo, na filamu zinazohusisha mazungumzo kati ya wazawa wa Kiswahili. Hii inawezesha wanafunzi kuona na kusikia matumizi halisi ya lugha, jambo ambalo linasaidia katika kuongeza uelewa wao na kuboresha ufasaha wao.

Licha ya uhaba wa zana za kufanikisha matumizi ya mbinu hii, mbinu husika ilionesha kwamba ina mchango mkubwa katika kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Hii ni kwa sababu zana za TEHAMA kama video na sauti zinaweza kuonyesha mifano halisi ya mazungumzo ya lugha, hivyo kutoa mazingira halisi ya kujifunza. Walimu wanatumia nyenzo hizi kwa umakini ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa miundo ya lugha, intonations, na matamshi yanayohusiana na matumizi ya kila siku ya Kiswahili.

Hivyo basi, walimu wanalazimika kuhakikisha wanapata na kutumia zana za TEHAMA kwa ufanisi ili kuboresha ufundishaji wa stadi za kuzungumza. Ingawa kuna changamoto za upatikanaji wa zana hizi, ni muhimu kwa walimu kuzingatia matumizi ya teknolojia kwa lengo la kuimarisha uzoefu wa kujifunza wa wanafunzi. Kwa hivyo, walimu wanahitaji kuendelea kutafuta suluhu za uhaba wa zana hizi na kuhakikisha wanatumia mbinu za TEHAMA kwa njia inayokidhi mahitaji ya wanafunzi.

### 4.3 Miongozo ya Utumiaji wa TEHAMA katika Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili

Lengo mahususi la pili lilikuwa kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Ili kutimiza lengo hili, kwanza, mbinu ya usaili ilitumiwa. Pili, mtafiti alitumia mbinu ya uchanganuzi wa matini. Mwisho, mtafiti alijiegemeza kwenye mhimili wa tatu wa Nadharia ya Kuunganishwa ambayo iliasisiwa na Smith & Jones (2015). Mhimili huu unasisistizia muktadha, ambapo unaonesha kuwa michakato ya akili inashawishiwa na muktadha wa kijamii na kihisia wa mtu. Hivyo basi, sehemu hii ina sehemu tatu. Sehemu hizo ni pamoja na utumiaji wa Michezo ya KiTEHAMA, utumiaji wa mikutano ya video mtandaoni na utumija wa programu za mtandaoni za kufundishia na kujifunzia stadi za kuzungumza.

### 4.3.1 Utumiaji wa Michezo ya KiTEHAMA

Kuzungumza ni muhimu sana kwa wanafunzi wa lugha ya pili. Hata hivyo, bado wanafunzi wengi wanakumbana na matatizo katika stadi za kuzungumza lugha lengwa. Jambo hili linathibitishwa na wanafunzi kutoweza kuzungumza lugha lengwa vizuri, iwe darasani au nje ya darasa. Andriani& Syarif (2021) wanasema kwamba ukosefu wa stadi za kuzungumza lugha lengwa mara nyingi unatokana na mbinu za ufundishaji zisizo bora. Kuwaomba wanafunzi kuandika na kukariri mazungumzo na kuyawasilisha mbele ya darasa kunawafanya washindwe kuwasiliana katika hali halisi ya maisha (Andriani & Syarif, 2021). Watafiti hawa wanaonesha kwamba utumiaji wa michezo ni mbinu moja inayotoa sifa maalum za kuboresha stadi za kuzungumza. Kwa hiyo, kwenye sehemu hii tumejikita kwenye kutoa mongozo ya utumiaji wa michezo ya TEHAMA katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke.

Katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili, walimu wanaweza kutumia michezo mbalimbali ya TEHAMA. Kwa mujibu wa Pérez na García (2020:478), michezo hii inaweza kuwa msaada mkubwa katika maendeleo ya lugha ya pili. Mchezo wa kwanza ni Quizlet, ambao unaweza kutumika kwa ajili ya kufundisha na kujifunza msamiati pamoja na kutoa majibu kwa maswali. Mchezo wa pili ni Kahoot!, unaotumiwa kwa ajili ya mashindano ya kuzungumza kwa njia ya michezo.

Padlet ni mchezo wa tatu, ambao hutumiwa kuunda ubao wa majibu na majadiliano ya makundi. Socrative ni mchezo wa nne, unaotumiwa kwa ajili ya maswali ya papo hapo na majibu ya wanafunzi. Michezo hii hutoa mazingira yenye changamoto na yanayovutia ambayo yanasaidia kuboresha stadi za kuzungumza kwa wanafunzi (Pérez & García, 2020).

Katika utekelezaji wa michezo hii katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili, kwanza ni lazima mwalimu achague mchezo mmoja kulingana na mazingira ya darasa lake, vifaa vinavyopatikana na aina ya wanafunzi wake. Hii ni kwa sababu mhimili wa tatu wa nadharia ya kuunganishwa unasisitizia muktadha, ambapo unaonesha kwamba michakato ya akili inashawishiwa na muktadha wa kijamii na kihisia wa mtu. Kwa hivyo, uchaguzi wa mchezo unaopangwa kwa umakini unahakikisha kuwa unakubaliana na hali halisi ya darasa na mahitaji ya wanafunzi, hivyo kuongeza ufanisi wa michezo hiyo katika kuboresha stadi za kuzungumza.

Pili, ni lazima mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi kulingana na uwezo wao, mtindo wa kujifunza, na mahitaji maalum. Kugawanya wanafunzi katika makundi kunasaidia kuimarisha ushirikiano na kuongeza ushirikishwaji wao katika michezo. Kila kundi linaweza kushughulikia majukumu maalum, kama vile kutekeleza mazungumzo au kushindana katika michezo ya kuzungumza, kulingana na uwezo wao. Hii inachangia katika kuwezesha wanafunzi wote kushiriki kwa ufanisi na kupokea msaada unaohitajika kutoka kwa wenzao. Kulingana na Hsu & Ching (2013**)**, njia bora ya kuwafanya wanafunzi wa lugha kuzungumza ni kuwaweka katika makundi madogo wanapocheza michezo ya kuzungumza au kukamilisha majukumu. Hii inawapa fursa ya kufanya mazoezi ya kuzungumza kwa lugha lengwa bila woga wa kuwasilisha mbele ya darasa zima.

Tatu, mwalimu anapaswa kuandaa vifaa na rasilimali zinazohitajika kwa mchezo uliochaguliwa kabla ya kipindi cha darasa. Hii inaweza kujumuisha kuandaa kompyuta, vifaa vya sauti au programu maalum zinazohitajika kwa mchezo. Kuwa na vifaa vilivyo tayari kabla ya darasa husaidia kupunguza muda wa kupoteza na kuhakikisha kuwa kipindi kinaendeshwa kwa ufanisi. Hii pia inasaidia kutoa mazingira ya kujifunza yaliyoandaliwa vizuri, ambayo ni muhimu kwa mafanikio ya michezo ya TEHAMA.

Nne, mwalimu anapaswa kufuatilia na kutathmini maendeleo ya wanafunzi wakati wa mchezo. Hii inaweza kufanywa kwa kutumia viashiria vya mafanikio, kama vile usahihi wa majibu, ushirikiano kati ya wanafunzi na ufanisi katika kutumia Kiswahili. Kufuata maendeleo ya wanafunzi husaidia mwalimu kubaini maeneo yanayohitaji uboreshaji na kutoa mrejesho wa mara moja ili kuboresha matumizi ya michezo. Pia, tathmini hii inasaidia kubaini michezo inayofaa zaidi kwa darasa.

Mwisho, ni muhimu mwalimu kufunga kipindi kwa kutoa muhtasari wa mambo yaliyofundishwa na kuzingatia mafanikio yaliyopatikana. Katika hatua hii, mwalimu anaweza kujadili na wanafunzi kuhusu uzoefu wao wa mchezo, changamoto walizokutana nazo na jinsi michezo ilivyosaidia katika kuboresha stadi zao za kuzungumza. Hii husaidia katika kuimarisha uelewa wa wanafunzi kuhusu umuhimu wa michezo katika ujifunzaji na kuwahamasisha kuendelea kutumia mbinu hizi katika masomo yao ya baadaye.

Katika utekelezaji wa michezo hii katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili, kwanza ni lazima mwalimu achague mchezo mmoja kiulingana na mazingira ya darasa lake, vifaa vinavyopatikana na aina ya wanafunzi wake. Hii ni kwa sababu

### 4.3.2 Utumiaji wa Mikutano ya Video Mtandaoni

Kwa kuwa mikutano ya video inaruhusu kuondoa umbali wa kijiografia, inaweza kutumika na walimu wa lugha za kigeni wanaotaka kuepukana na changamoto za ukosefu wa mazoezi ya kuzungumza (Loranc, 2015). Mikutano ya video huwafungulia wanafunzi fursa ya mwingiliano wa kweli ambapo uzoefu wa mawasiliano unaweza kupanuliwa. Kwa kutumia teknolojia hii, wanafunzi wanapata nafasi ya kuzungumza na watu kutoka sehemu mbalimbali za dunia, hivyo kuongeza ujuzi wao wa kuzungumza na kujifunza zaidi kuhusu tamaduni mbalimbali (Loranc, 2015). Kwa hiyo, kwenye sehemu hii tumejikita kutoa mwongozo wa utumiaji wa mikutano ya video mtandaoni katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke.

Katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili, mikutano ya video mtandaoni kama Zoom, Microsoft Teams, Google Meet, na Skype inaweza kutoa fursa muhimu. Zoom, kwa mfano, hutoa vyumba vya mazungumzo vidogo vidogo, hivyo kusaidia mazoezi ya kuzungumza kwa makundi madogo (Loranc, 2015).

Microsoft Teams ni bora kwa ushirikiano wa muda mrefu na usimamizi wa miradi, ikisaidia katika kuandaa shughuli za kujifunza (Andriani & Syarif, 2021). Google Meet inatoa huduma rahisi na bure kwa watumiaji wa Google Workspace, ikirahisisha upatikanaji wa mikutano (Pérez & García, 2020). Skype, kwa upande mwingine, imejijengea jina kama jukwaa la muda mrefu la kuzungumza, ikitoa uwezo wa mazungumzo ya moja kwa moja (Loranc, 2015). Kwa hiyo, kwa kutumia mikutano ya video mtandaoni, walimu wa Kiswahili wanaweza kuunda mazingira halisi ya mawasiliano ambapo wanafunzi wanaweza kuzungumza na watu kutoka sehemu mbalimbali, kuboresha ujuzi wao wa lugha na kuelewa tamaduni tofauti.

Katika utekelezaji wa mbinu ya utumiaji wa mikutano ya video mtandaoni kwa ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili, hatua ya kwanza ni kuweka malengo wazi na kulinganisha na mahitaji ya wanafunzi. Mwalimu anapaswa kufafanua malengo ya mikutano ya video, kama vile kuboresha mawasiliano ya muktadha halisi au kuimarisha ujuzi wa lugha kupitia mwingiliano wa

video. Malengo haya yanapaswa kuwa na athari kwa muktadha wa kijamii wa wanafunzi, ili kuhakikisha kuwa mikutano ya video inawasaidia kufikia malengo ya kielimu kwa ufanisi.

Hatua ya pili ni kuchagua jukwaa la mikutano ya video ambalo linaendana na mazingira ya darasa na uwezo wa vifaa vilivyo. Mwalimu anapaswa kuchagua jukwaa kama Zoom, Google Meet, au Skype kulingana na mahitaji ya darasa, kama vile huduma za vyumba vya mazungumzo vidogo au ushirikiano wa muda mrefu. Uchaguzi wa jukwaa unapaswa kuzingatia muktadha wa kijamii na kihisia wa wanafunzi, kuhakikisha kuwa mazingira ya kujifunza yanabaki kuwa ya kuvutia na yenye motisha.

Hatua ya tatu ni kutoa mafunzo ya awali kwa wanafunzi kuhusu matumizi ya jukwaa la mikutano ya video. Mwalimu anapaswa kuwasaidia wanafunzi kuelewa jinsi ya kujiunga na mikutano, kutumia zana zinazopatikana, na kushiriki katika mazungumzo. Mafunzo haya yanapunguza wasiwasi kuhusu teknolojia na kuimarisha uhusiano wa kijamii kati ya wanafunzi na jukwaa. Kwa kuwa muktadha wa kihisia wa wanafunzi unaweza kuathiri jinsi wanavyojihisi kuhusu matumizi ya teknolojia, mafunzo haya yanapaswa kuwa ya kusaidia na kujenga kujiamini.

Hatua ya nne ni kupanga ratiba ya mara kwa mara ya mikutano ya video ili kutoa fursa kwa wanafunzi kuzungumza na watu kutoka sehemu mbalimbali. Mwalimu anapaswa kupanga mikutano mara kwa mara kwa ajili ya mazungumzo na wenzao, walimu, au wageni wa nje. Ratiba hii inasaidia kuunda mazingira halisi ya mawasiliano ambapo wanafunzi wanapata nafasi ya kuimarisha stadi zao za kuzungumza katika muktadha wa kijamii wa kimataifa.

Hatua ya mwisho ni kutathmini matumizi ya mikutano ya video kulingana na mrejesho kutoka kwa wanafunzi. Mwalimu anapaswa kuchunguza jinsi wanafunzi wanavyoshiriki na kutoa mrejesho kuhusu utendaji wao.

Kurekebisha mikakati kulingana na matokeo ya tathmini na mrejesho inasaidia kuboresha ufanisi wa mafunzo na kuhakikisha kwamba mikutano ya video inajumuisha muktadha wa kijamii na kihisia wa wanafunzi, ikichangia katika kuimarisha uzoefu wa kujifunza. Kwa kufuata hatua hizi, walimu wa Kiswahili wanaweza kufanikiwa kufundisha stadi za kuzungumza Kiswahili kwa ufanisi na kwa urahisi zaidi.

### 4.3.3 Utumija wa Programu za Mtandaoni za Kufundishia na Kujifunzia Stadi za Kuzungumza

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unabadilika kila wakati kutokana na maendeleo ya kimataifa. Katika sekta ya elimu, matumizi ya TEHAMA yanabadilika mara kwa mara kutokana na kuongezeka kwa mwenendo wa utandawazi. Hii imeleta mabadiliko na mageuzi katika nyanja ya elimu katika karne hii ya 21. Hivyo basi, katika jitihada za kuunganisha TEHAMA katika ufundishaji, wataalamu wameunda programu mtandaoni kwa ajili ya kufundisha stadi za kuzungumza na kusikiliza. Idris, Megat, Abdul & Ya (2021:203). Kwa hiyo, kwenye sehemu hii tumejikita kutoa mwongozo wa utumiaji wa programu za mtandaoni za kufundishia na kujifunzia stadi za kuzungumza katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke.

Katika utekelezaji wa mbinu hii katika wilaya ya Nyamasheke ambapo upatikanaji wa zana za TEHAMA ni mdogo, hatua ya kwanza ni kufanya tathmini ya mahitaji ya wanafunzi na walimu pamoja na hali halisi ya rasilimali zilizopo. Hii inajumuisha kutathmini vifaa vya kiufundi kama vile kompyuta au simu za mkononi, pamoja na upatikanaji wa intaneti.

Kwa kuwa mahitaji ya wanafunzi yanaweza kuwa tofauti, ni muhimu kuainisha changamoto maalum zinazokabiliwa na wanafunzi katika mazungumzo na kuchagua programu zinazoweza kusaidia, kama vile programu rahisi na zinazopatikana kwa urahisi kama Zoom au WhatsApp.

Baada ya tathmini, chagua programu za mtandaoni zinazofaa kulingana na mahitaji yaliyoainishwa. Katika mazingira haya, programu kama Zoom na whatsapp zinaweza kuwa msaada mkubwa kwa sababu zinahitaji upatikanaji wa intaneti wa kawaida na zinaweza kusaidia katika mazoezi ya mazungumzo kwa kutumia makundi ya video au sauti. Hakikisha kuwa umepata uelewa wa kina kuhusu jinsi ya kutumia programu hizi na jinsi ya kuziendesha kwa ufanisi, ili uweze kutoa mwongozo wa kutosha kwa wanafunzi.

Unda mpango wa mafunzo unaojumuisha matumizi ya programu za mtandaoni kwa kipindi chote cha somo. Mpango huu unapaswa kueleza jinsi programu zitakavyotumika, jinsi wanafunzi watakavyohusishwa, na malengo ya kila kipindi. Kwa mfano, unaweza kupanga vikao vya mtandaoni mara mbili kwa wiki kwa mazoezi ya mazungumzo, huku ukiweka ratiba ya shughuli na majukumu ya nyumbani yanayohusiana na matumizi ya programu. Hii itasaidia kuweka

mwendo mzuri wa mchakato wa kufundisha na kuhakikisha wanafunzi wanapata mazoezi ya kutosha.

Ili kuhakikisha matumizi ya programu za mtandaoni yanakuwa na tija, ni muhimu kufanya tathmini ya mara kwa mara ya maendeleo ya wanafunzi. Hii inaweza kufanywa kwa kutumia vipimo vya mara kwa mara, maoni ya wanafunzi, na uchambuzi wa mazoezi yaliyokamilishwa. Tathmini hizi zitakusaidia kubaini maeneo yenye changamoto na kuamua kama kuna haja ya kubadilisha mbinu au programu zinazotumika. Marekebisho haya yanaweza kuwa muhimu ili kuhakikisha mbinu zako za kufundishia zinakuwa bora na zinaendana na mahitaji ya wanafunzi.

Hatua ya mwisho ni kutoa mafunzo na msaada kwa walimu na wanafunzi kuhusu matumizi ya programu za mtandaoni. Walimu wanapaswa kupata mafunzo kuhusu jinsi ya kutumia programu, jinsi ya kuanzisha vikao vya mtandaoni, na jinsi ya kusimamia mazoezi. Vile vile, wanafunzi wanahitaji mwongozi kuhusu jinsi ya kutumia programu, jinsi ya kushiriki katika mazungumzo ya mtandaoni, na jinsi ya kutatua matatizo yanayoweza kutokea. Kupitia mafunzo haya, wote wataweza kutumia teknolojia kwa ufanisi zaidi, hivyo kuboresha stadi za kuzungumza za wanafunzi.

### 4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura ya nne inahusu mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Sehemu ya kwanza ni utangulizi. Sehemu ya pili nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza. Sehemu ya tatu ni miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili. Sehemu ya mwisho ni muhtasari.

# SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura ya tano katika utafiti wetu ndiyo sura ya mwisho. Sura hii inajumuisha sehemu tano, ambazo ni utangulizi, muhtasari wa matokeo ya utafiti, ufaafu wa nadharia ya utafiti, hitimisho, na mapendekezo na muhtasari.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti wetu ulikusudia kutimiza malengo mahususi mawili. Kwanza, kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Pili, kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda.

### 5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo la kwanza la utafiti wetu lilikuwa kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Matokeo ya utafiti kuhusu lengo hili yameonesha kuwa TEHAMA ina nafasi kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili.

Kwanza, TEHAMA hurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza. Hii ni kwa sababu TEHAMA inatoa majukwaa mbalimbali ya mawasiliano ambayo yanawawezesha wanafunzi kufanya mazoezi ya kuzungumza kwa njia za kiubunifu na zenye mwingiliano zaidi. Pili, TEHAMA inatumiwa na walimu na wanafunzi wa lugha kwa kuwa inawawezesha kupata zana za kisasa za kufundishia stadi za kuzungumza. Tatu, TEHAMA ina nafasi katika kuongeza hamasa ya kuzungumza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Nne, matumizi ya TEHMA yamewezesha wanafunzi kujihusisha zaidi na shughuli za kuzungumza, kuboresha ujasiri wao na kuongeza motisha yao katika kujifunza Kiswahili. Tano, TEHAMA inatumiwa ili kuwezesha wanafunzi kuwasiliana na wazawa wa Kiswahili kwa urahisi. Hii ni kwa sababu, kupitia TEHAMA, wanafunzi wanaweza kufikia mitandao ya kijamii ambayo inawasaidia kuingiliana na wazawa wa Kiswahili, hivyo kuboresha stadi zao za kuzungumza lugha hii.

Hata hivyo, matokeo yanaonesha kuwa kuna changamoto za utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili. Kwanza, upungufu wa vifaa vya TEHAMA kama tarakilishi na matatizo ya upatikanaji wa chumba cha kompyuta yanakwamisha ufanisi wa ufundishaji, huku ukosefu wa ujuzi wa kutumia programu za TEHAMA ukiwa changamoto nyingine. Kupambana na hizi changamoto, mbinu zilizobainishwa ni kuandaa semina kuhusu matimizi ya TEAMA katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili. Aidha, shule na tasisi nyingine zinalazimika kuhakikisha kuwa kuna zana za TEHAMA za kutosha katika ufundishaji na ujifunzahi wa Kuzungumza Kiswahili

### 5.2.2 Lengo Mahususi la Pili

Lengo la pili la utafiti lilikuwa ni kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda. Ili kufanikisha hili, mbinu tatu tolewa mwongozo:

Kwanza, utafiti unatowa miongozo ya utumiaji wa michezo ya KiTEHAMA kama Quizlet, Kahoot!, Padlet na Socrative, ili kuboresha stadi za kuzungumza. Michezo hii inatoa mazingira ya changamoto na yanayovutia, na inahitajika kuendana na muktadha wa darasa, uwezo wa wanafunzi, na vifaa vilivyo.

Pili, mwongozo unajumuisha utumiaji wa mikutano ya video mtandaoni kama Zoom, Microsoft Teams, Google Meet, na Skype. Teknolojia hii inaruhusu mwingiliano wa kweli na watu kutoka sehemu mbalimbali, hivyo kuboresha ujuzi wa mazungumzo na kuelewa tamaduni.

Tatu, mwongozo unatoa mapendekezo ya kutumia programu za mtandaoni kama Zoom na WhatsApp, hasa katika mazingira yenye upatikanaji mdogo wa zana za TEHAMA. Hatua muhimu ni kufanya tathmini ya mahitaji, kuchagua programu zinazofaa, na kuunda mpango wa mafunzo unaojumuisha matumizi ya programu hizi kwa ufanisi.

## 5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti Iliyotumika

Kulingana na malengo ya utafiti, Nadharia ya Kuunganishwa ilitumika kama msingi wa nadharia. Nadharia hii, iliyoanzishwa na Smith & Jones (2015), inapendekeza kwamba mawazo, hisia, na tabia zote zinahusiana na kuathiriana.

Mhimili wa kwanza wa nadharia hii unasisitizia jinsi mawazo, hisia, na tabia zinavyohusiana na kuathiriana, ambapo mabadiliko katika sehemu moja yanaweza kusababisha mabadiliko katika sehemu nyingine. Katika utimizaji wa lengo mahususi la kwanza la kubainisha nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili, mihimili hii ilisaidia kuelewa jinsi TEHAMA inavyoweza kuathiri michakato ya mawazo, hisia, na tabia za wanafunzi. Hii ilichangia kubaini jinsi TEHAMA inaweza kuimarisha uzoefu wa kujifunza kwa kuboresha mwingiliano wa mawazo, hisia, na tabia zinazohitajika katika kujifunza Kiswahili.

Mhimili wa pili wa nadharia, mtazamo jumuishi, unaonesha kuwa akili inapaswa kueleweka kama mfumo mzima, sio kama mkusanyiko wa sehemu tofauti. Katika utimizaji wa lengo mahususi la kwanza, mhimili huu ulisaidia kuelewa jinsi zana tofauti za TEHAMA zinavyoweza kuunganishwa ili kuboresha stadi za kuzungumza Kiswahili. Kwa kuwa elimu ni mchakato wa kimfumo unaohitaji ushirikiano wa sehemu mbalimbali, mtazamo huu ulifanikisha kubaini jinsi TEHAMA inavyoweza kuwa sehemu ya mfumo mzima wa mchakato wa elimu, badala ya kipande kimoja tu. Hii ilisaidia kuhakikisha kwamba matumizi ya TEHAMA yalikuwa sehemu ya mkakati mzima wa ufundishaji na ujifunzaji.

Mhimili wa tatu wa nadharia ya kuunganishwa unasisitizia muktadha, ambapo unaonesha kwamba michakato ya akili inashawishiwa na muktadha wa kijamii na kihisia wa mtu. Katika utimizaji wa lengo mahususi la pili la kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA, mhimili huu ulisaidia kubaini jinsi muktadha wa kijamii na kihisia wa wanafunzi unavyoweza kuathiri matumizi ya TEHAMA katika kujifunza Kiswahili.

Kwa kuzingatia hali halisi ya darasa, vifaa vinavyopatikana, na mahitaji maalum ya wanafunzi, mwongozo ulipangwa ili kuhakikisha kwamba matumizi ya TEHAMA yanakubaliana na muktadha wa wanafunzi na kuboresha ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 5.4 Hitimisho

Kwa kuhitimisha, utafiti ulionesha umuhimu mkubwa wa TEHAMA katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyamasheke. Matokeo yanathibitisha kuwa TEHAMA si tu inarahisisha mazoezi ya kuzungumza kupitia majukwaa ya mawasiliano, bali pia inasaidia kuongeza hamasa, ujasiri, na motisha ya wanafunzi.

Ingawa kuna changamoto za upatikanaji wa vifaa na ujuzi wa matumizi, mbinu zilizopendekezwa kama vile matumizi ya michezo ya KITEHAMA, mikutano ya video, na programu za mtandaoni zinatoa suluhu nzuri kwa matatizo haya. Kwa kuzingatia mihimili ya Nadharia ya Kuunganishwa, utafiti umeweza kubaini jinsi TEHAMA inavyoweza kuathiri michakato ya mawazo, hisia, na tabia, na jinsi muktadha wa kijamii na kihisia unavyoweza kuimarisha matumizi yake. Hii inatoa mwanga kuhusu jinsi TEHAMA inavyoweza kuwa sehemu muhimu ya mfumo mzima wa elimu, hivyo kuboresha stadi za kuzungumza Kiswahili kwa ufanisi zaidi.

## 5.5 Mapendekezo

### 5.5.1 Mapendekezo kwa Wanafunzi

Ili kuboresha stadi zao za kuzungumza Kiswahili kwa kutumia vifaa vya TEHAMA vilivyopo shuleni, nyumbani, au mahali pengine, wanafunzi wanashauriwa kuchangamkia fursa zinazotolewa na teknolojia kwa kufanya mazoezi mara kwa mara kwenye majukwaa ya mtandaoni kama YouTube, Quizlet, na Kahoot! Aidha, wanapaswa kutumia mikutano ya video kama Zoom au Google Meet kwa mazungumzo ya mara kwa mara na wazungumzaji wa Kiswahili. Ni muhimu kwao kuunda ratiba ya kujifunza na kujitolea kwa muda wa ziada kwa kutumia vifaa vya TEHAMA ili kuboresha ujasiri na ufanisi wao katika kuzungumza Kiswahili.

### 5.5.2 Mapendekezo kwa Walimu wa Kiswahili

Walimu wanashauriwa kutumia zana za TEHAMA kwa ufanisi katika kufundisha stadi za kuzungumza Kiswahili kwa kuzingatia vifaa kama tarakilishi, simu, na mitandao ya kijamii. Ni muhimu kwao kujifunza kutoka kwa wenzao na kushiriki katika mafunzo yanayoandaliwa kuhusu matumizi bora ya TEHAMA. Walimu wanapaswa pia kushiriki katika mafunzo ya kitaalamu yanayohusu mbinu za matumizi ya TEHAMA ili kuendeleza ujuzi wao na kuboresha mbinu za ufundishaji wao.

### 5.5.3 Mapendekezo kwa Viongozi wa Shule

Viongozi wa shule wanashauriwa kufanya advocacy ili shule zao zipate zana za TEHAMA za kisasa kama tarakilishi na vifaa vya mafunzo.

Pia, wanapaswa kuhakikisha kuwa walimu wanashiriki katika mafunzo kuhusu matumizi ya TEHAMA na kuunga mkono mipango ya kuongeza upatikanaji wa vifaa. Kwa kuimarisha

ushirikiano na wadau, viongozi wa shule wanaweza kusaidia kuandaa mazingira yenye rasilimali za kutosha kwa ajili ya ufundishaji bora wa Kiswahili.

### 5.5.4 Mapendekezo kwa Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda

Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda inashauriwa kuanzisha mikakati ya kitaifa ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika shule za msingi na sekondari. Inapaswa kuwekeza katika ununuzi na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA kwa shule zote, pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu kuhusu matumizi ya teknolojia katika ufundishaji. Aidha, bodi inapaswa kuhakikisha kwamba sera za elimu zinahusisha matumizi ya TEHAMA kama sehemu muhimu ya mtaala wa Kiswahili, ili kuongeza ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 5.5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Watafiti wengine wanalazimika kufanya tafiti kuhusu mada zifuatazo ili kuendelea kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kupitia TEHAMA. Kwanza, kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu athari za matumizi ya michezo ya kidijitali katika kuboresha stadi za kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa sekondari. Pili, tafiti zinahitajika kuchunguza jinsi mazingira ya kujifunza kwa kutumia TEHAMA yanavyoweza kuboreshwa ili kuongeza ushirikiano kati ya wanafunzi na walimu.

Tatu, utafiti unapaswa kufanywa kuhusu changamoto na suluhisho za kiufundi katika utekelezaji wa TEHAMA kwa shule za vijijini ambazo zina upatikanaji mdogo wa vifaa vya teknolojia. Nne, kuna umuhimu wa kufanya utafiti kuhusu mbinu bora za mafunzo ya walimu katika matumizi ya TEHAMA kwa kufundisha lugha. Hatimaye, utafiti unahitajika kuhusu athari za muda mrefu za matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa lugha kwa maendeleo ya kitaaluma na kijamii ya wanafunzi.

## 5.6 Muhtasari wa Sura ya Tano

Sura ya tano inahusu hitimisho la jumla la utafiti. Sura hii imeonesha muhtasari wa matokeo ya utafiti. Sura hii pia imejadili ufaafu wa nadharia iliyoongoza utafiti. Isitoshe, sura hii imetoa mapendekezo kwa wanafunzi, walimu, viongozi wa shule na watafiti wengine.

# MAREJELEO


Abdelbaki, Z. (2021). The Role of Using Information and Communication Technologies (ICTs) in Enhancing English as a Foreign Language (EFL) Learners' Speaking Skill: A Review of Literature. *Bhartiyam International Journal of Education & Research*, 12(2), 113-125. Retrieved from https://doi.org/10.13140/RG.2.2.17804.69768.

Ahmadi, M. (2018). The Impact of Technology On Teaching and Learning in Higher Education: A Systematic Review. *Journal of Educational Technology and Online Learning*, 1(1), 1-20

Akram, H., Abdelrady, A. H., Al-Adwan, A. S., & Ramzan, M. (2022). *Teachers' Perceptions of Technology Integration in Teaching-Learning Practices.* A Systematic Review. Frontiers in Psychology, 13. https://doi.org/10.3389/fpsyg.2022.920317.

Anand, G., Larson, E. C., & Mahoney, J. T. (2020). Thomas Kuhn on Paradigms. *Wiley Online Library*, 29(7), 1650-1657. https://doi.org/10.1111/poms.13188.

Anczewski, J. (1987). Review of the Book *Social psychology and Second Language Learning: The Role of Attitudes and Motivation*, by R. Gardner. *Second Language Research, 3*(2), 180-182. Sage Publications, Ltd.

Andriani, D., & Syarif, H. (2021). Using Communicative Games to Improve Students' Speaking Skill. *Proceedings of the Eighth International Conference on English Language and Teaching (ICOELT-8 2020)*. 597(1), 128-130. https://doi.org/10.2991/assehr.k.210914.024.

Arslan, E. (2022). Validity and Reliability in Qualitative Research. Pamukkale University. *Journal of Social Sciences Institute*, 6(2), 312-324.

Arung, F. (2016). *Improving the Students' Speaking Skill through Debate Technique*. https://www.researchgate.net/publication/302900141.

Bellon, Joe, A. (2000). *Research-based Justification for Debate across the Curriculum*. Atlanta. Georgio State University Press.

Belotto, M. (2018). *Data Analysis Methods for Qualitative Research*: Managing the Challenges of Coding, Interrater Reliability, and Thematic Analysis. The Qualitative Report. https://doi.org/10.46743/2160-3715/2018.3492.

Benmeddah, W. (2017). *The Use of ICT in Developing the Speaking Skill in EFL Classes*: Case of First Year EFL Students at the University of Tlemcen. Improve students' speaking skill. *Project (Professional Journal of English Education),* 2(3), 416. https://doi.org/10.22460/project.v2i3.p416-420.

Bhatti, M. S. (2021). Teaching Speaking Skills through Role Play at Elementary Level: An Analysis. *Jurnal Arbitrer*, 8(1), 93–100. https://doi.org/10.25077/ar.8.1.93-100.2021.

Billon, M., Marco, R., & Lera-Lopez, F. (2017). Innovation and ICT use by firms and households in the EU. *Information Technology & People*, 30(2), 424–448. https://doi.org/10.1108/ITP-05-2015-0098.

Bilyalova, A. (2016). ICT in Teaching a Foreign Language in High School. *Procedia-Social and Behavioral Sciences*, 237(3), 175-181.

Bowen, G. A. (2009). Document Analysis as a Qualitative Research Method. *Qualitative Research Journal*, 9(2), 27–40. https://doi.org/10.3316/QRJ0902027.

Cacciattolo, M. (2015). *Ethical Considerations in Research*. In The Praxis of English Language Teaching and Learning. SensePublishers. https://doi.org/10.1007/978-94-6300-112-0_4.

Carrier, M. (2017). Automated Speech Recognition in language learning: Potential models, benefits and impact. *Training Language and Culture*, 1(1), 46–61. https://doi.org/10.29366/2017tlc.1.1.3.

Chapelle, C. A., & Sauro, S. (2017). *The Handbook of Technology and Second Language Teaching and Learning*. Wiley. https://doi.org/10.1002/9781118914069.

Chen, X. (2020). The Impact of Social Anxiety on EFL Learners' Oral Communication in Online Environments. *International Journal of Instruction*, 13(2), 187-202.

Chew-Graham, C. A., Carl, R. M. & Mark, S. P. (2001). Qualitative Research and the Problem of Judgement: Lessons from Interviewing Fellow Professionals. *Family Practice*, 19(3), 285-289.

Chirag, P. (2003). Use of Multimedia Technology in Teaching and Learning Communication Skill. *International journal of Research Academics*, 17 (5), 473–495.

Chun, D., Kern, R., & Smith, B. (2016). Technology in Language Use, Language Teaching, and Language Learning. *The Modern Language Journal*, 100(1), 64-80. https://doi.org/10.1111/modl.12302.

Creswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Davis, N. (2017). *The Interconnected Mind: Integrating Cognitive Science with Interpersonal Communication*. New York: Routledge.

Ebrahim, N. A. (2016). *Introduction to the "Research Tools" for Research Methodology Course*. https://doi.org/10.6084/m9.figshare.3187673.v1.

Emadhavi, L. F. (2023). Developing Learners' English-Speaking Skills using ICT and AI Tools. *Journal of Advanced Research in Applied Sciences and Engineering Technology*, 32(2), 142–153. https://doi.org/10.37934/araset.32.2.142153.

Froehling, A. (2023). *Language Acquisition with Video Games*: Adult Learning Game-based Learning K12. https://www.filamentgames.com/blog/language-acquisition.

Fu, J. S. (2013). ICT in education: A critical Literature Review and Its Implications. *International Journal of Education and Development using Information and Communication Technology (IJEDICT)*, 9(1), 112-125.

Gajjar, N. B. (2013). Ethical Consideration in Research. *International Journal for Research in Education,* 2(7), 8-15.

Garcia, M. (2021). The Importance of Speaking Skills in Second Language Acquisition. *TESOL Quarterly,* 55(2), 345-362.

George, T. (2023). *What Is an Observational Study?* | Guide & Examples. Scribbr. Retrieved 20 February 2024, from https://www.scribbr.co.uk/research-methods/observational-study/.

Ghavifekr, S. & Rosdy, W.A.W. (2015). Teaching and Learning with Technology: Effectiveness of ICT integration in schools. *International Journal of Research in Education and Science (IJRES)*, 1(2), 175-191.

Graziano, A.M. & Raulin, M.L. (2006). *Research Methods*: A Process of Inquiry, (6th Ed.) Boston, MA: Allyn & Bacon.

Holmqvist, M. (2019). *Lack of Qualified Teachers: A Global Challenge for Future Knowledge Development.* In Teacher Education in the 21st Century. IntechOpen. https://doi.org/10.5772/intechopen.83417

Hussain, S. (2017). Teaching Speaking Skills in Communication Classroom. *International Journal of Media, Journalism and Mass Communication*s, 3(3), 14-21. https://doi.org/10.20431/2454-9479.0303003.

Hox, J. J., & Boeije, H. R. (2005). Data Collection, Primary vs. Secondary. *Encyclopedia of Social Measurement*, 20 (1), 593–599. . https://doi.org/10.1016/B0-12-369398-5/000414.

Hsu, H.-Y., & Ching, Y.-H. (2013). The Effects of Online Games On Students' Speaking Skills in an EFL context. *Educational Technology & Society, 16*(4), 123-134. https://www.jstor.org/stable/23612238.

Ibrahim, A. (2016). The Use of Technology in Language Classroom in Libya. *International Journal of Social Science and Humanity*. 6 (4), 262-267. DOI:10.7763/IJSSH2016.V6.655.

Idayani, A., & Sailun, B. (2017). Roles of Integrating Information Communication Technology (ICT) in Teaching Speaking at the First Semester of English Students oF FKIP UIR. J-SHMIC : *Journal of English for Academic*, 4(2), 12-23. https://doi.org/10.25299/jshmic.2017.vol4(2).603.

Idris, S. L., Megat, P. R., Abdul, Z. I., & Ya, S., M. S. (2021). Approaching Listening and Speaking Skills Using Online to Facilitate Interactive Learning from Students' Perspectives. *Asian Journal of University Education, 17*(2), 203-214. https://doi.org/10.24191/ajue.v17i2.13400.

Johnson, K. (2008). The Negative Affect focus effect: Distinct Roles of Rumination and Emotional Reactivity. *Journal of Personality and Social Psychology*, 94(3), 523-534.

Kevogo, S. A. (2017). Kiswahili katika Kufundishia TEHAMA katika Shule za Msingi Nchini Tanzania: Umuhimu na Changamoto zake. *Kioo cha Lugha*, (13) 52-64.

Kim, J. and Craig, D. (2012). Validation of a Video Conferenced Speaking Test. *Computer Assisted Language Learning*, 25 (7), 257-268.

Kimberlin, C. L., & Winterstein, A. G. (2008). Validity and Reliability of Measurement Instruments Used in Research. *American Journal of Health-System Pharmacy*, 65(23), 2276-2284. https://doi.org/10.2146/ajhp070364.

Kivunja, C., & Kuyini, A. B. (2017). Understanding and Applying Research Paradigms in Educational Contexts. *International Journal of Higher Education*, *6*(5), 26. https://doi.org/10.5430/ijhe.v6n5p26.

Kovac, M. M., & Mrsic, A. (2017). Students' Attitudes towards Foreign Languages. *Journal of Educational and Developmental Psychology*, 7(2), 124-137. https://doi.org/10.5539/jedp.v7n2p124.

Kuhn, T.S. (1962). *The Structure of Scientific Revolutions*. London: University of Chicago Press Ltd.

Kumar, S., & Tammelin, M. (2014). The Role of Technology in Language Learning: A Study of the Effectiveness of Technology-Enhanced Language Teaching**.** *International Journal of Language and Linguistics*, *1*(2), 113-120. https://doi.org/10.11648/j.ijll.20140102.15.

Kurum, E. Y. (2016). Te*aching Language Skills for Prospective English Teachers Teaching Speaking Skills*. Istanbul Aydin University Perikan Editors.

Lechman, E., Kutrzeba, F., & Mustakoski, K. (2020). ICT and social development. Routledge Society and Technology 3(2), 1–12. https://doi.org/10.4324/9780429278945-1.

Lightbown, P.M. & Spada, N. (2006): How Languages Are Learned. Oxford: Oxford University Press.

Loranc, B. (2015). Videoconferencing as a Tool for Developing Speaking Skills. In *Advances in Intelligent Systems and Computing. 14*(4), 123-134. https://www.jstor.org/stable/23612238.

Marlina, R. (2018). *Teaching Language Skills*. In The TESOL Encyclopedia of English Language Teaching. Wiley. https://doi.org/10.1002/9781118784235.eelt0665.

Maulana, A., Musthafa, I., & Hayati, T. N. (2020). The Efficiency of Teaching Listening and Speaking Skills to Develop Students' Communicative Competences. *Universal Journal of Educational Research*, 8(3), 802–808. https://doi.org/10.13189/ujer.2020.080310.

Maxwell, J. (2013). *Qualitative research design: An interactive approach (3rd ed.)*. Thousand Oaks, CA: Sage.

Mertens, D. M. (2012). What Comes First? The Paradigm or the Approach? *Journal of Mixed Methods Research*, 6(4), 255-257. https://doi.org/10.1177/1558689812461574.

Miltenoff, P. (2004). Effective Teaching with Technology in Higher Education: Foundation for Success (review). Portal. *Libraries and the Academy*, 4(2), 300–302. https://doi.org/10.1353/pla.2004.0034.

Mofareh, A. A. (2019). The Use of Technology in English Language Teaching. *Frontiers in Education Technology*, 2(3), p168. https://doi.org/10.22158/fet.v2n3p168.

Mohanta, R., Mahato, R. C., & Sutradhar, A. (2023). Use of ICT in Language Learning. *International Journal of Research and Review*, 10(4), 139-43. https://doi.org/10.52403/ijrr.20230418.

Msigwa A (2019). Mchango wa Media za Video katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni. *Mulika*, 38(4), 74-86.

Mullamaa, K. (2010). ICT in Language Learning - Benefits and Methodological Implications. *International Education Studies*, 3(1). https://doi.org/10.5539/ies.v3n1p38.

Nanai, N. E. (2023). Challenges of Teaching and Learning of Speaking Skills in Secondary Schools in Tanzania. International Journal of Language and Education Research, 5(2), 53–77. https://doi.org/10.29329/ijler.2023.591.3.

Negoescu, G., & Bastina-Bratu, S. (2016). ICT - A Key Element of the Modern Education System. *Journal of Knowledge Management, Economics and Information Technology*, 6(4), 1–9.

Newcombe, J., & Brick, B. (2017). Blending Video Games into Language Learning. *International Journal of Computer-Assisted Language Learning and Teaching*, 7(4), 75-89. https://doi.org/10.4018/IJCALLT.2017100106.

Nyamutari, J. (2020). Linguistic Diversity and Dynamics in Border Regions: A Case Study of Kiswahili Speakers in Gisenyi and Kamembe, Rwanda. *Journal of African Languages and Linguistics*, 42(3), 456-469.

Omidvar, R., & Bahadorfar, M. (2014). *Technology in Teaching Speaking Skill*. In Technology in Teaching Speaking Skill Article in International Journal of Multidisciplinary Research Review. http://www.aijmr.net.

Pérez, C., & García, J. (2020). The Effectiveness of Online Games in the Development of Speaking Skills for Language Learners. *Journal of Language Teaching and Research, 11*(3), 473-480. https://doi.org/10.17507/jltr.1103.14.

Palinkas, L. A., Horwitz, S. M., Green, C. A., Wisdom, J. P., Duan, N., & Hoagwood, K. (2015). Purposeful Sampling for Qualitative Data Collection and Analysis in Mixed Method Implementation Research. *Administration and Policy in Mental Health and Mental Health Services Research*, 42(5), 533–544. https://doi.org/10.1007/s10488-013-0528-y.

Passey, D & Goodison, R. (2004). *The motivational Effect of ICT on Pupils*. University of Lancaster. DfES Publications.

Pervin, N., & Mokhtar, M. (2022). The Interpretivist Research Paradigm: A Subjective Notion of a Social Context. *International Journal of Academic Research in Progressive Education and Development*, *11*(2). https://doi.org/10.6007/IJARPED/v11-i2/12938.

Phillips, M. (2010). The Perceived Value of Video Conferencing with Primary Pupils Learning to Speak a Modern Language. *Language Learning Journal*, 38(5), 221–238.

Pizarro, C. G. (2022). Students' Perception of Interacting with Native Speakers. *LETRAS*, 72, 165–192. https://doi.org/10.15359/rl.2-72.7.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma- Central Tanganyika Press.

Qasserras, L. (2023). Systematic Review of Communicative Language Teaching (CLT) in Language Education: A Balanced Perspective. *European Journal of Education and Pedagogy*, 4(6), 17-23.

Rao, P. P. (2018). Developing Speaking Skills in ESL or EFL Settings. *International Journal of English Language, Literature and Translation Studies*, 5(2), 286-293. https://doi.org/10.33329/ijelr.52.286orhttp://www.ijelr.

Rao, P. S. (2019). *The Importance of Speaking Skills in English Classrooms*. www.acielj.com.

Ratheeswari, K. (2018). Information Communication Technology in Education. Journal of *Applied and Advanced Research*, 6(2), 45–S47. https://doi.org/10.21839/jaar.2018.v3iS1.169.

Reid S. (2002). The Integration of ICT into Classroom Teaching. *Alberta Journal of Educational Research*, 48 (2), 30-46.

Saville, N. (2015). *Computer tutor. University of Cambridge*. Retrieved from http:// www.cam.ac.uk/research/features/computer/tutor/sthash.NmmbdTSh.dpuf.

Siddig, B. E. (2020). Social Media in Teaching of Languages. *International Journal of Emerging Technologies in Learning (IJET),* 15(12), 72. https://doi.org/10.3991/ijet.v15i12.12645.

Smith, A., & Jones, B. (2015). Interconnectionism: exploring the close relationships between Mental Processes, Emotions, and Behaviors. *Journal of Psychology*, 20(3), 45-58.

Smith, S. (2003). Online Video Conferencing: An application to Teacher Education. *JSTE E Journal*, 18 (2), 62–65.

Sulistyaningrum, S. D. (2019). *ICT-Based Learning in Public Speaking at English Language Education Study Programme*. Proceedings of the 1st International Conference on Education Social Sciences and Humanities (ICESSHum 2019). https://doi.org/10.2991/icesshum-19.2019.127.

Taherdoost, H. (2021). *Handbook on Research Skills*: The Essential Step-By-Step; Guide on How to Do a Research Project (Kindle ed.): Amazon.

Thienthong, A., & Lian, A. (2014). *The Use of Internet Resources and Applications for Language Instruction*. https://www.researchgate.net/publication/279771125.

Thornbury, S. (2005). *How to teach speaking*. U.K.: Pearson.

Tierney, A. J. (2002). Research Design in Social Research. *International Journal of Nursing Studies*, 39(6), 669–670. https://doi.org/10.1016/S0020-7489(01)00040-2.

Turner III, D. W. (2010). Qualitative Interview Design: A Practical Guide for Novice Investigators. *The qualitative Report*, 15(3), 754.

Vicent, S. & Msigwa, A. (2021). Umuhimu na Changamoto za TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa Wageni. *MULIKA*, 40(2), 142-157.

Wang, Y. (2007). Task design in Videoconferencing-Supported Distance Language Learning. *CALICO Journal*, 24(3), 590–630.

Whelan, R. (2008). Use of ICT in education in the South Pacific: findings of the Pacific eLearning Observatory. *Distance Education*, 29 (5), 53-70.

Williams, C. (2007). Research Methods. *Journal of Business & Economic Research*, 5(3), 65-72.

Wu, J., Lee, J., Schmidt, T., Heil, C. R., Wu, J. S., & Lee, J. J. (2016). A Review of Mobile Language Learning Applications: Trends, Challenges and Opportunities.*The EUROCALL Review*, 24(2), 205-217. https://www.researchgate.net/publication/313346126.

Wulandari, W., Ayuningtias, D. O., & Yana, Y. (2019). The Use of Role Play to Improve Students' Speaking Skill. *Project (Professional Journal of English Education)*, *2*(3), 416. https://doi.org/10.22460/project.v2i3.p416-420.

Yasim, I. M. Md., Lubis, M. A., Noor, Z. A. M., & Kamarudin, M. Y. (2016). The Use of Teaching Aids in the Teaching and Learning of Arabic Language Vocabulary. *Creative Education*, 07(03), 443–448. https://doi.org/10.4236/ce.2016.73044.

Yuan, Z., & Briscoe, T. (2016). Grammatical Error Correction Using Neural Machine Translation. In Proceedings of the 2016 Conference of the North American Chapter of the Association for Computational Linguistics: *Human Language Technologies*, 8 (3), 380-386.

Zake, P., & Akinyemi, A. O. (2020). Challenges in Teaching and Learning Speaking Skills in Secondary Schools in Nigeria. *International Journal of Education and Research*, 8(4), 231-242.

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho I. Mwongozo wa Usaili kwa Walimu wa Kiswahili**

i) Je, ni zana zipi za TEHAMA unazotumia ili kukuza stadi za kuzungumza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wako?

ii) Unatumiaje zana za kiTEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili?

i) Ni changamoto zipi unazokumbana nazo katika ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili

ii) Ni mbinu gani unazotumia ili kuepukana na changamoto zinazokabili ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili?

iii) Je, TEHAMA ina mchango gani katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili?

iv) Je, ni mbinu gazi zinazoweza kutumiwa ili kuunda mwongozo wa kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyamasheke nchini Rwanda? (What are the effective methods that can be used to develop a guide for improving the teaching and learning of Kiswahili speaking skills for secondary school students in selected schools in Nyamasheke district, Rwanda?)

**Kiambatisho II. Mwongozo wa Usaili kwa Wakuu wa Masomo na Wakurugenzi**

i) Je, ni zana zipi za TEHAMA zinazotumiwa na mwalimu wa Kiswahili katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kwenye shule yenu?

ii) Je, mwalimu wa Kiswahili anatumia vipi zana za TEHAMA katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kwenye shule yenu?

iii) Je, ni changamoto zipi anazokabiliana nazo mwalimu wa Kiswahili anapofundisha stadi za kuzungumza Kiswahili kwa kutumia TEHAMA?

iv) Ni mbinu gani ambazo mwalimu wa Kiswahili anaweza kutumia ili kuepukana na changamoto za ufundishaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili kupitia matumizi ya TEHAMA?

v) Je, TEHAMA ina mchango gani katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kuzungumza Kiswahili?

**Kiambatisho III. Mwongozo wa Ushuhudiaji**

<table>
<tr><td colspan="3">1) Mchango wa TEHAMA Katika Ufundishaji na Ujifunzaji Wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili kwa Wanafunzi wa Shule za Sekondari Teule Wilayani Nyamasheke Nchini Rwanda</td></tr>
<tr><td rowspan="2">a) Mwalimu anapoandaa somo la kuzungumza anabainisha zana za TEHAMA ambazo atazitumia?</td><td>Ndiyo</td><td>Hapana</td></tr>
<tr><td>Maoni<br>……………..</td><td>Maoni<br>…………………….</td></tr>
<tr><td rowspan="2">b) Mwalimu anapofundisha stadi za kuzungumza Kiswahili anatumia TEHAMA?</td><td>Ndiyo</td><td>Hapana</td></tr>
<tr><td>Maoni<br>……………..</td><td>Maoni<br>…………………….</td></tr>
<tr><td rowspan="2">c) Je, mwalimu anatumia TEHAMA anapotathmini stadi za kuzungumza Kiswahili?</td><td>Ndiyo</td><td>Hapana</td></tr>
<tr><td>Maoni<br>……………..</td><td>Maoni<br>…………………….</td></tr>
<tr><td>d) Je, ni zana gani za TEHAMA anazotumia mwalimu anapofundisha somo la kuzungumza Kiswahili?</td><td colspan="2">………………………………………..</td></tr>
<tr><td>e) Mwalimu anatumiaje TEAHAMA anapofundisha stadi za kuzungumza Kiswahili?</td><td colspan="2">………………………………………..</td></tr>
</table>

<table>
<tr><td colspan="2">2. Changamoto za Ufundishaji wa Stadi za Kuzungumza Kiswahili katika Shule za Sekondari Wilayani Nyamasheke Nchini Rwanda</td></tr>
<tr><td>Changamoto</td><td>Mikakati ya Kuepukana na Changamoto</td></tr>
<tr><td>a) ………………………………..</td><td>a). ………………………………..</td></tr>
<tr><td>b) ………………………………..</td><td>b). ………………………………..</td></tr>
<tr><td>c) ………………………………..</td><td>c). ………………………………..</td></tr>
<tr><td>d) ………………………………..</td><td>d) ………………………………..</td></tr>
</table>

**Kiambatisho IV. Mwongozo wa Uchanganuzi Matini kuhusu Mwongozo wa Utumiaji wa TEHAMA katika Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili**

| Jina la Matini (Mada), Mwandishi na Mwaka | Mwongozo wa Utumiaji wa TEHAMA katika Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza | Maelezo kuhusu Mwongozo wa Utumiaji wa TEHAMA katika Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza | Namna ya Utekelezaki wa Mwongozo wa Mwongozo wa Utumiaji wa TEHAMA katika Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**Kiambatisho V. Idhini ya Itikeli ya Utafiti**

UNIVERSITY of RWANDA

COLLEGE OF EDUCATION

**RESEARCH AND INNOVATION OFFICE**

Rukara, 27th May, 2024
Ref: DRI-CE/006(a)/ EN/gi/2024

**Emmanuel NIYOBUHUNGIRO**
**Reg N°: 218001026**
Master Student
Master of Education in Kiswahili Education
School of Education
UR-CE

Dear Mr Niyobuhungiro,

**RE: RESEARCH ETHICAL CLEARANCE FOR YOUR STUDY**

Following your application for research clearance for your study entitled: **"The Contribution of ICT in Teaching and Learning Kiswahili Speaking Skills: A Case of Selected Secondary Schools in Nyamasheke District, Rwanda;"**

Having reviewed your application and being satisfied with your protocol (your research topic, interview schedule, and informed consent): your study is ethically acceptable. This ethical clearance shall last for 12 months and is renewable upon your request and presentation of the progress report to the UR-CE Research Screening and Ethics Clearance Committee (RSEC-C) through the Research and Innovation Unit. Please note that you will have to apply for ethical clearance before making changes in the protocol during the implementation phase. The Research and Innovation Unit shall receive a final copy of your study report at the end of your study.

We wish you success in your study.

COLLEGE OF EDUCATION
UNIVERSITY of RWANDA
RESEARCH AND INNOVATION UNIT

**Assoc. Prof. Eugene NDABAGA**
Chairperson, UR-CE RSEC-C
Director of Research and Innovation Unit
Tel.: 250788308862
Email: ndabagav@yahoo.ie
UR-College of Education
**Cc:**

- The Principal, CE
- Dean, School of Education
- Dr Wallace K. Mlaga, Supervisor

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw P.O. Box 55 Rwamagana WEBSITE: www.ur.ac.rw

**Kiambatisho VI. Barua ya Chuo ya Kukusanya Data**

UNIVERSITY of RWANDA

COLLEGE OF EDUCATION

RESEARCH AND INNOVATION UNIT

Rukara, 27th May 2024
Ref: DRI-CE/006(b)/EN/gi/2024

**The Mayor**
**Nyamasheke District**
**Western Province**
**Rwanda**

**Re: Research recommendation letter for Mr Emmanuel NIYOBUHUNGIRO (Reg N°: 218001026)**

I am pleased to introduce Mr **Emmanuel Niyobuhungiro:** our student enrolled in the "Master of Education in Kiswahili Education in the Department of Humanities and Language Education of the School of Education at UR-CE. He is conducting research entitled: **"The Contribution of ICT in Teaching and Learning Kiswahili Speaking Skills: A Case of Selected Secondary Schools in Nyamasheke District, Rwanda."** This research will involve students studying languages, Kiswahili teachers, Deans of Studies, and Head Teachers from selected secondary schools in Nyamasheke district.

Thus, we kindly request his permission to collect data from identified schools of the concerned district.

Your support to him in conducting this study is highly appreciated.

Yours sincerely.

COLLEGE OF EDUCATION — UNIVERSITY of RWANDA — RESEARCH AND INNOVATION UNIT

**Assoc. Prof. Eugene NDABAGA**
Director of Research and Innovation
University of Rwanda-College of Education
E-mail: ndabagav@yahoo.ie
Mobile: +250788308862
**Cc:**

- Principal, UR-CE
- Dean School of Education
- Dr Wallace K. Mlaga (Supervisor)

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw P.O. Box 55 Rwamagana WEBSITE: www.ur.ac.rw

**Kiambatisho VII. Kibali cha Wilaya cha Kukusanya Data**

REPUBLIC OF RWANDA

WESTERN PROVINCE
NYAMASHEKE DISTRICT

Ref N° 6103/03.07/2024 Nyamasheke 13 JUN 2024

Dear NIYOBUHUNGIRO Emmanuel
Email: niyobuhungiroemmanuel9@gmail.com
Phone: +250781787564

RE: Authorization to carry out a research

With reference to your letter received on 29th May 2024 requesting to carry out a research on the topic, **"The Contribution of ICT in Teaching and Learning Kiswahili Speaking Skills: A Case of Selected Secondary Schools in Nyamasheke District".**

After analyzing the nature of your topic, I am pleased to inform you that you are allowed to conduct this research in Nyamasheke District. We request you to observe all research ethics related to the nature of your topic and to share with us the findings of your research and the recommendations.

Please accept our best wishes.

**MUPENZI Narcisse**

Mayor of Nyamasheke District

Cc:
- The Vice Mayors (Both)
- The District Executive Secretary
- Corporate Services Division Manager
- District Director of Education
  **NYAMASHEKE**

**Kiambatisho VIII. Mpango Kazi wa Utafiti**

| | SHUGHULI | MWAKA WA 2023 | | | | MWAKA WA 2024 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Sep | Okt | Nov | Des | Jan | Feb | Mch | Apr | Mei | Jun | Jul | Ago | Sep |
| 1 | Kuandaa sura ya kwanza ya utafiti | | | | | | | | | | | | | |
| 2 | Kuandika sura ya pili ya utafiti | | | | | | | | | | | | | |
| 3 | Kuandaa sura ya methodolojia ya utafiti | | | | | | | | | | | | | |
| 4 | Kukamilisha pendekezo la utafiti | | | | | | | | | | | | | |
| 5 | Kuomba ridhaa za kukusanya data | | | | | | | | | | | | | |
| 6 | Kukusanya data | | | | | | | | | | | | | |
| 7 | Kukamilisha sura ya nne ya na ya tano ya tasnifu | | | | | | | | | | | | | |
| 8 | Kukusanya na kutetea tasnifu na kuandaa makala ya tasnifu | | | | | | | | | | | | | |
| 9 | Kutuma makala ya tasnifu katika jalida fulani kwa ajili ya uchapishaji | | | | | | | | | | | | | |

Chanzo (Mtafiti, 2024)

Imetayarishwa na:

Jina: Niyobuhungiro Emmanuel

Sahihi:

Imeidhinishwa na Msimamizi:

Jina: Dkt. Wallace Kapele Mlaga

Sahihi:

**Kiambatisho IX. Ripoti ya Mfanano**

TEHAMA NA STADI YA KUZUNGUMZA

ORIGINALITY REPORT

| 17% | 15% | 6% | 14% |
|---|---|---|---|
| SIMILARITY INDEX | INTERNET SOURCES | PUBLICATIONS | STUDENT PAPERS |

PRIMARY SOURCES

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Submitted to University of Rwanda<br>Student Paper | 5% |
| 2 | www.ajol.info<br>Internet Source | 2% |
| 3 | repository.out.ac.tz<br>Internet Source | 1% |
| 4 | Submitted to University Der Es Salaam<br>Student Paper | 1% |
| 5 | Submitted to The University of Dodoma<br>Student Paper | <1% |
| 6 | www.out.ac.tz<br>Internet Source | <1% |